

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Nne – Tarehe 3 Septemba, 2021

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA– KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

NAIBU SPIKA: Hati za kuwasilisha mezani, Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 *(The Accountants and Auditors (Registration) (Amendments), Bill, 2021)*.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, kwa niaba yake Mheshimiwa Jacqueline Kainja. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE A. KAINJA K.n.y. MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 (*The Accountants and Auditors (Registration) (Amendments), Bill, 2021*).

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Katibu.

NDG. EMMENUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali. Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Fatma Toufiq

Na. 40

Ujenzi wa Stendi - Chemba

MHE. FATMA H. TOUFIQ K.n.y. MHE. MOHAMED L. MONNI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga stendi katika Mji wa Chemba ambao unakuwa kwa kasi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu, Mheshimiwa Dkt. Dugange.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Mohamed Lujoo Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Wilaya ya Chemba kuwa na kituo cha kisasa cha mabasi. Kwa umuhimu huo Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Chemba imetenga eneo la ekari 22 kwa ajili ya ujenzi wa stendi kuu ya mabasi katika Mji wa Chemba ambayo imekadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi milioni 643.8 mpaka kukamilika kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ilitenga kiasi cha shilingi milioni 37 kutoka katika mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi hiyo ambapo ujenzi wa vyoo na ofisi za muda umekamilika kwa gharama ya shilingi milioni saba ili kuwezesha wananchi kuanza kupata huduma za stendi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi milioni 16 ili kuendeleza ujenzi wa stendi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa utekelezaji wa miradi ya kimkakati unahusisha andiko maalum la mradi linaloandaliwa na Halmashauri na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kufuata utaratibu huo ili Serikali itafute fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini kwa kuwa Mheshimiwa Rais alishatoa ahadi wakati wa kampeni mwaka 2020 na Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza kwamba ni mradi wa kimkakati.

Je, kwa kuwa ilikuwa ni ahadi ya Rais, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na jambo hili? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi stendi ya Chema ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na ahadi zote za viongozi zinatekelezwa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha na mipango inavyoandaliwa. Na katika jibu langu la msingi nimewaelekeza Halmashauri ya Chemba waandae andiko rasmi ambalo litawezesha sasa Serikali kuanza kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo wa kimkakati, lakini pia ambao pia ni ahadi ya viongozi wetu wa Kitaifa.

Kwa hiyo, niombe watekeleze utaratibu huo na Serikali iweze kuona namna ya kuanza kutekeleza mradi huu. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Bunda ni Halmashauri inayokua lakini pia ina *route* nyingi za usafiri ikiwepo kwenda Arusha, Mwanza na maeneo mengine, lakini stendi yake ni mbaya sana.

Ni lini sasa Serikali mtatusaidia hasa Halmashauri yetu changa kutujengea stendi ya kisasa na hasa ukizingatia Mji wa Bunda unakua? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Bunda ni Mji ambao unakua, una muingiliano mkubwa wa kibiashara, lakini pia una muingiliano wa magari yanayokwenda katika Mikoa mbalimbali, kwa hiyo, una kila sifa ya kupata stendi ya kisasa na mimi nichukue nafasi hii kwanza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalitambua hilo, lakini Serikali inalitambua hilo lakini Serikali ya Halmashauri kwa maana ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Halmashauri ya Bunda waanzishe utaratibu wa kufanya tathmini ya gharama ambazo zinahitajika kujenga stendi ile ili wawasilishe Serikalini na sisi tutafanya tathmini na kuona uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi ya Bunda. Nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Bunda Mjini.

Na. 41

Ahadi ya Mheshimiwa Rais ya Ujenzi Wa Barabara za Lami – Bunda

MHE. ROBERT C. MABOTO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano ya ujenzi wa barabara za lami katika Mji wa Bunda kwa kuwa mpaka sasa hauna barabara za lami?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu

swali la Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Bunda ina barabara za lami zenye urefu wa kilometa 2.22. Barabara hizi ni za Boma kilometa 1.36; Malugu kilometa 0.42; DC kilometa 0.24 na Posta kilometa 0.2. Barabara hizi zilijengwa kufuatia ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendelezaji Miundombinu katika Miji (*TACTIC*) unaotarajiwa kutekelezwa katika Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji 45 ikiwemo Halmashauri ya Bunda Mji. Programu hii itahusisha pia ujenzi wa barabara za lami katika Mji wa Bunda kwa kuzingatia vipaumbele vitakavyoainishwa na Halmashauri ya Bunda Mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itatekeleza ahadi zote za Rais zilizotolewa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano kama ilivyoahidiwa na Rais wa Awamu ya Sita Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan katika hotuba aliyotoa wakati akilihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, swali la nyongeza.

MHE. ROBERT C. MABOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ahadi ambazo Hayati Dkt. Magufuli aliahidi wakati wa kampeni ilikuwa ni pamoja na kujenga soko kuu la Mji wa Bunda pamoja na stendi mpya.

Je, kati ya stendi na soko kuu, ahadi hii yenyewe itatekelezwa lini? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKO ANA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Bunda Mji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba hapa nimeelezea kwa chini kwamba Serikali inaendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa *TACTIC*, uendelezwaji wa miundombinu katika miji yetu. Na ule uendelezwaji wa miundombinu kwenye *TACTIC* haihusu barabara peke yake, ni pamoja na masoko, stendi, madampo ya taka yaani tunatengeneza mji kuwa wa kisasa. Kwa hiyo, hata hiki anachokizungumza kuhusu soko kuu pamoja na stendi mpya katika Mji wa Bunda nafikiri itakuwa ndani ya *package* katika mradi huu wa *TACTIC* ambao mara utakapotekelezeka ni sehemu ya huo mradi, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, swali la nyongeza.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, sambamba na hilo swali la Mheshimiwa Robert Maboto nauliza je, ni lini Serikali itakamilisha lami kutoka Kinesi yaani Wilaya ya Rorya inayounganisha kutoka Rorya mpaka Tarime ambayo pia ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa wetu Hayati Magufuli? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, majibu kwa swali hilo.

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za viongozi wetu wakuu tutaendelea kuzitekeleza kulingana na fedha

itakavyopatikana ikiwa ni pamoja na hiyo barabara ya kutoka Rorya hadi Kinesi, ahsante.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini ambalo swali hilo litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

Na. 42

Fidia kwa Wakazi wa Mlima Nkongore

MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. MHE. MICHAEL M. KEMBAKI aliuliza:-

Serikali ilichukua eneo la Mlima Nkongore ambao ndani yake kulikuwa na makazi ya wananchi na kuliwekea *beacon* na kusababisha kaya zaidi ya 10 zilizochukuliwa maeneo hayo kuishi kwa hofu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzilipa fidia Kaya hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Dkt. Dugange majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mlima Nkongore uliopo katika Halmashauri ya Mji Tarime una eneo lenye ukubwa wa ekari 266.65. Wananchi wanaozunguka eneo hilo walikuwa wakiutumia Mlima Nkongore kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo ukataji kuni, uchomaji mkaa na kilimo kinyume na taratibu za Mamlaka ya Upangaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Mlima Nkongore ni moja ya eneo lililokuwa limekithiri kwa shughuli haramu ikiwemo kilimo cha bangi. Hivyo, mwezi Novemba, 2017 Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Tarime ilikabidhi eneo hilo kwa Jeshi la Magereza ili kuhakikisha kuwa eneo hilo linalindwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira Namba 20 ya mwaka 2004 kifungu cha 58(1) na (2) ambacho kinazuia kufanya shughuli zozote zinazoweza kusababisha hifadhi ya mlima kuharibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Tarime kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira inakamilisha taratibu za kulifanya eneo la Mlima Nkongore kuwa hifadhi. Hivyo, eneo la Mlima Nkongore litaendelea kuwa chini ya uangalizi wa Jeshi la Magereza hadi taratibu zitakapokamilika na kulitangaza kuwa eneo la hifadhi, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza; kwa kuwa eneo lote lile la mlima lilikuwa la kijiji na kwa kuwa sheria zetu za ardhi haziruhusu mtu kwenda kuvamia kijiji au Kamati ya Ulinzi kwenda kutwaa eneo la kijiji na kuligawia taasisi nyingine, ile ni mali ya wanakijiji.

Sasa ni lini taasisi hiyo iliyotwaa eneo la wanakijiji watalipa fidia ya kaya 10 ambazo zilikuwa zinafanya kazi pale? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa migogoro ya ardhi Mkoa wa Mara imekuwa mingi sana na hata juzi tumesikia Rorya pale kuna mtu amekufa kwa migogoro ya ardhi. Ni lini sasa Serikali itaenda kupima hasa

vijiji 30 vya Tarafa ya Chamriho, Jimbo la Bunda kuwapa Hati ya Kimila?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Getere kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza Sheria ya *National Environmental Management Act No. 20* ya 2004 hairuhusu maeneo yale ambayo ni hatarishi kama milima na maeneo ya kingo za mito kuweza kumilikiwa na wananchi, yanakuwa ni *protected* chini ya usimamizi wa Waziri wa Ardhi. Kwa hiyo, eneo la mlima analolizungumzia si halali kwa watu kumilikishwa pale na litabaki *under protection* kama ambavyo Kamati ya Usalama ya Wilaya imekwishaelekeza kuwapa watu wa Magereza kuliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusiana na vijiji 30 kuhusu suala zima la kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi; kama nilivyojibu juzi, ni suala tu la mamlaka yenyewe ya upangaji, pale watakapokuwa tayari sisi kama Wizara kupitia Tume ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi tutakuwa tayari kushirikiana nao kwa sababu kadri wanavyopima na kuweka mpango wa matumizi katika vijiji vyao, ndivyo jinsi ambavyo wanapunguza migogoro ya ardhi kwa watumiaji ardhi katika maeneo. Kwa hiyo, sisi tupo tayari wakati wowote pale ambapo Halmashauri itakuwa tayari kufanya kazi hiyo, waangalie kama bajeti wanayo, tutakwenda kuwasaidia, ahsante.

NAIBU SPIKA: Kuna swali ameuliza kuhusu kaya 10 kama zitalipwa fidia ama itakuwaje, hilo nani anajibu? Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika,

kwanza nilipata fursa ndani ya kipindi cha mwezi mmoja uliopita nilienda kutembelea eneo hilo na bahati nzuri tulikuwa na Mbunge husika na zile kaya tuliweza kuzibaini pale katika eneo lile. Tulichokifanya na Kamati ya Ulinzi na Usalama chini ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya tukasema kwamba wale ambao kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira maana yake hakuna *compensation* isipokuwa nini utaratibu wa busara ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo hilo tumeliacha chini ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, DC wetu wa Tarime linafanyiwa kazi lakini utaratibu wa kulitangaza eneo lile kuwa eneo lindwa, utaratibu huo kwa mujibu wa Kanuni zetu tunaenda kubadilisha Kanuni hivi sasa si muda mrefu tutatangaza baadhi ya maeneo likiwemo eneo la Mlima Nkongore, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, watu wetu wa Kumbukumbu Rasmi za Bunge mimi ni Naibu Spika jamani, Makamu wa Rais ni mtu mwingine kabisa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango. (*Makoff*)

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Hassan Sadiki Simai, Mbunge wa Nungwi sasa aulize swali lake.

MHE. SIMAI HASSAN SADIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza samahani kidogo kwenye jina, jina langu halisi ni Simai Hassan Sadiki.

Na. 43

Kuboresha Miradi ya *African Adaptation Program-Nungwi*

MHE. SIMAI HASSAN SADIKI aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kufanya mapitio kuimarisha miundombinu ya miradi ya maji ya *African Adaptation Program (AAP)* iliyojengwa kutokana na mabadiliko ya

tabianchi ili kuondokana na mahitaji makubwa ya maji kutokana na ongezeko la watu katika Jimbo la Nungwi?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa marekebisho hayo, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Chande, majibu

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya ufadhili wa Serikali ya Japan kupitia Shirika la Maendeleo la *UNDP* ilitekeleza mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kupitia *African Adaptation Program (AAP)* mwaka 2011 katika eneo la Nungwi, Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja na kufaidisha jumla ya watu 11,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ipo haja ya kufanya mapitio ya kuimarisha miundombinu ya miradi ya maji kupitia mpango wa *African Adaptation Program (AAP)* ili kukabiliana na mahitaji makubwa ya maji kutokana na ongezeko la watu katika Jimbo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeshaandaa mpango wa kuimarisha miondombinu ya maji katika maeneo mbalimbali Unguja ikiwemo eneo la Nungwi kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Usambazaji Maji Safi na Salama na Misingi ya Maji Machafu Zanzibar chini ya mkopo wa Benki ya Exim ya India. Katika mpango huo, matenki mawili ya zege yatajengwa, moja la lita 500,000 na lingine la lita 300,000 ambapo mtandao wa maji utakuwa na urefu wa kilometa 14. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki kutokea Msekwa swali la nyongeza

MHE. SIMAI HASSAN SADIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mabadiliko ya tabia ya nchi yanaendelea kuathiri vyanzo na miundombinu ya maji kule kijijini Nungwi jambo ambalo limepelekea kuwa na kero kubwa kwa Watanzania wanaoishi maeneo yale. Napenda kusikia kauli ya Serikali ni lini mradi huo unaozungumziwa hapa unatarajiwa kuanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Mheshimiwa Waziri ni lini atakuwa tayari kuongozana na mimi kwenda kuangalia moja kwa moja uhalisia wa athari ya mabadiliko ya tabia nchi?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kwa idhini yako nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Simai kwa juhudi yake ya kufuatilia miradi mbalimbali katika Jimbo lake ikiwepo miradi ya maji kwa kweli ni mwanaharakati mkubwa kufatilia maendeleo ya maslahi ya jimbo lake na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara tu baada ya utaratibu wa kifedha utakapokamilika mradi huu utaenda kutekelezwa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tupo katika harakati za kufatilia taratibu hizi za kifedha zikamilike ili kusudi kwenda kutekeleza mradi huo katika eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili mara tu baada ya kumaliza kikao hiki mwishoni mwa mwezi huu tutafuatana mimi na yeye twende tukaone athari hiyo ambayo inajitokeza ndani ya jimbo lake, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, pia Kumbukumbu Rasmi za Bunge zikae vizuri ni tabianchi sio tabia ya nchi. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Jesca David Kishoa Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 44

Kudhibiti Mapato Yanayotokana na Gawio

MHE. JESCA D. KISHOA aliuliza:-

Je Serikali inatumia mikakati gani kudhibiti mapato yatokanayo na gawio kutoka kwenye makampuni ambayo Serikali inamiliki hisa chini ya 50%?

NAIBU SPIKA: Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba majibu.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ambaye ndiye msimamizi wa uwekezaji wa Serikali katika Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na Kampuni ambazo Serikali ina hisa chache, inadhhibiti mapato yatokanayo na gawio kwa kuhakikisha kuwa kila kampuni ina sera ya gawio, kurejea kwa mikataba ya mauzo ya hisa katika kuhakikisha maslahi ya Serikali yanalindwa pamoja na kufanya chambuzi za mara kwa mara kuhusu utendaji wa taasisi hizo. Aidha, Serikali inauwakilishi kwenye bodi za wakurugenzi wa kampuni ambapo pamoja na mambo

mengine husimamia maslahi ya Serikali kwenye kampuni ikiwa ni pamoja na malipo ya gawio.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati hii imeiwezesha Serikali kuongeza makusanyo yake ya gawio kutoka kampuni ambazo ina hisa chache kutoka shilingi bilioni 34.92 mwaka 2015/2016 hadi kufikia shilingi bilioni 155.10 mwaka 2020/2021.

SPIKA: Mheshimiwa Jesca David Kishoa swali la nyongeza

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha uhalali wa magawio ambayo tunapewa kutoka kwenye makampuni haya Serikali haioni kama kuna haja ya ku-*list share* zake kwenye *stock market* ambako kule wanafanya *scrutiny* ya hali ya juu pamoja na kuweka hesabu wazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa maslahi mapana ya umma ni lini Serikali itaona ipo haja ya *CAG* kupewa mamlaka kisheria ya kuweza kufanya ukaguzi kwenye mashirika na makampuni hayo? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango majibu kwa maswali hayo

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mazuri ambayo yanaelezea mpango mbadala wa kuona namna gani *CAG* anaweza akakagua mashirika haya ambayo Serikali ina hisa chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na la kwanza la *listing of shares* nadhani kuna taratibu tu ambazo huwa tunafanya uchambuzi hata kwa mashirika haya ambayo Serikali ina hisa kubwa tunaangalia namna ambavyo yanaweza yakastahimili kwenye ushindani ule punde

watakapokuwa wameshaweka hesabu zao zote zikiwa sawa, kwa sababu kuna *implication* zingine za viashiria vya *performance* za mashirika ambavyo vinatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la *CAG* kuweza kukagua hata kwenye maeneo ambayo Serikali ina hisa chache nikiri tu kwamba hilo ni wazo jema na sisi kama Serikali tunaona tunapokwenda huenda kukawa na uhitaji huo kwa sababu utakubaliana na mimi kwamba hata juzi juzi tulibadilisha sheria kuweza kuiruhusu Serikali kuweka *guarantee* hata katika maeneo ambayo Serikali ina hisa chache, tukiwa tumeenda kwenye uchumi wa kisasa ama kwenye uwekezaji wa kisasa wa maeneo ambayo ni miradi mikubwa kama ilivyo kwenye bomba la mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo kwenye bomba la mafuta hata kama Serikali ina hisa chache lakini uwekezaji wake ambao Serikali inaweka unaweza ukawa mkubwa kuliko eneo ambalo Serikali ina hisa chache kwa maana hiyo kutakuwepo na *justification* ya kuona kwamba *CAG* anaenda kufanya ukaguzi kwenye maeneo ambayo Serikali imeweka uwekezaji na ni uwekezaji mkubwa licha ya kwamba inaweza ikawa nah isa chache.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza Mbunge wa Chumbuni sasa aulize swali lake.

Na. 45

Wanafunzi Wote wa Elimu ya Juu Kunufaika na Mkojo

MHE. USSI SALUM PONDEZA aliuliza:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati wa wanafunzi wote kunufaika kwa 100% bila kujali shule walizosoma?

(b) Je, Serikali inawasaidiaje wazazi waliostaafu ambao wameshindwa kuchangia gharama za elimu ya juu?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Jimbo la Chumbuni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo inayotolewa na Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo (SURA 178) ambayo inaelekeza kuwa walengwa wa mikopo hiyo ni wahitaji (*needy*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa uhitaji wa mwanafunzi hupimwa kwa kuchambua taarifa zilizowasilishwa wakati wa maombi ya mkopo, zikiwemo gharama za masomo ya sekondari au stahhada. Uchambuzi huu hutumia king'amua uwezo (*means testing tool*) ambacho hubaini kiwango cha uhitaji cha mwombaji mmoja mmoja ukilinganisha na wengine.

Aidha, uhitaji wa mnufaika unatumika kuamua kiasi anachopangiwa kulingana na gharama ya shahada aliyodahiliwa. Baada ya uchambuzi linganishi, waombaji hupangiwa mikopo kulingana na uhitaji wao. Katika mwongozo, vigezo na sifa za kunufaika na mikopo ya elimu ya juu, hakuna kigezo mahususi cha shule aliyosoma mwombaji na mnufaika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu waombaji wa mikopo ambao wazazi wao wamestaafu katika utumishi, Serikali inaamini utaratibu wa sasa wa kutambua na kuwapangia mikopo wahitaji wanaotoka katika familia zisizo na uwezo wa kumudu gharama za elimu ya juu kwa watoto wao unajitosheleza. Hata hivyo, Serikali ipo tayari kuendelea kupokea maoni ya namna ya kuboresha zaidi utaratibu huu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza swali la nyongeza.

MHE. USSI SALUM PONDEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana ningependa nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza ningependa kujua katika bajeti yao ya mwaka huu wa 2021 ni wanufaika wangapi ambao wataweza kunufaika na mikopo hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nilikuwa napenda niulize Serikali ina mpango gani wa kuwezesha wanafunzi ambao wako vyo vya kati ambao wale ndio wenye mahitaji makubwa zaidi ya hii mikopo?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia swali la nyongeza la kwanza kwa sababu linahitaji takwimu unaweza ukamjibu baadaye labda kama unazo hapo takwimu lakini majibu kwa swali la pili ikiwa swali la kwanza hauna takwimu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoeleza katika bajeti yetu wakati tunapitisha katika Bunge la Bajeti kwamba bajeti ya Bodi ya Mikopo imeweza kupanda kutoka shilingi bilioni 464 mwaka 2021 mpaka shilingi bilioni 570 mwaka 2122 na kwa hali hiyo basi wanufaika wa bodi watapanda kutoka 149,000 wale ambao walinufaika katika kipindi kilichopita mpaka kufika 160,000 katika mwaka 2021/2022 katika mchanganuo kwamba wale wanaoendelea 98,000 watakuwa wanaoendelea 62,000 tunakadiria katika watakaodahiliwa katika mwaka wa kwanza. Kwa hiyo kwa ujumla wao watakaonufaika tunakadiria kuwa watakuwa sio chini ya 160,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili amezungumzia kuhusiana na suala la wanafunzi wa vyuo vya kati. Kutokana na ufinyu wa bajeti yetu bado hatujaweza kuwafikia wanafunzi hawa wa vyuo vya kati kwa hiyo naomba tulichukue kama Serikali jambo hili wakati tunaboresha bajeti yetu kama Serikali, lakini ninyi Wabunge ndio ambao tunapitisha bajeti hapa, basi tunaweza kulileta mezani kwa ajili ya mjadala ili tuweze kuona namna gani tunaweza kuwafikia wale wa kada ya kati. Lakini kwa mujibu wa sheria sasa hivi bodi hii inashughulikia wale wa elimu ya juu peke yake, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nape Moses Nnauye swali la nyongeza.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya kugharamia elimu kutoka chekechea mpaka kidato cha nne na utaratibu unaofanywa na Serikali wa kutoa mikopo kwa elimu ya juu bado hapa vijana wa kidato cha tano na sita kuna tatizo la kugharamia elimu.

Ni lini Serikali itaweka sasa utaratibu ili kuwahusisha vijana wa kidato cha tano na sita katika utaratibu wa elimu bila malipo?

NAIBU SPIKA: Najaribu kutafakari kama hili litakuwa ni swali la Wizara hii au ni TAMISEMI. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia mikopo kwa kidato cha tano na sita.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimwa Naibu Spika, napenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Nape kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli vijana wetu wa kidato cha tano na sita wanatakiwa kugharamia kwa maana ya ada kwa wale wa kidato cha tao na sita ambao kwa

wanafunzi wetu wa bodi kulipa shilingi 70,000 na wale wa *day* kulipa shilingi 35,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii tunaiona kwamba ni *affordable* au inaweza sana Watanzania wengi kuilipa lakini kwa vile Mheshimiwa Mbunge amelezea hapa acha basi tulibebe jambo hili tuweze kwenda kuliangalia kwa kina kama Serikali, kwa vile Serikali sasa imeanza kutoa elimu bila malipo kutoka elimu ya awali mpaka kidato cha nne basi na hili tulingize kwenye mjadala tuweze kuliangalia katika kipindi kijacho kama tunaweza kama Serikali tukaweza ku-*wave* na kuweza kuondoa ada hii kwa upande wa kidato cha tano na sita, aHsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe swali la nyongeza

MHE. ALLY A. M. JUMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; Serikali kama kawaida imekuwa ikifanya kazi kubwa sana kwenye elimu. Sasa hivi imetokea wanafunzi wanaotoka kidato cha nne wanachaguliwa moja kwa moja kwenda kwenye vyuo.

Sasa nilitaka kuuliza na wengine hawana uwezo kabisa na wazazi wao wameshindwa kuwalipia na utakuta ana *division one* au *two*. Sasa nilitaka kuuliza je, Serikali inawasaidiaje hawa vijana ambao wanashindwa uwezo wa kwenda huko vyuoni kwa ajili ya kuwasaidia wafike huko vyuoni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimwa Naibu Spika, napenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Jumbe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jumbe anazungumza kwamba wapo wanafunzi ambao wanafaulu lakini nafasi za kujiunga kwenye elimu ya juu zimekuwa ni

changamoto na suala kubwa hapa ni kuweza kufanya upanuzi. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Jumbe na Wabunge wote kwamba tumesaini sasa mkopo kutoka Benki ya Dunia katika mradi wetu wa *HIT* ambao zaidi ya dola za Kimarekani milioni 425,000 ambazo zinakwenda kufanya upanuzi mkubwa pamoja na ukarabati wa miundombinu katika vyuo vikuu. Tutakapofanya ukarabati huu tunaamini tutaongeza nafasi za udahili na kuondoa changamoto hii ya wanafunzi wengi ambao wamefaulu vizuri lakini kuachwa kwenye vyuo vyetu. Nafasi hizo zitakapoongezeka tunaamini wanafunzi hawa wote ambao watakaofaulu wataweza kupata nafasi ya kwenda kuingia katika vyuo vyetu, asante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kutoka Msekwa swali la nyongeza.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini niseme ukweli kwamba mikopo inayotolewa ni mikopo na si zawadi. Sasa kuna kitu ambacho kimejitokeza kwamba watu wanaosoma shule binafsi au watoto wa watumishi wa Serikali hawapati mikopo huo ndio ukweli tusiseme uongo.

Je, wako tayari kama itajirudia tena hiyo kitu walete sheria Bungeni ibadilishwe ili itamke wazi kwamba watakaopewa mikopo ni watu waliosoma Serikalini na sio waliosoma kwenye shule za watu binafsi au watoto wa watumishi wa Serikali? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na napenda kujibu swali dogo la Mheshimiwa Ndakidemi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi mikopo hii inaratibiwa kwa ile Sheria Namba 178 ya Bodi ya Mikopo ambayo imebainisha vigezo na

vielelezo vya mwanafunzi gani na mwenye sifa zipi wa kupata mikopo hiyo na ambayo haibainishi kwamba amesoma shule gani na alikuwa analipa ada gani katika hizo shule za nyuma zilizopita. Lakini kwa vile yeye Mheshimiwa Mbunge amelieleza jambo hili hapa, tunalichukua tunakwenda kulifanyia kazi na kama kulikuwa na mchezo fulani ambao unachezwa nimwahidi tu kwamba katika kipindi hautatokea na mikopo hii itawafikia wote wenye uhitaji wa kupata mikopo hii.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 46

Kuanza Ujenzi wa Kiwanda cha Vifaa Tiba – Simiyu

MHE. LUCY J. SABU aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa kiwanda cha vifaa tiba vinavyotokana na zao la pamba Mkoani Simiyu utanza kwa kuwa upembuzi yakinifu ulishafanyika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda vya dawa hapa nchini ina jumla ya viwanda 17 ambapo viwanda 12 vinatengeneza dawa za binadamu, viwanda viwili vinatengeneza vifaa kinga na viwanda viwili vinatengeneza dawa za mifugo na kimoja vifaa tiba. Viwanda 17 hivyo vinauwezo wa kuzalisha dawa chini ya asilimia 12 tu ya dawa zote zinazohitajika nchini. Hivyo zaidi ya asilimia 88 ya dawa za binadamu zinazotumika zinaagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mkakati na mbinu za makusudi kuwezesha uwekezaji wa viwanda vya dawa vilivyopo na kuongeza ufanisi ili kufikia asilimia 60 ya uzalishaji wa dawa na vifaa tiba hapa nchini ifikapo mwaka 2025. Mikakati na mbinu hizo inahusisha pia kuongeza idadi ya viwanda vya vifaa tiba nchini. Aidha, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwenye sekta hiyo ili kuvutia wawekezaji wengine katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo, kuna umuhimu pia wa kuanzisha Kiwanda cha Vifaa Tiba Simiyu ambapo malighafi ya pamba inayolimwa kwa wingi nchini itatumika. Taratibu zote za kuanzisha kiwanda husika zimekamilika ikiwa ni pamoja na upembuzi yakinifu kama alivyobainisha Mheshimiwa Lucy John Sabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kiwanda hicho unategemea kuanza mara tu baada ya Serikali kukamilisha utaratibu bora wa kugharamia mradi huo. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Lucy John Sabu, swali la nyongeza.

MHE. LUCY J. SABU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninalo swali moja ambalo kwa kuwa *NHIF* na *WCF* walishaomba kibali hususani kwa ujenzi wa kiwanda hiki.

Ni lini sasa Serikali itatoa kibali cha ujenzi wa kiwanda hicho cha vifaa tiba Mkoani Simiyu? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kigahe, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Lucy John Sabu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilivyosema tayari mkakati huu wa kujenga kiwanda hicho upo na kweli

WCF na NHIF ndiyo walikuwa wamepewa kazi hiyo kujenga kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kamati Maalum ambayo inaratibu au inashughulikia sekta ya viwanda vya dawa na vifaa tiba ambao wanaendelea kuchanganua namna bora kama nilivyosema ya kutekeleza mradi huu. Kwa hiyo, kama nilivyosema tukishakamilisha taratibu hizo kiwanda hicho kitaanza kujengwa mara moja kupitia mifuko hii, lakini pia na MSD nao watashiriki kuhakikisha tunakidhi vigezo vya kutengeneza dawa zenye ubora unaotakiwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 47

Serikali kufufua Kiwanda cha *MUTEX* – Musoma Mjini

MHE. JULIANA D. MASABURI aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Kiwanda cha *MUTEX* kilichopo Wilaya ya Musoma Mjini kinafunguliwa na kurudisha ajira kwa vijana wa Mkoa wa Mara?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kigahe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina jumla ya viwanda 12 vya nguo na mavazi na viwanda vitatu kati ya viwanda hivyo havifanyi kazi ikiwemo Kiwanda cha *Musoma Textiles*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *MUTEX* ni moja kati ya viwanda vilivyobinafsishwa na Serikali kwa wawekezaji kwa lengo la kuviendeleza ili viweze kukuza sekta ndogo ya nguo na mavazi, kutoa ajira kwa wananchi, kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi na kuleta ustawi kwa jamii. Kiwanda hiki kimekuwa kinafanya kazi kwa kusuasua na mara kadhaa kimesimamisha uzalishaji. Kiwanda cha *MUTEX* ni moja kati ya viwanda 20 ambavyo vimerejeshwa Serikalini baada ya wawekezaji wa awali kushindwa kuviendeleza na kukiuka masharti ya mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya dhati ya Serikali ni kuona viwanda hivyo vinafanya kazi kwa tija na ufanisi mkubwa ili kuongeza ajira kwa ajili ya maendeleo ya watu, kuchochea shughuli za kiuchumi, na kuongeza mapato ya ndani ya nchi. Serikali imeshatoa Tamko la kuvitafutia wawekezaji wapya wa kuviendeleza kwa tija viwanda vyote vilivyorejeshwa Serikalini ili vilete manufaa kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Ni matumaini ya Serikali, kuona kuwa wawekezaji makini watajitokeza kwa lengo la kutumia fursa hii adhimu kuwekeza katika viwanda hivi. Serikali inaandaa utaratibu maalum utakaowezesha kupatikana wawekezaji wapya kwa njia ya zabuni ya kiushindani na wazi kwa kuzingatia vigezo vitakavyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha wawekezaji wenye nia na uwezo wa kuwekeza katika Kiwanda cha *MUTEX* na viwanda vingine vilivyorejeshwa Serikalini kuwasilisha maombi yao mara baada ya utaratibu utakapotangazwa rasmi. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi, swali la nyongeza.

MHE. JULIANA D. MASABURI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kuwashukuru Serikali kwa majibu yao mazuri, lakini je, Serikali imejipangaje hasa kuwachukulia hatua hawa wawekezaji ambao wanapewa hivi viwanda na wanavitelekeza na wanaenda mbali zaidi wanavichukulia

mikopo na kuviacha hapo? Serikali imejipangaje kisheria kuwabana aina hii ya wawekezaji? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza kuchukua hatua na ndiyo maana tumeona katika viwanda vile 68 ambavyo vilikuwa haviendelezwi tayari hivi 20 vimesharejeshwa Serikalini. Lakini pia tunaendelea kuvitathimini na hivyo vingine.

Kwa hiyo niwahakikishie watanzania na Mheshimiwa Juliana Masaburi na Wabunge wote kwamba Serikali ipo makini kuona sasa wawekezaji wote watakaolingia mikataba ya kuviendeleza viwanda katika sekta zote pale ambapo watakiuka masharti ya mikataba tutakayoingia nayo sheria zitachukuliwa na hatua mahsusi ikiwemo kuwanyang'anya viwanda hivyo vitachukuliwa ili kuhakikisha sasa tunapata wawekezaji makini ambao kweli wataleta tija katika uendelezaji wa sekta ya viwanda nchini. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, swali fupi la nyongeza.

MHE. VEDASTUS M. MATHAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kile Kiwanda cha *MUTEX*, Mheshimiwa Naibu Waziri amekubali kwamba aliyekuwa anakiendesha alinyang'anywa kwa sababu alikuwa hakiendesha kwa tija na sasa yapata ni miaka mitatu kile kiwanda kimesimama.

Je, ni kwanini basi hata huyo, huyo asingepewa akakiendeleza kuliko ambavyo sasa kile kiwanda kimesimama na watu wanakosa ajira?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ubinafsishaji wa viwanda hivi kulikuwa na mikataba na katika mikataba hiyo kulikuwa na vigezo maalum na ndiyo maana tuliona sasa katika kuvunjwa kwa mikataba hiyo ndiyo maana imechukua muda mrefu ili kujihakikishia, ilikuwa mojawapo ni kumshawishi yule aliyepo kuona kama anaweza kuendeleza, lakini baada ya kujiridhisha kwamba ameshindwa ndiyo maana vimerejeshwa Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kupata wawekezaji mahiri ambao kweli wapo makini na watawekeza kwa tija. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, kwanza tuna dhamira ya dhati ya kupata wawekezaji sasa mahiri ambao watawekeza katika viwanda hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tusingependa kuwaonea au kumpa mtu kwa upendeleo. Kwa hiyo tufuate utaratibu ambao utatangazwa na baadaye wawekezaji wengi watapatikana ambao watawekeza kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe kutoka Msekwa, swali la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala hili la viwanda tutakumbuka pia kulikuwa na viwanda vingi vya korosho vilivyopo maeneo ya kusini, Mtwara, Lindi, Masasi, Nachingwea na maeneo mengi. Serikali imesema imeamua kubinafsisha na kuna vingine vilikuwa vinatumika kama maghala ya kuhifadhia mazao badala ya kuviendeleza kuwa viwanda vya korosho ili kuweza kutoa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tusikie *commitment* ya Serikali, ni lini zoezi hili wanalolifanya litakamilika ili kuweza kuvirejesha hivi viwanda, watu muda sahihi wa kukamilisha? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil David Mwambe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kweli kuna viwanda vingi ambavyo vimekuwa havifanyi kazi baada ya wawekezaji wengi kuvitelekeza au kutokuviendeleza au kuendeleza kwa kusuasua au kubadilisha matumizi ya viwanda hivyo ikiwemo wengine waling'oa hata mitambo ya viwanda hivyo na kubadilisha kuwa ma-*godown*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge watuelewe kwamba Serikali ina nia ya dhati ya kuona sasa tunapata wawekezaji mahiri. Kwa hiyo hata viwanda vya korosho ambavyo vilikuwa vimetelekezwa kama nilivyosema tunaenda kutangaza utaratibu maalum wa kuweza kuwapata wawekezaji kwa njia ya wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya hapo naamini wengi ambao wana nia ya kuwekeza katika viwanda hivi watapatikana na hakika tunaamini viwanda hivi vitaenda kufanya kazi kwa tija kama ambavyo Serikali imekusudia. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mbunge wa Chake Chake sasa aulize swali lake.

Na. 48

Kulijengea Uwezo Jeshi la Kujenga Uchumi – Zanzibar

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wa kulisaidia kwa kulijengea uwezo Jeshi la Kujenga Uchumi la Zanzibar (JKU)?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, majibu kwa niaba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI K.n.y. WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mbunge wa Chake Chake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mashirikiano kati ya JKT na JKU yalianza mwaka 1975, kuanzishwa kwa JKU kutoka mfumo wa kambi za vijana ulioanzishwa tarehe 3 Machi, 1965 kwa sehemu kubwa kulitokana na mashirikiano hayo. Tangu wakati huo JKT na JKU wameendelea kubadilishana uzoefu katika maeneo mbalimbali ya kiutawala na uzalishaji mali na ndiyo maana JKU ina sura ya JKT. Mwaka 2001 iliundwa Kamati ya Mashirikiano yaliyopelekea kuwa na Katiba ya Mashirikiano ya mwaka 2007. Katiba hiyo pamoja na mambo mengine imeainisha vikao mbalimbali vya mashirikiano ikiwa ni pamoja na ratiba za vikao vya wakuu wa vyombo hivyo.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, swali la nyongeza.

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na majibu mazuri ya Serikali sitakuwa na swali la nyongeza.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, tunaenda kwenye swali la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 49

Gari Lililotolewa Kama Msaada kwa Serikali katika Kituo cha Polisi Gonja

MHE. ANNE K. MALECELA aliuliza:-

Je, Serikali ilishawahi kulifanyia matengenezo yoyote muhimu gari lililotolewa na Mbunge kutoka kwa wafadhili toka Japan na kupelekwa Kituo cha Polisi Gonja katika Jimbo la Same Mashariki mwaka 2015?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, swali la nyongeza. Aah, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba ama napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Same Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi cha Gonja kilichopo Wilaya ya Same kina gari namba PT 1988 *Toyota Land Cruiser*, ambalo lililetwa hapo mnamo mwaka 2015 ili kuhudumia wananchi. Mnamo tarehe 22 Juni, 2021 gari hilo lilisimama kufanya kazi ili kulinda usalama wa watumiaji na katika kulifanyia ukaguzi gari hilo lilikutwa lina ubovu wa mfumo wa usukani, mfumo wa *break, clutch plate*, mfumo wa umeme, *ball joints* na kuisha kwa matairi na *bush*. Aidha, tathmini ya matengenezo ya gari hilo ni shilingi 4,500,000 na

fedha za matengenezo zimeshaombwa kutoka Makao Makuu ya Polisi. Ninakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata majibu ya Serikali, lakini sina raha na haya majibu, naomba kuuliza maswali mawili.

Kwa kuwa wakati wa Bunge la Kumi nilishauliza hili swali mara mbili, kwa sababu hili gari limekuwa bovu kwa muda mrefu; je, Serikali mnavyonijibu leo mko *serious* kweli hili gari litatengenezwa na litatengenezwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, hivi Serikali inafahamu kwamba hiki Kituo cha Polisi kipo Mahore na Mahore ni tambarare na asilimia 68 ya wananchi wa Jimbo la Same Mashariki wanaishi milimani na kama kituo kile kinakuwa hakina gari wale wananchi hawana ulinzi na maisha yao.

Je, Serikali mnalijua hilo na kama mnalijua mtafanya jitihada ya kutengeneza hili gari? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa maswali hayo.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba gari hili ni bovu na ni kweli kwamba ni muda mrefu, lakini ni ukweli pia ambao Mheshimiwa Mbunge hajausema. Gari hili alipewa baada ya yeye kutoa gari kwa Jeshi la Polisi aliyekuwa amepewa msaada na wafadhili wake, kwa ajili ya kituo hiki. Sasa kwa sababu gari lile aliyekuwa la kwake aliyekuwa amepewa lilikuwa la kisasa sana ambalo kwa kweli

lisingeweza kupelekwa kule kijijini, Makao Makuu ya Jeshi la Polisi walilibakiza kwa ajili ya shughuli za Makao Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo hii Mbunge anaposikitika hivi mbele yako niseme tu kwa niaba ya Serikali na Wizara tutaitengeneza hili gari mapema iwezekanavyo ili kutoa heshima na shukrani kwa Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa nia njema tu ya kufanya ndugu zetu wale wa Same Mashariki, kule Mahore wapate huduma hii vizuri zaidi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa majibu hayo maana nilikuwa nashangaa hapa, Serikali inafanya mambo mazito sana kweli kuuliza swali la shilingi 4,500,000 humu ndani, nikawa nawaza imeshindikana vipi huko nje, lakini tunashukuru kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma Mbunge wa Mtoni, sasa aulize swali lake.

Na. 50

Kufunguliwa kwa Kituo cha Polisi cha Mtoni Zanzibar

MHE. ABDUL- HAFAR IDRISSA JUMA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukifungua Kituo cha Polisi cha Betrasi kilichopo katika Jimbo la Mtoni Zanzibar ambacho kimefungwa kwa zaidi ya mwaka sasa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI, alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrisa Juma Mbunge wa Mtoni Zanzibar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi cha Betراسي ni kituo kidogo cha polisi ambacho kilijengwa mwaka 1994 na kilikuwa kinafanya kazi kwa masaa 12, kutwa na kilikuwa kinawahudumia wananchi wa eneo la Mtoni na kilijengwa na mdau wa ulinzi kwa wakati ule Ndugu Noushad Mohamed. Kituo hiki kilifungwa mwaka 2018 kutokana na uhaba wa askari. Wananchi wa eneo hilo pia wanapata huduma za polisi katika Kituo cha Polisi cha Bububu na pindi pakipatikana ongezeko la askari kituo hicho pamoja na vituo vingine vya aina hiyo vitafunguliwa ili kuhudumia wananchi. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrisa Juma, swali la nyongeza.

MHE. ABDUL-HAFAR IDRISA JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya kuridhisha kiasi ya Naibu Waziri, lakini vitendo vya udhalilishaji na uhalifu katika Wilaya ya Magharibi "A" ambapo Jimbo langu la Mtoni lipo, lakini pia na kituo hicho cha polisi tunachokizungumzia kipo, vimekuwa vikiongezeka sana.

Sasa je, nini kauli ya Serikali katika wakati huu wa vitendo vikiongezeka na kituo kimefungwa nini kauli ya Serikali juu ya mapambano yake ama inafanya nini kuhakikisha kwamba vitendo hivi vya uhalifu na udhalilishaji unapungua?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa, Khamis Hamza Khamis, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrisa Juma, Mbunge wa Jimbo la Mtoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimuambie Mheshimiwa Abdul kwamba nipo tayari kufuatana na yeye kwanza kwenda kukiona kituo hicho, lakini pia nipo tayari kwenda kukaa na uongozi wa Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Mjini ili lengo na madhumuni kuweza kufanya nao

mazungumzo, ili ikiwezekana baada ya kujiridhisha tuone namna ambavyo tunaweza tukakifungua kituo hiki na kikaendelea kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nipo tayari kwenda kukaa na wananchi kuweza kuwaambia maneno mazuri ambayo yatawapa imani ya kuendelea kuwa amani na salama na utulivu katika Jimbo lao. Lakini kikubwa nimuambie kwamba hili suala lake aliloluliza la kuongezeka kwa matukio haya ya udhalilishaji katika Mkoa huu, katika Jimbo lake na katika Wilaya hii, Serikali tuna mipango mingi ambayo tumeshaanza kuifanya. Lakini kubwa nimuambie kwamba kwanza tunakwenda kuongeza nguvu kwenye masuala mazima ya ulinzi shirikishi. Ulinzi ambao unawapa nafasi wananchi wenyewe kushiriki katika ulinzi huu wa wananchi wao binafsi na hapa nataka nichukue fursa hii, nimpongeze sana Mheshimiwa Abdul-Hafar amekuwa anafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza amewatafutia kituo hawa walinzi shirikishi, lakini kubwa amewatafutia vifaa vya ulinzi kwa ajili ya kufanya doria zao. Lakini pia anafika wakati anawagawia hata posho ili lengo na madhumuni shughuli za ulinzi katika Jimbo lake ziendelee. Lakini kingine ni doria, misako na operesheni mbalimbali tunaziendesha katika Jimbo hili, ili lengo na madhumuni wananchi waishi kwa amani. Lakini kikubwa ziara za Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikoa tutajitahidi tuziongeze katika Jimbo hili na maeneo mengine ili lengo na madhumuni wananchi waweze kujua wajibu wao na waishi kwa ulinzi, amani na utulivu. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali fupi la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Niishukuru Serikali kwa mpango wake wa kujenga mahakama kule Mbulu, Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mbulu iko ndani ya hifadhi ya barabara ya mita 30 na kwa kuwa barabara hiyo ya kwenda Haydom

iko kwenye mpango wa kutangazwa *tender* kwa kiwango cha lami. Je, Serikali ni lini itakuja kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ili kuondoa kadhia hii ambayo itasababisha huduma kusimama?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa, Khamis Hamza Khamis, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia na ninajibu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali tunatambua changamoto ya ulinzi au changamoto ya ukosefu wa Kituo cha Polisi hilo eneo ambalo Mheshimiwa amelitaja, lakini kikubwa nimuambie kwamba moja ya miongoni mwa kazi kubwa ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inawapelekea wananchi huduma za ulinzi na usalama. Nimhakikishie mbele ya Bunge lako hili kupitia Wizara yetu, Kituo cha Polisi Mbulu kitafika na wananchi wataendelea ku-*enjoy* ama kupata huduma za ulinzi na usalama. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Shanif Jamal Mansoor, Mbunge wa Kwimba, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mbunge wa Sumve.

Na. 51

Ujenzi wa Barabara ya Hungumalwa - Ngudu - Magu

MHE. KASALALI E. MAGENI K.n.y. MHE. SHANIF M. JAMAL aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Hungumalwa - Ngudu hadi Magu kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shanif Mansoor Jamal, Mbunge wa Kwimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Hungumalwa – Ngudu hadi Magu ni barabara ya Mkoa yenye urefu wa kilometa 71. Barabara hii ni kiunganishi muhimu kati ya Wilaya za Kwimba na Magu kupitia Hungumalwa - Ngudu - Bukwimba hadi Isandula Wilayani Magu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ilikamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Hungumalwa – Ngudu – Bukwimba – Magu yenye urefu wa kilometa 71 mwaka 2019. Katika mwaka huu wa fedha wa 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 1,500 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, Serikali kupitia (*TANROADS*) inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka ambapo katika mwaka huu wa fedha jumla ya shilingi milioni 926.711 zimetengwa. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na majibu mazuri ya Serikali, kwa kuwa swali hili limeulizwa kwa muda mrefu, kuanzia katika Mkutano wa Tatu, ambapo Mheshimiwa Kiswaga na mimi Mbunge wa Sumve tuliuliza na tukapata majibu ya namna hii hii.

Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kulifanyia kazi jambo hili na kuanza taratibu za manunuzi ili barabara hii ijengwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa ujenzi wa barabara hii unaendana sambamba/unaathiriana na ujenzi wa reli ya kiwango cha *standard gauge* kutokea Isaka kwenda Mwanza kwa sababu, barabara hii kwa usanifu mpya inapita eneo tofauti na barabara iliyopo inapita na reli hii ikishajengwa, ina maana hakutakuwa na njia tena ya kupita kutoka Kwimba kwenda Magu.

Je, Serikali haioni sasa umefika wakati iharakishe ujenzi wa barabara hii, ili kuepuka kufunga njia ya kutoka Kwimba kwenda Magu? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mbunge wa Sumve kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii tuliyoitaja kwa kiwango cha lami. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii itajengwa na sisi kwa upande wa Wizara tayari tumeshakamilisha taratibu zote ili fedha itakapopatikana basi tuanze utaratibu wa kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa suala la barabara hii aliyoitaja kuingiliana na reli hii ya kisasa ya *SGR*, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, yote hayo yalizingatiwa kwenye usanifu na kwa hiyo, tumuhakikishie kwamba, hakutatokea hiyo changamoto anayoisema kati ya muingiliano wa hizo barabara na hiyo reli. Cha msingi tu avute subira kwamba wakati reli imeshaanza kujengwa hiyo

ya SGRkati ya Isaka na Mwanza, lakini fedha ikipatikana mara moja pia barabara hii itajengwa ili basi hii miundombinu yote iende sambamba kuyafungua hayo maeneo. Ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate.

Na. 52

Hitaji la Kituo cha Umeme – Tunduru

MHE. DAIMU I. MPAKATE K.n.y. MHE. HASSAN Z. KUNGU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Umeme Wilayani Tunduru chenye uwezo wa kupokea 132 KV ambazo ni uhitaji halisi kwa Wilaya ya Tunduru, Nanyumbu na Masasi?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato Rujwahuka, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme nchini (*TANESCO*) inaendelea na upembuzi yakinifu kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 132 kutoka Songea hadi Masasi kupitia Namtumbo, Tunduru na Nanyumbu umbali wa kilometa 395.

Mheshimiwa Naibu Spika, (*TANESCO*) pia inaendelea na taratibu za ujenzi wa Vituo vya kupoza umeme vya msongo wa kilovoti 132 kwenda 33 vya Namtumbo na

Tunduru Mkoa wa Ruvuma, pamoja na vituo vya Nanyumbu na Masasi Mkoa wa Mtwara. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza ifikapo Desemba, 2022 na kukamilika mwezi Desemba, 2023 na gharama ya mradi inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 132.7.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Moja ya changamoto inayosababisha Tunduru kukatika umeme mara kwa mara ni ubovu wa miundombinu ya kutoka Namtumbo kuja Tunduru na kutoka Tunduru kwenda Nanyumbu mpaka Masasi.

Je, Serikali haioni sasa ni muhimu kuweka nguzo za zege kutoka Namtumbo mpaka Tunduru na kutoka Tunduru mpaka Masasi ili kudhibiti uharibifu wa nguzo za umeme unaotokea mara kwa mara na kufanya umeme kukatika katika maeneo hayo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Steven Byabato Rujwahuka, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Daimu na muuliza swali mwenyewe Mheshimiwa Hassan, kwa nia ya kuendelea kuhakikisha kwamba miundombinu inaendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mkoa wa Ruvuma kwa mwaka huu wa fedha umetengewa shilingi 1,200,000,000 kwa ajili ya marekebisho ya miundombinu mbalimbali ya umeme ikiwemo nguzo, transfoma na waya. Lakini kabla sijasema kuhusiana na uwepo wa nguzo za zege kwanza niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote watusaidie katika kuhakikisha miundombinu yetu ya umeme inalindwa kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko huko Tunduru jana kuamkia leo na upo Mwenge, lakini wananchi wamechoma miundombinu ya umeme na kusababisha umeme kukatika katika maeneo hayo. Na ni kweli kwamba tunatoka kwenye nguzo za miti kwenda kwenye nguzo za zege kwenye maeneo yenye matatizo korofi. Maeneo ambayo kuna wadudu waharibifu kama mchwa, maeneo ambayo ni oevu yana majimaji, lakini pia kwenye maeneo ambayo ni ya kwenye hifadhi ambako hakuwezi kufikika mara kwa mara na wanyama waharibifu wanakuwa wanaiharibu ile miti yetu ya kushikilia umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye maeneo ambayo hayana matatizo hayo tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, waendeleo kuwa mstari wa mbele kuhamasisha ulinzi wa miundombinu yetu ili isiharibiwe.

Kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Daimu kwamba maeneo ambayo nimeyataja yanayohitaji nguzo za zege yatapelekewa nguzo za zege na tayari tumeshaanza. Wazabuni wanaotengeneza nguzo za zege tumeshawapata na kwenye baadhi ya maeneo kama mnavyoona Waheshimiwa Wabunge, tayari tumeshazipeleka na tutahakikisha miundombinu inaboreshwa zaidi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha tunamalizia swali la mwisho kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Jonas Vanzila ni Mbunge wa Mvomero sasa aulize swali lake.

Na. 53

Kuwaondoa Wanyama wakali katika Tarafa ya Mlali

MHE. JONAS V. ZEELAND: aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaondoa wanyama wakali hasa tembo katika Tarafa ya Mlali na kuwarudisha kwenye Hifadhi ya Taifa Mikumi kwa kuwa wamekuwa kero kwa wananchi?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa pole kwa wananchi wote wanaokutana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu hususan tembo. Wizara imeendelea kudhibiti wanyamapori hawa katika Wilaya ya Mvomero, Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kukabiliana na matukio haya, Wizara kwa kushirikiana na viongozi wa Mkoa iliweka mkakati wa pamoja ambapo kutakuwa na vikosi maalum vya kudhibiti tembo. Vikosi hivyo vimeendelea kutoa msaada wa haraka pale inapotokea tatizo katika Mkoa wa Morogoro na maeneo mengine ikiwemo Wilaya ya Mvomero. Vikosi hivyo vimewezeshwa kwa kupatiwa vitendea kazi muhimu vinavyohitajika katika zoezi la kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Vifaa hivyo ni pamoja na magari, risasi za moto, risasi baridi na mabomu maalum ya kufukuzia wanyamapori hususan tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na jitihada hizo, Wizara imenunua na kusambaza simu zenye namba maalum katika maeneo 14 nchini kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanatoa taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu, kwa haraka bila malipo na kwa wakati ili ziweze kushughulikiwa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, swali la nyongeza.

MHE. JONAS V. ZEELAND: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na niishukuru Serikali kwa majibu mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa tuna vijiji ambavyo vimepakana moja kwa moja na Hifadhi ya Mikumi. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuweka kila kijiji angalau kuwe na *game* ambaye ataweza kuzuia tembo mara tu anapotoka kwenye hifadhi na kutaka kuingia kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili, kwa kuwa tuna wananchi zaidi ya 28 wameshapoteza maisha kwa sababu ya tembo, lakini wananchi zaidi ya 2,000 mazao yao yameharibiwa na tembo.

Je, ni lini sasa Serikali itaenda angalau kuwafuta machozi na kuwafuta jasho kwa kupata uharibifu na tembo katika Wilaya yetu hii ya Mvomero? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Maliasili na Utali, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameomba kuwepo na askari maalum kwa ajili ya kuweka usalama wa wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi vikiwemo vijiji ambavyo amevielezea, nimuahidi tu Mbunge kwamba Serikali inatambua changamoto hii na ndio maana tumekuwa tukitoa ushirikiano wa karibu sana na wananchi kuhakikisha kwamba wananchi wanalindwa na mali zao pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba atuvumilie lakini tutaandaa eneo maalum kwa ajili ya kuweka askari *game* ambao watakuwa *standby* kwa ajili ya kufanya *patrol* katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tuna upungufu wa askari kwa maana ya kuweka kila Kijiji, nimuombe aendelee kutuvumilia, lakini tutahakikisha tunaimarisha eneo lile ili wanyama wakali na waharibifu wasiendelee kuvamia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kifuta machozi nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili Tukufu nitazunguka kwenye maeneo yote ambayo hayajapata kifuta machozi. Nimuahidi kwamba nitalisimamia zoezi hili mimi mwenyewe kuhakikisha kwamba wananchi wanalipwa kwa wakati. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Wabunge, lakini pia majibu kutoka upande wa Serikali.

Nilete matangazo niliyonayo hapa mezani na nina tangazo moja tu muhimu; kwanza wageni walioko hapa Bungeni, tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Spika kutoka Benki ya *NMB* ambao kwanza ni Ndugu Ruth Zaipuna ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu wa *NMB*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mkisikia Benki ya *NMB* inafanya vizuri mwanamama amekaa pale. Kwa hiyo, kama tunavyosema Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anafanyakazi nzuri, basi na wanawake walioko sehemu nzuri hivi wanamwakilisha vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na yeye ameongozana na Ndugu Filbert Mponzi ambaye ni Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, karibu sana; yupo pia Ndugu Juma Kimori ambaye ni Afisa Mkuu wa Fedha, karibu sana; ypo pia Ndugu Emmanuel Akonaay ambaye ni Afisa Mkuu Rasilimali Watu, karibu sana; yupo pia Ndugu Alfred Shao ambaye ni Afisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikalini, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Benedicto Baragomwa ambaye ni Afisa Mkuu Ukaguzi wa Ndani, karibu sana; Ndugu Kwame

Makundi - Kaimu Afisa Mkuu Teknolojia na Mabadiliko ya Kidijitali, karibu sana; yupo pia Ndugu Jerry Jumanne - Msaidizi wa Mwenyekiti wa Bodi, karibu sana; yupo pia Ndugu Vicky Bishubo ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Biashara za Serikali, karibu sana na tunaye pia Ndugu Nsolo Mlozi, ambaye ni Meneja wa Kanda ya Kati, karibu sana. *(Makofi)*

Sasa Afisa Mtendaji Mkuu wa *NMB* ukishasikia makofi mengi kwa Wabunge maana yake kijana wako Nsolo anafanya kazi nzuri ana mahusiano mazuri na Wabunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa sisi tunatamani aendelee kubaki, haya makofi yasiashirie kwamba aondoke Dodoma, labda kama anapanda cheo. *(Makofi)*

Lakini Ndugu Janeth Shango ambaye ni Meneja wa Kanda ya Kusini, karibu sana, tunaye pia Ndugu Donatus Richard - Meneja wa Kanda ya Dar es Salaam na Zanzibar, karibu sana, tunaye pia Ndugu Baraka Ladislaus - Meneja wa Kanda ya Ziwa, karibu sana, tunaye pia Ndugu Dismas Prosper - Meneja wa Kanda ya Kaskazini, karibu sana, Ndugu Sospeter Magesse - Meneja wa Kanda ya Magharibi, karibu sana, tunaye pia Ndugu Harold Lambileki - Kaimu Meneja wa Kanda ya Mashariki, karibu sana na tunaye pia Ndugu Vicent Mnyanyika - Meneja Mahusiano, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Amanda Feruzi huyu ni Meneja Mahusiano Mwandamizi, karibu sana, tunaye pia Ndugu Rumuna Kassim - Meneja Rasilimali Watu na tunaye pia Grace Matemtu ambaye ni Meneja wa Tawi la Bunge. *(Makofi)*

Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, Afisa Mtendaji Mkuu wa *NMB* umesikia makofi hayo ya Wabunge, maana yake Grace Matemtu anafanya kazi nzuri kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wabunge hawa huwa hawapigipigi hovyoy makofi, kwa hiyo, wanapiga wakiwa na uhakika na huduma. Huyu naye utuachie achie hapo hapo labda kama unampandisha

cheo, lakini akae hapo hapo aendelee kutuhudumia, ahsante sana Grace kwa huduma nzuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge huu ni uongozi wa *NMB*, ukiacha bodi hapa nchini uko Dodoma, kwa hiyo, mpate picha tukio ambalo alielekeza Spika, jana. Pamoja na kutangaza lakini alielekeza Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote kesho kushiriki kwenye zoezi ambalo naenda kulantangaza hapa na alitamani sana asiwepo Mbunge wa kukosa wala mtumishi wa kukosa, ndio maana hakuna semina imetangazwa hapa, tangazo ni moja nalo linalohusu tamasha la michezo kati ya *Bunge Sports Club* na Benki ya *NMB* na *NMB* yote iko Dodoma kwa ajili ya zoezi hili. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama alivyosema Mheshimiwa Spika, jana niwakumbushe, siku ya kesho ni siku ambayo kutakuwa na tamasha la michezo kati ya *Bunge Sports Club* na Benki ya *NMB*. Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba tamasha hilo litahusisha matembezi ya asubuhi yaani *jogging* kuanzia geti la Bunge kwenda viwanja vya Chinangali. Kwa hiyo, tutakutana geti kubwa hili linaloingilia Waheshimiwa Wabunge halafu tutakimbia mwendo wa upole, ama wengine mwendo wa kutembea mpaka chinangali tutaenda taratibu. Wale wenye vitambi kama mimi wasiwe na wasiwasi. Kwa hiyo, tutaanzia hapo mpaka Chinangali halafu tutakapofika huko, Chinangali, michezo ifuatayo itafanyika; mchezo wa mpira wa kikapu yaani *basketball*; mpira wa pete yaani *netball*; mpira wa wavu yaani *volleybal*, pamoja na kuvuta kamba yaani *tag of war*.

Baadaye muda wa mchana michezo ifuatayo itafanyika katika uwanja wa Jamhuri, nayo ni riadha; kufukuza kuku na mpira wa miguu.

Waheshimiwa Wabunge, na ninyi mnafahamu katika hii michezo sisi Wabunge ndio huwa tunaongoza, hakuna mchezo unaotushinda hapa. Kwa hiyo, viongozi wa *NMB* wajipange vizuri, Bunge tumejiandaa kuchukua kila kitu ikiwa pamoja na kuku kwa sababu humu ndani tunamfukuzaji wa kuku maarufu kabisa Mheshimiwa Saada, ndio huwa

anatuongoza huyu kwenye kukimbiza kuku. Kwa hiyo, hata kuku hamtaondoka naye. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia jioni baada ya hilo tamasha la michezo tutahitimisha na sherehe ya mchapalo katika viwanja vya Chinangali, hivyo Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa msikose kama alivyosisitiza Mheshimiwa Spika jana. *(Makofi)*

Sasa jana mliambiwa ni siku nzima kesho, siku nzima kwa maana ipi, yaani asubuhi tukitoka hapa na yale matembezi au mwendo wa pole wa kukimbia, tukifika kule Chinangali tutakutana na chai ya maana halafu baada ya michezo michezo ile ya asubuhi, nadhani kabla hatujaelekea Jamhuri basi tutakuwa tumeshashiba, tutakula huko huko. Halafu tukishatoka Jamhuri tumeshachukua yale makombe yetu na medali kwa wakimbaji basi tutaelekea Chinangali kula tena. Kwa hiyo, kesho mzime majiko kabisa jamani, msiwe na wasiwasi *NMB* wamejipanga vizuri kwa ajili yenu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, unapotoka nyumbani asubuhi, tafadhali toka na vitu vyote unavyovihitaji siku hiyo ikiwa ni pamoja na wale wachache wetu ambao huwa tuna dawa dawa zetu, utoke nazo usisahau nyumbani ili mambo yakae sawa kama Mheshimiwa Spika alivyosema. Kule msiwe na wasiwasi wale wala nyama wapo, wale waliokatazwa na daktari pia mambo yao yatakuwa mazuri msiwe na wasiwasi. Karibuni sana viongozi wa *NMB* Bungeni na tunawatakiya kila la heri katika siku ya kesho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama Mheshimiwa Spika alivyosema jana siku ya kesho ni mwanzo wa mchezo unaokuja baadaye tarehe 18 wa mbio yaani marathoni ambapo *NMB* imekusudia kukusanya fedha kwa ajili ya kuwasaidia akinamama wenye changamoto ya fistula. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote tujitoe kushiriki katika zoezi hili kwa sababu wananchi hawa wanaoenda kusaidiwa ni wananchi ambao ni wapiga kura wetu.

Kwa hiyo, wanawake tuliopo humu Bungeni kwa wingi wetu wote tushiriki katika hili zoezi zima, lakini pia kushiriki hizo mbio na kujiandikisha kwa sababu unakuwa na wewe umechangia ili mwanamke mmojawapo aweze kusaidiwa na kwa mwaka huu watawasaidia akinamama 60 ambao ni wapiga kura wetu.

Kwa hiyo, niwaombe na wababa pia mshiriki kwa sababu akinamama wasingepata hii changamoto bila mchango wenu. Kwa hiyo, na ninyi mshiriki kuhakikisha kinamama wanaondokana na hii changamoto.

Kwa hiyo, wanawake wa humu Bungeni tukiongozwa na Mheshimiwa Shally Raymond, Mwenyekiti wetu tuwashawishi Wabunge wanaume wajiandikishe kwa wingi ili na wao watoe mchango kwenye hili jambo muhimu kabisa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Baada ya kumaliza tangazo hilo muhimu Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu!

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu kwa mwaka 2021
(The Accountants and Auditors (Registration) (Amendment) Bill, 2021)

(Kusomwa Mara ya Pili)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita Waziri, nimeulizwa hapa asubuhi tunakutana saa ngapi, muda wa kukutana ni saa 12.00 asubuhi, matembezi yataanza saa 12.00 asubuhi.

Sasa nimuite Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ili aje awasilishe hoja mbele yetu.

WAZIRI WA FEHDA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa mwaka 2021 (*The Accountants and Auditors Registration Amendment, 2021*) pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhiti kwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka kwa kujadili kwa kina na kutoa ushauri kwa ajili ya kuboreshwa muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati na wadau mbalimbali kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao. Aidha, nitoe shukrani zangu za dhiti kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi wa Sheria, wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania yaani *NBAA* kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la muswada huu ni kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria ya Usajili ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Sura Namba 286 ili kuiwezesha Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (*NBAA*) kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hususani katika kusimamia tasnia ya uhasibu na wakaguzi wa hesabu. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

(a) Seti tofauti za taarifa ya hesabu za fedha; baadhi ya taasisi ama kampuni kupitia wakaguzi wao zimekuwa

zikiandaa seti tofauti za taarifa za hesabu za fedha kwa nia ya kupotosha usahihi wa taarifa hizo. Ili kukidhi matakwa tofauti ya wahusika, hali hii inaiokosesha Serikali mapato kwa kuwa baadhi ya seti hizi zinazojadiliwa zinahusisha kiwango cha faida ili makadirio ya kodi inayotakiwa kulipwa Serikalini yawe madogo.

(b) Viwango vidogo vya adhabu; viwango vya adhabu vilivyopo kwenye sheria ya sasa havilingani na ukubwa ama uzito wa kosa na hivyo kuchangia katika ukiukwaji wa viwango na miongozo ya uandaaji wa taarifa za hesabu za fedha. Ukiukwaji huu una madhara makubwa kwa Serikali na umma ikiwemo ukwepaji wa kodi na wananchi kupata taarifa potofu za mizania za kampuni zinazovutia uwekezaji kupia ununuzi wa hisa.

(c) Ukosefu wa kanzidata ya taarifa za hesabu; kuhusu hili *NBAA* kutokuwa na utaratibu wa uhifadhi wa taarifa za hesabu za fedha zilizokaguliwa na hivyo kuongeza vitendo vya kugushiwa kwa taarifa husika. Kwa kuwa vyombo vya Serikali vinakosa sehemu salama ya kuthibitisha uhalali wa taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kutokuwepo kwa masharti kwa kampuni za ukaguzi kuwasilisha *NBAA* taarifa za hesabu za fedha zilizokaguliwa. Jambo hili la kutokuwepo kwa utaratibu wa kuyalazimisha makampuni ya ukaguzi kupitia taasisi zao kuwasilisha *NBAA* taarifa za hesabu za fedha zilizokaguliwa kumesababisha kukosekana kwa kumbukumbu sahihi za taarifa hizo ili kufanya mapitia ya ulinganisho na zile zilizokaguliwa na zile zilizogushiwa pale inapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya marekebisho haya ni kuondoa upungufu ambao umebainika katika utekeleza wa baadhi ya masharti yaliyomo katika sheria husika ili kuendana na mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na kiteknolojia ambapo yamejitokeza katika miaka ya hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika muswada huu ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kuweka masharti kwa wakaguzi wa hesabu za fedha kuwasilisha *NBAA* taarifa ya hesabu za fedha walizozikagua kwa ajili ya kumbukumbu na rejea na kuruhusu mapitio pale inapohitajika.

(ii) Kuongeza adhabu na kuzifanya zienande na ukubwa wa makosa;

(iii) Kubainisha sifa za mtu anayefaa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa *NBAA* na majukumu yake;

(iv) Kubadili muundo wa Wajumbe wa Bodi ya Rufaa ya wahasibu na wakaguzi wa hesabu na kuainisha mamlaka yao ya uteuzi; na

(v) Kumpa Mkurugenzi Mtendaji wa *NBAA* mamlaka ya kufilisha makosa chini ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza, inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria hii na sehemu ya pili, ni kama ilivyorekebisha inapendekeza kufanya marekebisha kama ifuatavyo:-

(i) Kurekebisha kifungu cha 2 ili kufanya marekebisha ya kiuandishi, kuongeza na kuboresha tafsiri za maneno mbalimbali ambayo yametumika katika masharti ya sheria. Lengo la marekebisha haya ni kuhakikisha matumizi ya tafsiri sahihi ya masharti ya sheria na kuondoa mgawanyiko unaoweza kujitokeza wakati wa utekezaji wa sheria.

(ii) Kurekebisha kifungu cha 4 na 3 ili kupanua wigo wa majukumu ya bodi na kujumuisha baadhi ya majukumu ambayo yamekuwa yakitekelezwa na bodi lakini

hayajainishwa pamoja na kuainisha majukumu ambayo bodi haikukasimu kwa afisa au mtu yeyote. Aidha, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha sita ili kubainisha sifa za mtu anayeweza kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA.

(iii) Kuongeza kifungu kipya cha 6(a) ili kuweka mfumo madhubuti wa kudhibiti utoaji wa taarifa na kuweka masharti kuhusu usiri wa taarifa na kurekebisha kifungu cha 7 ili kuainisha utaratibu wa usajili wa wanachama na kuongeza makundi mapya ya wanachama kwenye sheria. Aidha, inapendekezwa kuweka masharti yatakatayotambua wahasibu na wakaguzi waliokuwa wametambuliwa na kusajili kabla ya sheria hii kuanza kutumika.

(iv) Kufuta vifungu namba 10, 11, 12, 13 na 14 kwa kuwa maudhui yake yamejumuishwa katika kifungu namba 7 kama inavyopendekezwa kurekebisha na Muswada huu. Lengo la marekebisho hayo ni kuwa na kifungu kimoja jumuishi ili utaratibu wa usajili na vigezo vya wanachama wote uainishwe kwenye kanuni. Aidha, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 18 ili kuweka masharti yanayohusu uhuishaji wa cheti cha utendaji kazi ili kuhakikisha kwamba wanachama waliosajiliwa wanajumuishwa katika kifungu hiki.

(v) Kurekebisha vifungu vya 27, 28, 29, 30, 31 na 42 ili kuongeza adhabu na kuzifanya ziendane na ukubwa wa makosa na hivyo kupunguza ukiukwaji wa sheria kwenye tasnia hii. Vilevile inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 24 na 25 ili kubadili muundo wa Wajumbe wa Bodi ya Rufaa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu na kuainisha mamlaka ya uteuzi pamoja na kuweka masharti kwa mwanachama ambaye hajaridhika na maamuzi ya Bodi ya Rufaa aweze kufuata utaratibu wa kimahakama.

(vi) Kurekebisha kifungu cha 26 kwa kukifuta na kukiandika upya ili kuleta maana iliyokuwa imekusudiwa. Aidha, kifungu cha 27(a) kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti ya utaratibu wa ukaguzi wa makampuni ya ukaguzi wa hesabu. Lengo la marekebisho haya ni

kuhakikisha kwamba makampuni yanatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti ya sheria husika.

(vii) Kuongeza vifungu vipya vya 30(a), (b) na (c) ili kuweka masharti kwa wakaguzi wa hesabu za fedha kuwasilisha kwenye bodi taarifa za hesabu za fedha walizokagua kwa ajili ya kumbukumbu na rejea, kuipa bodi mamlaka ya kufanya mapitio ya taarifa za hesabu za fedha zilizokaguliwa na kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa wanachama waliosajiliwa na kuainisha adhabu kwa wahasibu na wakaguzi watakaokiuka masharti hayo. Lengo la marekebisho hayo, ni kuhakikisha kuwa wahasibu na wakaguzi wa hesabu wanazingatia viwango na miongozo ya uhasibu inayoainishwa katika sheria wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

(viii) Kufuta vifungu vya 36 na 40 na kuviandika upya ili kuboresha masharti yanayohusu utaratibu wa uandaaji wa vitabu vya hesabu na ukaguzi kwa lengo la kuhakikisha kuwa masharti hayo yanaendana na Sheria ya Ukaguzi wa Fedha za Umma Sura 418. Aidha, kifungu cha 40(a) kinapendekezwa kuongezwa ili kubainisha mwaka wa fedha wa bodi.

(ix) Kuongeza kifungu kipya cha 42(a) ili kumpa Mkurugenzi Mtendaji mamlaka ya kufilisha makosa chini ya sheria hiyo. Lengo la marekebisho hayo ni kuokoa muda na gharama zinazohusiana na uendeshaji wa mashauri mahakamani. Vilevile inapendekezwa kuongeza kifungu kipya namba 48 ili kuweka masharti ya makosa ya jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu lijadili muswada huu na hatimaye kuridhia kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

No. 3

17th January, 2021

BILL SUPPLEMENT

to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.2. Vol.102 dated 17th January, 2021
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

THE ACCOUNTANTS AND AUDITORS (REGISTRATION)(AMENDMENTS) ACT, 2021

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Section Title

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Construction.

PART II
GENERAL AMENDMENTS

2. General amendments.
3. Amendment of section 2.
4. Amendment of section 4.
5. Repeal and replacement of section 6.
6. Addition of section 6A.
7. Repeal and replacement of section 7.
8. Repeal of sections 10, 11, 12, 13 and 14.
9. Amendment of section 18.
10. Amendment of section 21.
11. Repeal and replacement of section 24.
12. Amendment of section 25.
13. Repeal and replacement of section 26.
14. Amendment of section 27.
15. Addition of section 27A.
16. Amendment of section 28.
17. Amendment of section 29.
18. Amendment of section 30.
19. Addition of sections 30A, 30B and 30C.

20. Amendment of section 31.
21. Amendment of section 35.
22. Repeal and replacement of section 36.
23. Repeal and replacement of section 40.
24. Addition of section 40A.
25. Amendment of section 42.
26. Addition of section 42A.
27. Addition of section 48.

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dodoma,
13th January, 2021

JOHN W. H. KIJAZI
Secretary to the Cabinet

A BILL
for

An Act to amend the Accountants and Auditors (Registration) Act, Cap. 286 with a view to making better provisions for the regulation of accountants and auditors.

ENACTED by the Parliament of United Republic of Tanzania.

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

Construction
Cap. 286

1. This Act may be cited as the Accountants and Auditors (Registration) (Amendments) Act, 2021 and shall be read as one with the Accountants and Auditors (Registration) Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

PART II
GENERAL AMENDMENTS

General
amendments

- 2.** The principal Act is amended generally, by-
- (a) deleting the word “Registrar” wherever it appears in the Act and substituting for it the words “Executive Director”; and
 - (b) deleting the term “certified public accountant in public practice, certified public accountant, Graduate Accountant, Accounting Technician and practicing firm” wherever they appear and substituting for them the words “registered members”.

Amendment
of section 2

3. The principal Act is amended in section 2, by-

(a) deleting the definition of the terms “accountancy”, “accountant”, “auditor”, “Certified Public Accountant in Public Practice”, “Register” and “member” and substituting for them the following:

““accountancy” means a practice in which a professional accountant provides the measurement, recognition, preparation, analysis or disclosure of financial and relevant non-financial information or auditing of or provision of assurance and advisory services on financial information and, where applicable, non-financial information and preparing and analyzing tax information;

“accountant” means a person registered with the Board as a certified public accountant to perform accountancy functions;

“auditor” means a person registered as Certified Public Accountant in Public Practice, holding a valid practicing certificate issued under this Act to perform auditing functions;

“certified public accountant in public practice” means a person registered as such under section 7;

“Register” means a register of members and firms maintained by the Board in accordance with section 7;

“member” in relation to-

(a) the Board, means a member appointed pursuant to the First Schedule;

(b) a registered member, means a member registered by the

- Board in accordance with section 7; and
- (c) the Appeals Board, means a member appointed under section 24;"
- (b) inserting in their appropriate alphabetical order the following definitions:
- “audit firm” means an institution registered as such by the Board to provide audit services to a private or public entity;
 - “certified public accountant in training” means a person registered as such pursuant to section 7;
 - “registered member” means a person registered in any of the categories specified under section 7 of this Act;
 - “reporting entity” means an entity that prepares or is required to prepare financial statement;
 - “public interest entity” means a reporting entity with unique characteristics as shall be prescribed by the Board;
 - “standards” includes financial reporting standards, accounting standards, auditing standards, ethical standards, educational standards and any other standards issued by the Board;"
 - “tuition provider” means an institution accredited and registered by the Board to conduct review classes for candidates preparing to sit for the National Board of Accountants and Auditors (Tanzania) examinations; and
- (c) adding the words “or certified public accountant in public practice” at the end of the definition of the term “graduate accountant”.

Amendment
of section 4

- 4.** The principal Act is amended in section 4(1), by-
- (a) adding immediately after paragraph (j), the following:
 - “(k) supervise and regulate accountancy training conducted by the tuition providers;
 - (l) conduct audit quality review of accountancy and audit services;”;
 - (b) renaming paragraphs (k) and (l) as paragraphs (m) and (n) respectively.

Repeal and
replacement
of section 6

- 5.** The principal Act is amended by repealing section 6 and replacing for it the following:

“Appointme
nt of
Executive
Director

6.-(1) Subject to subsection (2), the Minister shall appoint the Executive Director of the Board on such terms and conditions as he may determine.

(2) A person shall be eligible to be appointed as Executive Director, if he-

- (a) is a holder of at least master degree in accounting, finance, management or economics;
- (b) has an accountancy professional qualifications obtained from recognized institution;
- (c) he is registered by the Board as a certified public accountant or certified public accountant in public practice; and
- (d) has at least ten years work experience out of which, eight years being in managerial position.

(3) The Executive Director shall be responsible to the Board for the administration and management of the functions and affairs of the Board.”.

Addition of
section 6A

- 6.** The principal Act is amended by adding immediately after section 6 the following:

“Disclosure
of
information

6A.-(1) A person who is or has been-

- (a) an employee of or a consultant employed by the Board; or

- (b) a member of the Board or committee established under this Act,

shall not disclose any information relating to the affairs of the Board or of any other person which he has obtained during the performance of his duties or the exercise of his functions under this Act, unless such disclosure is made-

- (a) with the written authorization of the person from whom the information was obtained;
- (b) in accordance with this Act or any other written law; or
- (c) in compliance with an order of the court.

- (2) A person who is or has been-

- (a) an employee of or a consultant employed by the Board; or
- (b) a member of the Board or of any committee established under this Act,

shall not, for his own personal benefit or benefit of any other person, make use of any information which has been obtained by him in the performance of his duties or the exercise of his functions.

(3) For the purposes of this section, “disclosure or making use of any information” includes permitting any other person to have access to any information relating to the affairs of the Board.

(4) Any person who contravenes this section commits an offence and shall, upon conviction, be liable to a fine of not less than two million shillings but not exceeding five million shillings or to imprisonment for a term of not less than one year but not exceeding three years or to both.”.

Repeal and replacement

7. The principal Act is amended by repealing section 7 and replacing for it with the following:

of section 7

"Registrat
ion of
members

7.-(1) Subject to the provisions of subsection
(2), a person shall upon-

- (a) payment to the Board of the prescribed fee;
- (b) making an application to the Board in the prescribed manner; and
- (c) meeting relevant qualification requirements specified pursuant to this Act,

be entitled to be registered under this Act and have his name entered in the Register as-

- (i) a graduate accountant or in the acronym "GA";
- (ii) a certified public accountant in public practice or in the acronym "CPA-PP";
- (iii) a certified public accountant or in the acronym "CPA";
- (iv) a certified public accountant in training;
- (v) an auditor for public interest entity;
- (vi) a practicing firm;
- (vii) a accounting technician or in the acronym "AT" ;
- (viii) a temporary certified public accountant or in the acronym "TCPA";
- (ix) a temporary certified public accountant in public practice or in the acronym "TCPA-PP";
- (x) a honorary member;
- (xi) a retired member; or
- (xii) any other category of members as may be determined by the Board.

(2) For the purpose of subsection (1), the Board shall, by by-laws published in the *Gazette* specify conditions and qualifications necessary for registration of each category under subsection (1).

(3) Notwithstanding the provisions of subsection (1), accountants and auditors who were

recognized and registered as such prior to 15th

January, 1972 shall, unless disqualified for any other reason under this Act, continue to be members registered under this section.

(4) A person registered under this section shall be issued with a certificate of registration.

(5) A person who does not qualify for registration under subsection (1) but who is an accounting or auditing personnel and has not completed relevant studies to qualify for registration, shall have a title in accordance with the prescription of titles as shall be issued by the Executive Director.

(6) The Executive Director shall keep and maintain a Register of registered members and firms in which shall be entered all categories of persons registered under this section.”.

Repeal of sections 10, 11, 12, 13 and 14
Amendment of section 18

8. The principal Act is amended by repealing sections 10, 11, 12, 13 and 14.

9. The principal Act is amended in section 18, by-

- (a) designating the contents of section 18 as subsection (1); and
- (b) adding immediately after subsection (1) as designated the following:

"(2) The certificate issued pursuant to sections 18 and 19 shall be valid for a period of twelve months and may, upon application in the prescribed manner and upon payment of fees prescribed by the Board, be renewed.

Amendment of section 21

10. The principal Act is amended in section 21(a) by deleting the words “registered accountant or auditor” and substituting for them the words “registered member”.

Repeal and replacement of section 24

11. The principal Act is amended by repealing section 24 and replacing for it with the following:

“Establishment of Accountants and

24.-(1) There is hereby established an appeals board to be known as the Accountants and Auditors Appeals Board

Auditors which shall consist of-

Appeals
Board

- (a) a Chairman who shall be appointed by the President from amongst retired judges or any person with qualifications which may warrant such person to be appointed as a judge; and
- (b) five other members appointed by the Minister as follows:
 - (i) a law officer representing the Attorney General, who shall be the Vice Chairman;
 - (ii) one senior member from the Ministry responsible for finance;
 - (iii) one senior member from the Bank of Tanzania;
 - (iv) one senior member from the Tanzania Revenue Authority; and
 - (v) two members with knowledge and practical experience in accountancy profession.

(2) The Accountants and Auditors Appeals Board shall have power to regulate its own proceedings."

Amendment
of section 25

12. The principal Act is amended in section 25(1) by deleting the words "and every order of the Appeals Board under this section shall be final, conclusive and binding upon all parties concerned, and shall not be subject to review by any court".

Repeal and
replacement
of section 26

13. The principal Act is amended by repealing section 26 and replacing for it the following-

"Use of
certain
styles and
titles

26. A person who is registered under this Act shall, in so far as his name remains in the Register, be entitled to adopt and to use the style and title specified under section 7."

Amendment
of section 27

14. The principal Act is amended in section 27, by-

(a) deleting paragraph (a) and substituting for it the following:

“(a) not being a registered member or firm falsely pretends to be a registered member or firm;”; and

(b) deleting the closing phrase and substituting for it the following:

commits an offence and shall on conviction, be liable-

(a) in the case of an individual person, to a fine of not less than five million shillings but not exceeding ten million shillings or to imprisonment for a term not exceeding two years or to both; and

(b) in the case of practising firm, to a fine of not less than five million shillings or ten percent of the firm’s gross revenue, whichever is greater, provided that the amount charged shall not exceed thirty million shillings.”

Addition of
section 27A

15. The principal Act is amended by adding immediately after section 27 as amended the following:

“Practice
review of
audit
firm

27A.-(1) For the purpose of enhancing audit quality, the Board may review the practice of any audit firm and for that purpose, the Board may-

(a) inspect any relevant document in the possession or under the control of the audit firm, make copies of or take any abstract of or extract from any document; and

(b) seek information or clarification from the audit firm.

(2) An audit firm shall, at the request of the Board, produce any relevant document in its possession or under its control for the purposes of subsection (1).

(3) Where the Board is satisfied that upon audit conducted the audited report does not meet the required standards, the Board may-

(a) order the audit firm to pay a fine of

not less than five million shillings
or ten percent of the firm's gross

revenue, whichever is greater, provided
that, the amount charged shall not
exceed thirty million shillings; or

(b) impose sanctions prescribed under
section 21."

Amendment
of section 28

16. The principal Act is amended in section 28-

(a) in subsection (5), by deleting the words "or approved
accountant" appearing at the end of that subsection;
and

(b) by deleting subsection (6) and substituting for it the
following:

"(6) A person who contravenes the
provisions of this section commits an offence
and shall, on conviction be liable-

(a) in the case of an individual person, to
a fine not exceeding ten million
shillings or to imprisonment for a
term not exceeding two years or to
both; and

(b) in the case of a practising firm, to a
fine of not less than ten million
shillings or ten percent of the firm's
gross revenue, whichever is greater,
provided that, the amount charged
shall not exceed twenty million
shillings."

Amendment
of section 29

17. The principal Act is amended in section 29-

(a) by deleting subsection (6) and substituting for it the
following:

"(6) Any person who contravenes the
provisions of this section commits an offence and
shall, on conviction be liable-

(a) in the case of an individual
person, to a fine of not
exceeding ten million
shillings or to imprisonment
for a term not exceeding
two years or to both; and

(b) in the case of a practising

firm, to a fine of not less than ten million shillings or ten percent of the firm's gross revenue, whichever is greater, provided that, the amount charged shall not exceed thirty million shillings."; and

(b) in subsection (9), by deleting the words "or the Tanzania Audit Corporation".

Amendment
of section 30

18. The principal Act is amended in section 30-

(a) in subsection (1)(a), by deleting the words "one hundred million shillings" and substituting for them the words "three hundred million shillings";

(b) in subsection (1)(b), by deleting the words "fifty million shillings" and substituting for them the words "one hundred and fifty million shillings";

(c) in subsection (2)(a), by deleting the words "one hundred million shillings" and substituting for them the words "three hundred million shillings";

(d) in subsection (2)(b), by deleting the words "fifty thousand million shillings" and substituting for them the words "one hundred and fifty million shillings"; and

(e) in subsection (3), by deleting the words "six hundred thousand shillings" and substituting for them the words "fifty million shillings".

Addition of
sections 30A,
30B and 30C

19. The principal Act is amended by adding immediately after section 30 the following:

"Submission
of audited
financial
statements

30A.-(1) Audited financial statements prepared under this Act shall be certified by a certified public accountant in public practice.

(2) Every auditor shall, within thirty days from the date of completion of the report, submit to the Board the auditee's audited financial statements and annual report.

(3) For the purpose of subsection (2), the Board shall establish a database for keeping the audited financial statements

submitted under this section.

(4) An auditor shall be responsible and accountable for financial statements audited and submitted by him to the Board under this section.

(5) A person who contravenes the requirements of this section commits an offence and shall, on conviction, be liable to a fine of not less than five million shillings but not exceeding ten million shillings or ten percent of the firm's gross revenue, whichever is greater, provided that, the amount charged shall not exceed thirty million shillings.

(6) For the purpose of this section, "auditor" includes an audit firm.

Board may
review
financial
statements
and reports

30B.-(1) The Board may, on its own motion or upon request by any user of the audited financial statements, review the audited financial statements and reports of a reporting entity submitted under section 30A.

(2) For the purpose of subsection (1), the Board may require production of further information or clarification from-

- (a) any officer or director of a public interest entity or other entities; and
- (b) any auditor or audit firm responsible for the audit of the financial statements of that entity.

(3) A person who refused to produce further information under this section, commits an offence and shall, on conviction, be liable to a fine not exceeding twenty million shillings or to imprisonment for a term not exceeding two years or to both.

Monitoring
of
registered
member

30C.-(1) For the purpose of ensuring compliance with the provisions of this Act, the Board shall monitor the conduct of any registered member and, for that purpose, the Board may seek information or clarification

from the registered member.

(2) A registered member who refused to provide information or clarification sought under this sections commits an offence and shall, on conviction, be liable to a fine of not exceeding five million shillings or to imprisonment for a term not exceeding two years or to both."

Amendment
of section
31

20. The principal Act is amended in section 31-

- (a) in subsection (1), by deleting the phrase "prepared or certified by a Certified Public Accountant or a Certified Public Accountant in Public Practice" and substituting for them the words "prepared by a Certified Public Accountant or certified by a Certified Public Accountant in Public Practice"; and
- (b) by deleting subsections (4) and (5) and substituting for them the following:

Cap. 212
“(4) Every audited financial statement of a body corporate required to be submitted to any public officer or public authority under the Companies Act or any other written law shall be certified by a certified public accountant in public practice.

(5) Any person who contravenes any of the provisions of this section commits an offence and shall, on conviction, be liable-

- (a) in the case of an individual person, to a fine of not less than five million shillings but not exceeding ten million shillings or to imprisonment for a term not exceeding two years or to both; and
- (b) in the case of practising firm, to a fine of not less than ten million shillings or ten percent of the firm's gross revenue, whichever is greater, provided that, the amount charged shall not exceed thirty million shillings."

Amendment
of section 35

21. The principal Act is amended in section 35, by-
(a) designating the contents of section 35 as subsection

(1); and

(b) adding immediately after subsection (1) as designated
the following:

“(2) Notwithstanding subsection (1), the
Board shall not delegate its powers to-

(a) invest, prescribe fees, charges and
commissions, borrow or lend money;
and

(b) issue final examination results, save
for provisional results.”.

Repeal and
replacement
of section 36

22. The principal Act is amended by repealing section 36
and replacing for it the following:

“Accou
nts and
audit

36.-(1) The Board shall keep proper
books of account, and shall prepare the annual
financial statements for the immediate preceding
financial year not later than the 30th day of
September in the following financial year in
accordance with the prescribed accounting
standards issued by the Board.

(2) The annual financial statements shall
be audited by the Controller and Auditor General
or an auditor appointed by the Controller and
Auditor General.

(3) The Board shall, as soon as possible
after receiving the audited report from the
Controller and Auditor General, submit to the
Minister the audited financial statements.”.

Repeal and
replacement
of section 40

23. The principal Act is amended by repealing section 40
and replacing it with the following:

“Annual
performanc
e report

40.-(1) The Board shall prepare and
submit to the Minister within four months after
the close of each financial year the annual report
on the performance of the Board during that
financial year.

(2) The Minister shall, at the earliest
available opportunity, cause a copy of the report
referred to under subsection (1) to be laid before
the National Assembly.”.

Addition of
section 40A

24. The principal Act is amended by adding immediately after section 40 the following-

40A. The financial year of the Board shall be the period of one year ending on the 30th June.".

Amendment
of section 42

25. The principal Act is amended in section 42-

(a) in paragraph (c), by deleting the words “knowingly and willfully makes” and substituting for them the words “makes or certifies”;

(b) deleting the closing phrase and substituting for it the following:

“commits an offence and shall, on conviction, be liable-

(a) in the case of an individual person, to a fine of not less than ten million shillings or to imprisonment for a term not exceeding two years or to both; and

(b) in the case of a practising firm, to a fine of not less than ten million shillings or ten percent of the firm’s gross revenue, whichever is greater, provided that, the amount charged shall not exceed thirty million shillings. ”.

Addition of
section 42A

26. The principal Act is amended by adding immediately after section 42 the following-

42A.-(1) Notwithstanding the provisions of this Act relating to penalties, where a person admits in writing that he has committed an offence under this Act or any other sector legislation, the Executive Director or a person authorised by him in writing may, at any time prior to the commencement of the proceedings by a court of competent jurisdiction, compound such offence and order such person to pay a sum of money not exceeding one half of the amount of the fine to which such person would otherwise have been liable to pay if he had been convicted

of such offence.

(2) Where the person fails to comply

with the compounding order issued under this section within the prescribed period, the Executive Director or a person authorised by him may, in addition to the sum ordered, require the person to pay an interest at the rate prescribed in the regulations.

(3) Where the person fails to comply with subsection (2), the Director may enforce the compounding order and interest accrued thereof in the same manner as a decree of a court.

(4) The Director shall submit quarterly reports of all compounded offences under this section to the Director of Public Prosecutions.

(5) Offences to be compounded under this section and the manner of compounding offences shall be as prescribed in the regulations made under this Act."

Addition of sections 48

27. The principal Act is amended by adding immediately after section 47 the following:

"General offence

48. A person who contravenes any of the provisions of this Act for which no specific penalty is provided, commits an offence and shall, on conviction, be liable to a fine of not less than five million shillings but not exceeding ten million shillings or to imprisonment for a term of not less than six months but not exceeding two years or to both."

OBJECTS AND REASONS

This Bill proposes to amend the Accountants and Auditors (Registration) Act, Cap. 286 in order to address some challenges which were encountered during its implementation.

This Bill is divided into Two Parts.

Part I deals with preliminary provisions.

Part II proposes general amendments by amending various provisions of the Act.

The Bill proposes to amend the Act by deleting the words "Registrar" and "certified public accountant in public practice, certified public accountant, Graduate Accountant, Accounting Technician and practising firm" wherever they appear in the Act and in their place introducing the use of the words "Executive Director" and "registered members". The aim is to recognize the position of the "Executive Director" which is reflected in the existing NBAA's Scheme of Service and use the word "registered members" rather than enlisting categories of members under the Act.

Section 2 is amended so as to improve the definitions of various terms used in the Act. The section is further amended by adding new terms that are necessary to be defined so as to enable smooth and correct interpretation of the provisions of the Act.

Section 4 is amended for purposes of widening the scope of functions of the Board and recognizing other functions which are performed by the Board but are not expressly provided under the Act.

Section 6 is proposed to be amended in order to clearly specify the qualifications for eligibility for appointment as the Executive Director of the Board. The aim is to ensure that the Executive Director is appointed from amongst persons with the necessary knowledge required to discharge duties efficiently and effectively. Furthermore, a new section 6A is introduced in order to prohibit unlawful disclosure of information.

Section 7 of the Act is amended so as to stipulate procedures for registration of members and to provide for new categories of registered members. It is further proposed to recognize the registration of accountants and auditors who were registered by the Board prior to the coming into force of the Act .

Sections 10, 11, 12, 13 and 14 are proposed to be repealed since their contents have been incorporated in section 7. Further, the Bill proposes to have a single provision for registration of all members whose qualification and registration process will be prescribed in the by laws.

Section 18 is proposed to be amended to provide for renewal of a practising certificate, and section 21 is amended so as to ensure that the provision is applicable to all registered members under the Act.

Sections 27, 28, 29, 30 and 42 are amended in order to increase the penalties provided in the Act proportional to offences committed. The aim is to increase compliance of the provisions of the Act.

Section 24 is proposed to be repealed and replaced. The aim is to change the composition of the members of the Accountants and Auditors Appeals Board and to provided for their appointing authorities. Section 25 is amended so as to provide an opportunity for any person who is aggrieved by the decision of the Appeals Board to seek remedy in court.

Section 26 is proposed to be rewritten for clarity purposes. Further, a new section 27A is proposed to be introduced in order to make provision for review of audit firms by the Board. The aim of the amendment is to ensure that the firms adhere to the provisions of the Act.

New sections 30A, 30B and 30C are proposed to be introduced so as to require accountants and auditors to submit audited financial statements to the Board for record and reference, to empower the Board to review audited financial statements and monitor the conduct of registered members and to provide for the penalty in case of non-compliance. The aim of the amendments is to ensure that accountants and auditors are accountable for the financial statements that they prepare or certify and that registered members comply with the standards prescribed in the Act.

Section 31 is proposed to be amended so as to enhance clarity of the provision and to increase the penalty provided for contravention of the provision.

Section 35 is proposed to be amended so as to limit the Board's power of delegation and clearly state the functions which the Board cannot delegate to any other person.

Sections 36 and 40 are proposed to be repealed and replaced in order to improve the procedures for preparations of books of accounts and audit so as to ensure compliance with the Public Audit Act, Cap. 418. Further, a new section 40A is proposed to be introduced in order to provide for the financial year of the Board.

The Bill proposes to introduce a new section 42A so as to empower the Executive Director or his authorised officer to compound offences under the Act. The proposed amendments aim at facilitating the reduction of costs and delay that result in the course of prosecuting cases in court.

Lastly, a new section 49 is proposed to be introduced in order to provide for general offences.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kurekebisha Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Sura ya 286. Lengo la marekebisho haya ni kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria hii.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Mbili.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo masharti mbalimbali ya Sheria yanavyopendekezwa kurekebishwa.

Sehemu ya Pili ya Muswada inahusu marekebisho ya jumla katika vifungu mbalimbali vya Sheria.

Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya jumla katika Sheria kwa kufuta neno "Msajili" popote lilipotumika kwenye Sheria na badala yake kutumia maneno "Mkurugenzi Mtendaji". Lengo la marekebisho haya ni kutambua cheo kinachotumika kwenye muundo wa Bodi. Aidha, inapendekezwa kutumia maneno "wanachama waliosajiliwa" badala ya kuorodhesha makundi yote ya wanachama wanaosajiliwa kama ilivyo sasa kwenye Sheria kwa urahisi wa rejia.

Kifungu cha 2 kinarekebishwa kwa kuongeza na kuboresha tafsiri za misamiati mbalimbali ambayo imetumika katika Sheria. Aidha, kifungu hiki kinaongeza misamiati mingine mipya ambayo ni muhimu kutafsiriwa kwa ajili ya kurahisisha ufasiri wa masharti ya Sheria hii.

Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa kwa madhumuni ya kupanua wigo wa majukumu ya Bodi na kutambua baadhi ya majukumu ambayo yamekuwa yakitekelezwa na Bodi lakini hayajaainishwa katika Sheria.

Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha sifa za mtu anayeweza kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa Mkurugenzi Mtendaji anateuliwa

kutoka miongoni mwa watu wenye sifa stahiki ili kuhakikisha kuwa majukumu ya Bodi yanasimamiwa na kutekelezwa na mtu mwenye sifa zinazohitajika. Aidha, kifungu kipyua cha 6A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka mfumo madhubuti wa kudhibiti utoaji wa taarifa na kuweka masharti kuhusu usiri wa taarifa.

Kifungu cha 7 kinarekebishwa ili kuainisha utaratibu wa usajili wa wanachama na kuongeza makundi mapya ya wanachama kwenye Sheria. Aidha, inapendekezwa kuweka masharti yatakayo watambua Wahasibu na Wakaguzi waliokuwa wametambuliwa na kusajiliwa kabla ya sheria hii kuanza kutumika.

Vifungu vya 10, 11, 12, 13 na 14 vinapendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui yake yamejumuishwa katika kifungu cha 7 kama kinavyopendekezwa kurekebishwa. Lengo la marekebisho hayo ni kuwa na kifungu kimoja jumishi kinachoweka utaratibu wa usajili na vigezo kwa wanachama wote, uainishwe kwenye kanuni za bodi.

Kifungu cha 18 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti yanayohusu uhuishaji wa cheti cha utendaji kazi (practising certificate), marekebisho haya yanaenda sambamba na marekebisho ya kifungu cha 21 ili kuhakikisha kwamba wanachama waliosajiliwa wanajumuishwa katika kifungu hiki.

Vifungu vya 27, 28, 29, 30 na 42 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza adhabu na kulingana na ukubwa wa makosa. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza utii wa Sheria na kupunguza utendaji wa makosa.

Kifungu cha 24 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya. Lengo ni kubadili muundo wa wajumbe wa Bodi ya Rufaa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu na kuainisha mamlaka yao ya uteuzi. Kifungu cha 25 kinarekebishwa ili kuweka masharti kwa mwanachama ambaye hajaridhika na uamuzi wa Bodi ya Rufaa kufuata utaratibu wa kimahakama.

Kifungu cha 26 kinarekebishwa ili kuhakikisha kuwa masharti ya kifungu hicho yanajumuisha makundi mapya ya wanachama. Aidha, kifungu kipyua cha 27A kinapendekezwa kuongezwa ili kuainisha masharti na utaratibu wa ukaguzi wa makampuni ya ukaguzi wa hesabu. Lengo la

marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa makampuni yanatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii.

Vifungu vipya vya 30A, 30B na 30C vinapendekezwa kuongezwa ili kuainisha masharti kwa wakaguzi wa hesabu za fedha kuwasilisha kwenye Bodi taarifa za hesabu za fedha walizokagua kwa ajili ya kumbukumbu na rejea, kuipa Bodi mamlaka ya kufanya mapitio ya taarifa za hesabu za fedha zilizokaguliwa na kufanya ufatiliaji wa mwenendo wa wanachama waliosajiliwa na kuainisha adhabu kwa wakaguzi na wahasibu watakaokiuka masharti hayo. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa wahasibu na wakaguzi wa hesabu wanazingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebisha kwa kukifanyia maboresho ya kiuandishi ili kifungu hicho kieleweke kwa urahisi na kuongeza adhabu ili iendane na ukubwa wa kosa.

Kifungu cha 35 kinapendekezwa kurekebisha ili kuainisha majukumu ambayo Bodi haitakasimu kwa afisa au mtu yeyote. Lengo ni kuhakikisha kuwa majukumu hayo yanatekelezwa na Bodi pekee.

Vifungu vya 36 na 40 vinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuboresha masharti yanayohusu utaratibu wa uandaaji wa vitabu vya hesabu na ukaguzi kwa lengo la kuhakikisha kuwa masharti hayo yanaendana na Sheria ya Ukaguzi wa Fedha za Umma, Sura ya 418. Aidha, kifungu kipya cha 40A kinapendekezwa kuongezwa ili kubainisha mwaka wa fedha wa Bodi.

Muswada huu unapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 42A kwa lengo la kumpa Mkurugenzi Mtendaji mamlaka ya kufililisha makosa chini ya Sheria hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kuokoa muda na gharama zinazohusiana na uendeshaji wa mashauri mahakamani.

Mwisho, kifungu kipya cha 49 ili kuainisha masharti ya makosa ya jumla.

Dodoma
11 Januari, 2021

PHILIP I. MPANGO
Waziri wa Fedha na Mipango

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO REMOVED BY HON. MWIGULU LAMECK NCHEMBA,
THE MINISTER FOR FINANCE AND PLANNING AT THE SECOND READING OF THE BILL
ENTITLED "THE ACCOUNTANTS AND AUDITORS (REGISTRATION) (AMENDMENTS)
ACT, 2021"**

(Made under S. O 99(10))

The Bill entitled "The Accountants and Auditors (Registration) (Amendments) Act" is amended as follows:

A: Generally by deleting the words "gross revenue" wherever they appear in the Bill and substituting for them the words "gross audit fee".

B: By deleting Clause 2 and substituting for it the following:

"General amendments **2.** The principal Act is amended generally by deleting the terms "certified public accountant in public practice, certified public accountant, graduate accountant, accounting technician and practising firm."

C: In Clause 3-

- (a) by deleting the word "accountancy" appearing in the opening phrase of paragraph (a);
- (b) by deleting the interpretation of the term "accountancy" appearing in paragraph (a);
- (c) in the interpretation of the term "certified public accountant in training" appearing in paragraph (b) by deleting the word "training" and substituting for it the word "academics";
- (d) in the interpretation of the term "standards" by deleting the words "accounting standards";
- (e) in paragraph (b) by inserting in its appropriate alphabetical order the following definition:

"“accountancy” means a practice in which a professional accountant provides the measurement, recognition, preparation, analysis or disclosure of financial and relevant non-financial information, or auditing of or provision of assurance and advisory services on financial information and, where applicable, nonfinancial information and preparing and analyzing tax information;”.

- D:** In Clause 4-
- (a) in paragraph (a), by-
 - (i) deleting the words “and audit” appearing in the proposed paragraph (l); and
 - (ii) adding immediately after the proposed paragraph (l) the following:
 - “(m) foster collaboration between the Board and other institutions dealing with accountancy services;”
 - (b) in paragraph (b) be deleting the words “(m) and (n)” and substituting for the them the words “(n) and (o)”.
- E:** In Clause 7, by deleting the word “training” appearing in the proposed clause 7(1)(iv) and substituting for it the word “academics”.
- F:** By adding immediately after Clause 7 the following:
- Amendment of section 9 **8.** The principal Act is amended in section 9(2) by inserting the words “Executive Director” between the words “hand of the” and “shall”.
- G:** In Clause 9 by deleting the words “twelve months” appearing in the proposed subsection (2) and substituting for it the words “three years”.
- H:** In Clause 11 by deleting paragraphs (b)(iv) and (v) appearing in the proposed section 24 and substituting for them the following:
- “(iv) one senior member representing higher learning institutions;
 - (v) two members from association representative of all accountancy professionals or private sector.”
- I:** In Clause 16 by deleting paragraph (a) and substituting for it the following:
- (a) by deleting subsection (5) and substituting for it the following:
 - “(5) Nothing in this Act shall be construed as entitling any body of persons, whether corporate or unincorporated, to be registered as, or as empowering the Executive Director to register any body of persons as, certified Public Accountant in Public Practice or Certified Public Accountants.”
- J:** In Clause 18-
- (a) in paragraph (a) by deleting the words “three hundred million shillings” and substituting for them the words “seven hundred million shillings”;
 - (b) in paragraph (b) by deleting the words “one hundred and fifty million shillings” and substituting for them the words “five hundred

million shillings”;

- K:** In Clause 19, by-
- (a) deleting the proposed subsection (1) and substituting for it the following:
“(1) Financial statements prepared under this Act shall be audited by a certified public accountant in public practice.”;
 - (b) deleting the word “refused” appearing in the proposed section 30B(3) and substituting for it the word “refuses”;
 - (c) deleting the word “refused” appearing in the proposed section 30C(2) and substituting for it the word “refuses”.
- L:** In Clause 20, by deleting the word “certified” appearing in the fifth line of paragraph (a) and substituting for it the word “audited”.
- M:** In Clause 23, by deleting the words “during that” appearing in the proposed section 40 (1) and substituting for them the words “for the previous”.
- N:** In Clause 26, by deleting the words “or any other sector legislation” appearing in the proposed section 42A (1).
- O:** By adding immediately after Clause 26 the following:
“Amendment **27.** The principal Act is amended in section of section 44 44 by-
- (a) deleting paragraph (c); and
 - (b) renaming paragraph (d) as paragraph (c).”
- P:** By renumbering Clauses 8 to 27 as Clauses 9 to 28 respectively.

Dodoma
3rd September, 2021

MLN
MoFP

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, karibu sana. *(Makofi)*

(Hapa kipaza sauti kilikuwa na hitilafu)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, subiri iwake kwanza halafu utaanza upya. Haiwaki? Hapana. Basi ukasomee kwenye kiti kwa sababu...

Ah, sasa ngoja kwanza, ngoja. Hapo wewe hujatumia hiyo *microphone* au ngoja tufanye marekebisho kidogo. Ngoja akusaidie, anaweza akasoma kwenye yake lakini hapo itamrahishia zaidi nafikiri. Kwa ajili ya nafasi, hii hapa. Subiri Mheshimiwa Kaboyoka, wataifanya mambo kidogo hapo. Mheshimiwa Mwaifunga hiyo sasa ni balaa. *(Kicheko)*

Karibu Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Hesabu za Serikali.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa mwaka 2021 *(The Accountants and Auditors (Registration) (Amendments) Acts, 2021)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi; naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa mwaka 2021

(The Accountants and Auditors (Registration) and (Amendments) Act, of 2021) kwa mujibu ya Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa mwaka 2021 ulisomwa Bungeni mara ya kwanza tarehe 12 Februari, 2021 katika Kikao cha Tisa cha Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Mbili.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) kilichosomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge uliuleta Muswada huo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati iliujadili muswada huu kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna uchambuzi wa muswada ulivyofanyika; hatua za kuufanyia kazi muswada huu zilianza kwa maandalizi mbalimbali ya kiutendaji yaliyofanywa na Sekretarieti kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati. Hatua hii ilijenga msingi wa utekelezaji wa kazi za Kamati kuhusiana na muswada huu ambapo utekelezaji wake ulikuwa kama ifuatavyo:-

(a) Maelezo ya uchambuzi wa Muswada uliofanywa na kuwasilishwa kwenye Kamati na Sekretarieti ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 21(2)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

(b) Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu madhumuni na sababu za muswada yaliyowasilishwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mbunge ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hapa niseme Waziri wa Fedha alipata darura hakuweza kutokea kwenye Kamati.

(c) Kupokea maoni ya wadau kwa mujibu wa kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Wadau waliofika

mbele ya Kamati ni hawa wafuatao ambao walikuwa saba; Chama cha Wahasibu Tanzania (*Tanzania Association of Accountants – TAA*); Ndugu Ludovick L. Utouh; Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (*NBAA*); Taasisi ya Uhasibu Arusha; Taasisi ya Uhasibu Tanzania; Kampuni ya Ushauri na Ukaguzi wa Hesabu ya *Ernest & Young* na Kampuni ya Ushauri na Ukaguzi wa Hesabu ya *KPMG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau wengine waliwasilisha maoni yao kwa maandishi ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *Institute of Internal Auditors, Delloite*, Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Kampuni ya Ushauri na Ukaguzi wa Hesabu ya *Price water House Coopers* na Kampuni ya Ushauri na Ukaguzi wa Hesabu ya *Barketilly*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine za utendaji kazi ya Kamati kuhusiana na muswada huu ni:-

(a) Uchambuzi wa Kamati wa kila ibara ya muswada kwa kuzingatia hoja zilizotokana na maelezo, uchambuzi, maoni pamoja na nyaraka mbalimbali kuhusiana na muswada huu.

(b) Majadiliano kati ya Kamati na Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba (Mbunge) kuhusiana na hoja zilizobainika kwa kila ibara ya muswada na kumshauri Waziri kufanya marekebisho katika ibara zilizoonekana kuhitaji marekebisho kwa mujibu wa Kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge; na

(c) Uandaaji ya Taarifa ya Kamati pamoja na kutoa Taarifa kwa Spika kwa mujibu wa kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri mahsusi kwa Kamati kuhusiana na muswada huo; muswada huu unalenga kufanya marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi, Sura ya 286. Sheria inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ilitungwa na Bunge kupitia Sheria Namba 33 ya mwaka 1972 ambapo ni

takribani miaka 49 iliyopita na imewahi kufanyiwa maboresho mara moja tu kupitia Sheria Namba 2 ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi, Sura ya 286 ina jumla ya vifungu 47 na Jedwali moja. Kupitia Muswada unaopendekezwa, jumla ya vifungu 23 vinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ambavyo ni takribani nusu ya vifungu vyote vya sheria hii na vifungu vipya nane vinapendekezwa kuongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa maudhui ya marekebisho hayo kwa kuzingatia changamoto ambazo mtoa hoja alieleza Kamati ambazo muswada huu umelenga kuzitatua pamoja na masuala mengine ambayo Kamati iliona yanafaa kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizo ni pamoja na:-

(a) Wakaguzi wa hesabu kuandaa seti tofauti za taarifa za hesabu za fedha kwa nia ya kupotosha usahihi wa taarifa hizo.

(b) Viwango vidogo vya adhabu vilivyopo kwenye sheria ya sasa ikilinganishwa na uzito wa kosa hali inayochangia ukiukwaji wa miongozo ya uandaaji wa hesabu; na

(c) Kutokuwepo kwa masharti kwa wakaguzi wa hesabu kuwasilisha taarifa za ukaguzi kwa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) na hivyo kusababisha kukosekana kwa kanzidata ya taarifa za hesabu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Taarifa yangu yote itaingia kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kamati imefanya uchambuzi wa mapendekezo yote ya marekebisho kwa kila ibara ya Muswada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 4 inayohusu Marekebisho ya Kifungu cha 4 cha Sheria; Ibara ya 4 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 4 kinachohusu majukumu ya *NBAA*. Muswada unapendekeza kuongeza wigo wa majukumu ya Bodi ili iweze kusimamia na kudhibiti mafunzo yanayotolewa kuhusu masuala ya hesabu pamoja na kufanya mapitio ya ubora wa ukaguzi wa hesabu. Majadiliano ya Kamati na Serikali yalifikia mwafaka wa kukubaliana na majukumu yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati iliishauri na kukubaliana na Serikali kufanya maboresho zaidi kwa kuongeza jukumu jipya litakaloiwezesha Bodi kushirikiana na taasisi nyingine zinazojihusisha na masuala ya uhasibu na ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya yataiwezesha *NBAA* kushirikiana na vyama na wadau wengine wanaohusiana na taaluma hii nchini kama vile Vyama vya Wahasibu Tanzania Bara na Zanzibar (*TAA* na *ZAA*) pamoja na taasisi nyingine zenye mrengo huo. Hatua hii itaiwezesha *NBAA* kubadilishana uzoefu na kupata namna bora zaidi ya kusimamia na kuiwezesha taaluma ya uhasibu nchini kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 9 inayohusu Marekebisho ya Kifungu cha 18 cha Sheria; Ibara ya 9 inayopendekeza marekebisho katika kifungu cha 18 kinachohusu utoaji na taratibu za cheti cha utendaji kazi. Ibara ya 9(b) ya muswada inapendekeza kifungu kipya cha 18(2) kinachopendekeza muda wa uhuishaji wa leseni kuwa ni kipindi cha miezi 12. Mapendekezo haya yanaenda sambamba na marekebisho ya kifungu cha 21 kupitia Ibara ya 10 ili kujumuisha wanachama ambao tayari wamesajiliwa. Kamati imeishauri na kukubaliana na Serikali kuwa muda huo uongezwe ili leseni za utendaji ziwe zinahuishwa kila baada ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya yamezingatia kuwa kipindi cha miezi 12 ni kifupi mno na

kuhuisha leseni kila baada ya muda huo mfupi itakuwa usumbufu kwa wanataaluma na utoaji wa huduma kwa ujumla. Aidha, mapendekezo haya yanaendana na uzoefu unaotumika katika usimamizi wa taaluma nyingine kama vile wahandisi na madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 inayohusu marekebisho ya Kifungu cha 24 cha Sheria; Ibara ya 11 inayopendekeza kufuta kifungu cha 24 kinachohusu uanzishwaji wa Bodi ya Rufaa ya Wahasibu na Wakaguzi na kukiandika upya kifungu hicho. Ibara hii inapendekeza kuboresha muundo wa Bodi ya Rufaa hususan kwa kupendekeza mtu anayeteuliwa na Rais kuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo awe Jaji Mstaafu au mtu mwenye sifa za kuwa Jaji. Kamati inakubaliana na mapendekezo haya lakini imeishauri Serikali kufanya marekebisho yafuatayo:-

(a) Kifungu cha 24(1)(b)(iv) kinapendekeza kuwa Mjumbe wa Bodi ya Rufaa kutoka Mamlaka ya Mapato; inapendekezwa kuwa, kwa kuwa tayari kuna mjumbe kutoka Wizara ya Fedha, ni vyema badala ya mjumbe kutoka *TRA*, nafasi hiyo ateuliwe Mjumbe kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu.

(b) Kifungu cha 24(b)(v) kiboreshwe ili kujumuisha wajumbe wanaoteuliwa kutokana na mapendekezo ya wawakilishi wa vyama vya wahasibu na wakaguzi, wawakilishi kutoka sekta binafsi au asasi za kiraia wenye ujuzi na uzoefu katika masuala ya uhasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 14 inayohusu Marekebisho ya kifungu cha 27 cha sheria; Ibara ya 14 inapendekeza kufanya maboresho katika kifungu cha 27 kwa kuboresha adhabu kwa watu wanaofanya udanganyifu kana kwamba wao ni wahasibu au wakaguzi waliosajiliwa. Muswada unapendekeza kuongeza adhabu kutoka faini isiyozidi shilingi laki sita au kifungu kisichozidi miaka miwili au zaidi hadi faini isiyozidi shilingi milioni tano na isiyozidi asilimia kumi ya mapato ghafi lakini faini hiyo haipaswi kuzidi shilingi milioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo vya udanganyifu vinafanywa na wahalifu wasiokuwa na sifa katika taaluma husika almaarufu makanjanja au vishoka ambavyo athari zake kwa Taifa na umma ni kubwa. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuongeza adhabu lakini Kamatii inapendekeza adhabu hizo ziboreshwe zaidi kwa kuongeza adhabu ya kutwaa (*forfeiture*) mapato yote yatakayokuwa yamepatikana kutokana na udanganyifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo hili lizingatiwe pia katika Ibara ya 16 ya Muswada inayopendekeza marekebisho katika kifungu cha 28 cha sheria kuhusiana na udanganyifu. Aidha, adhabu za faini zinazopendekezwa ziboreshwe ili ziwiane na kiasi cha mapato kitakachokuwa kimepatikana kwa njia ya udanganyifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 15 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 27A; Ibara ya 15 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 27A kinachoipa NBAA mamlaka ya ukaguzi wa utendaji kazi wa makampuni ya ukaguzi wa hesabu. Kamati inakubaliana na pendekezo katika ibara hii ambayo inaeleza kuwa Bodi inaweza kufanya mapitio ya utendaji kwa kampuni yoyote ya ukaguzi ili kuboresha kazi za ukaguzi. Katika kutekeleza hilo, Bodi inaweza kukagua nyaraka zozote zinazohusika zilizopo kwenye usimamizi wa kampuni, kutoa nakala au kuchukua sehemu ya nyaraka hizo. Aidha, Bodi inaweza kuomba taarifa zaidi au ufafanuzi wa jambo fulani kutoka kwenye kampuni ya ukaguzi na kampuni husika itawajibika kiutekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo zaidi katika ibara hii yanaipa mamlaka NBAA kuamuru kampuni ya ukaguzi kulipa faini endapo NBAA itajiridhisha kuwa taarifa ya ukaguzi iliyoandaliwa na kampuni hiyo haijafikia viwango vinavyotakiwa. Faini hiyo ni kiasi cha fedha kisichopungua shilingi milioni tano au asilimia 10 ya mapato ghafi ya kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kamati kuwa adhabu hii ni kubwa mno kwa kuzingatia kuwa inahusisha moja kwa moja na utendaji kazi wa kila siku wa wanataaluma

hawa. Hivyo Kamati ilishauriana na kukubaliana na Serikali kufanya maboresho katika mapendekezo haya ya adhabu kwa kuweka faini isiyozidi asilimia kumi ya mapato yaliyotokana na kazi iliyobainika kutofikia viwango vya ukaguzi vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 17 inayohusu marekebisho ya kifungu cha 29 cha sheria; Ibara ya 17 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 29(6) kinachozuia mtu yeyote kuajiri mtu ambaye hana sifa za masuala ya uhasibu kwa kukifuta na kukiandika upya kwa lengo la kuongeza faini. Sheria ilivyo hivi sasa inaeleza kuwa mtu yeyote atakayeajiri mtu ambaye hana sifa za masuala ya ukaguzi atakuwa ametenda kosa na endapo atatiwa hatiani atahukumiwa faini isiyozidi shilingi 750,000 au kifungu kisichozidi miaka mitano au adhabu zote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, muswada unapendekeza kurekebisha adhabu hii kwa kuongeza faini kuwa ni kiasi kisichozidi shilingi milioni kumi au kifungu kisichozidi miaka miwili au vyote kwa mtu binafsi na ikiwa ni kampuni ya ukaguzi, kampuni hiyo itatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichozidi shilingi milioni kumi au asilimia kumi ya mapato ghafi ya kampuni au itakayokuwa kubwa zaidi isipokuwa kiasi hicho hakitazidi shilingi milioni thelathini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo haya lakini ilishauriana na kukubaliana na Serikali kuwa kufanya maboresho zaidi katika faini inayoihusu kampuni ili faini hiyo iwe ni asilimia 10 ya ada ghafi ya ukaguzi (*gross audit fee*) badala ya mapato ghafi ya kampuni (*gross revenue*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 18 inayohusu marekebisho ya kifungu cha 30 cha sheria; kifungu cha 30 cha Sheria kinaweka ulazima wa mtu yeyote au kampuni inayofanya biashara au kazi yoyote ya kitaaluma hapa nchini na yenye mali au mapato ghafi yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria kuajiri mhasibu aliyesajiliwa na bodi ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa za hesabu. Marekebisho

yanayopendekezwa katika kifungu hiki yana lengo la kuongeza kiwango cha mali au mapato ghafi ambacho kinatumika kama kigezo cha kuajiri mhasibu aliyesajiliwa na bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, muswada unapendekeza kubadilisha kiwango hicho kwa kigezo kwamba, mtu yeyote au kampuni inayofanya biashara au kazi yoyote ya kitaaluma italazimika kuajiri mhasibu liyesajiliwa na bodi pamoja na kuandaa taarifa za hesabu kwa kuzingatia thamani ifuatayo:-

(a) Kuhusu thamani ya mali itakayozingatiwa, badala ya shilingi 100,000,000 za sasa, thamani ya mali itakayozingatiwa iwe ni shilingi 300,000,000; na

(b) Kuhusu mapato ghafi kwa mwaka yatakayozingatiwa, badala ya shilingi 50,000,000 za sasa, mapato yatakayozingatiwa yawe ni shilingi 150,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikubaliana na pendekezo la Serikali lakini bado ilikuwa na maoni kuwa kiwango kilichoboreshwa ni kidogo mno kwa kuzingatia hali halisi ya biashara na ujasiriamali nchini, mathalani, wajasiriamali wengi hivi sasa wanafanya shughuli zao katika maeneo ya katikati ya miji au maeneo yenye wakazi wengi ambapo thamani ya mali ni kubwa sana ikilinganishwa na mapato yanayotokana na shughuli hizo. Wengi wa wajasiriamali au wafanyabiashara wanafanya shughuli zao katika majengo yenye thamani kubwa, lakini mapato ni madogo kwa kiasi cha kuweza kuajiri watu wengine zaidi ya wale wanaojihusisha moja kwa moja na shughuli za uzalishaji. Hivyo, kuwalazimisha kuajiri mhasibu aliyesajiliwa na bodi itakuwa mzigo ambao unaweza kusababisha kufungwa kwa biashara ama za tozo vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kamati ilishauriana na Serikali na kukubaliana kuboresha vigezo hivyo kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusu thamani ya mali itakayozingatiwa, badala ya shilingi 100,000,000 za sasa, thamani ya mali itakayozingatiwa iwe ni shilingi 700,000,000; na

(b) Kuhusu mapato ghafi kwa mwaka yatakayozingatiwa, badala ya shilingi 50,000,000 za sasa, mapato yatakayozingatiwa yawe ni shilingi 500,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati Ilishauriana na kukubaliana na Serikali kuwa ibara nyingine zibaki kama zilivyo kwenye muswada kwa misingi iliyofafanuliwa kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa jumla wa Kamati; pamoja na maoni na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa katika kila ibara ya muswada, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla ambao ni vyema Serikali ikauzingatia na kuufanyia kazi kwa kuwa ni masuala yanayohusiana na utungaji wa sheria na taaluma ya uhasibu nchini kama ifuatavyo:-

4.1 Inapotokea Serikali inakusudia kuwasilisha Muswada Bungeni, endapo sheria ina vifungu vingi ambavyo vinakusudiwa kufanyiwa marekebisho kwa wakati mmoja ni vema Serikali ikatumia utaratibu wa kuifuta na kuiandika upya sheria hiyo. Utaratibu huu utaliwezesha Bunge kuifanyia kazi sheria hiyo kwa ufanisi zaidi ikilinganishwa na inapowasilishwa kwa utaratibu wa marekebisho.

4.2 Kuna umuhimu wa kutenganisha majukumu ya taasisi inayohusika na udhibiti wa sekta/taaluma na ile inayohusika na wanachama kwa kuunda chombo cha usimamizi (*Public Oversight Body*).

4.3 Muswada haujaweka masharti kuhusu usimamizi wa wakaguzi wanaofanya kazi chini ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hivyo, inashauriwa suala hili liangaliwe kwa undani zaidi.

4.4 Ni vema Bodi zote za Wakaguzi za mashirika yote ya umma kuwa na angalau mhasibu mmoja ambaye atasaidia kutoa ushauri kuhusiana na masuala ya usimamizi wa fedha.

4.5 Uanzishwe mkakati mahsusi wa kupitia sheria zote zinazohusiana na taaluma mbalimbali nchini ili kujiridhisha kama maslahi ya umma yamezingatiwa ipasavyo katika sheria hizo.

4.6 Serikali iweke utaratibu wa wanachama wa Chama cha Wahasibu Tanzania Bara (*Tanzania Accountants Association - TAA*) na Chama cha Wahasibu Zanzibar (*Zanzibar Accountants Association - ZAA*) wa kuweza kufanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; naomba kutumia fursa hii kukushukuru wewe pamoja na Spika kwa namna ya kipekee kabisa kwa kuuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa mwaka 2021 katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Kusema kweli, kwa mara ya kwanza mimi na Kamati yetu tumepata uzoefu mpya katika kazi ya kulisaidia Bunge lako Tukufu kutekeleza mojawapo ya majukumu ya msingi ya Bunge ya utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali na hasa Makamu wangu ambaye alinisaidia sana kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutambua majina yote na ninaomba majina yao yote yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelewa Mwihambi kwa ushauri wake kwa Kamati pale alipotakiwa kufanya hivyo. Natoa shukrani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati kupitia kwa Mkurugenzi Ndugu Athuman Hussein,

Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wetu wa Kamati Ndugu Erick Maseke na Ndugu Wilfred Magova pamoja na Maafisa wa Sheria walioishauri Kamati Ndugu Stephano Seba Mbutu na Ndugu Rehema Lazarus Kipera.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo za kipekee, naomba sasa nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa mwaka 2021 mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.
(Makofi)

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
HESABU ZA SERIKALI (PAC) KUHUSU MUSWADA WA SHERIA
YAMAREKEBISHO YA SHERIA YA USAJILI WA WAHASIBU NA
WAKAGUZI WA HESABU WA MWAKA 2021
(THE ACCOUNTANTS AND AUDITORS (REGISTRATION)
(AMENDMENTS), ACT, 2021) – KAMA
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 (*The Accountants and Auditors (Registration) and (Amendments) Act, of 2021*), kwa mujibu ya Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza tarehe 12 Februari, 2021, katika Kikao cha Tisa (9) cha Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Mbili. Kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge uliuleta Muswada huo

kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Kamati iliujadili Muswada huu kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge.

2.0. NAMNA UCHAMBUZI WA MUSWADA ULIVYOFANYIKA

Mheshimiwa Spika, hatua za kuufanyia kazi Muswada huu zilianza kwa maandalizi mbalimbali ya kiutendaji yaliyofanywa na Sekretarieti kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati. Hatua hii ilijenga msingi wa utekelezaji wa kazi za Kamati kuhusiana na Muswada huu ambapo utekelezaji wake ulikuwa kama ifuatavyo:

(a) Maelezo ya uchambuzi wa Muswada uliofanywa na kuwasilishwa kwenye Kamati na Sekretarieti ya Bunge kwa mujibu wa kanuni ya 21(2)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

(b) Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu madhumuni na sababu za Muswada yaliyowasilishwa kwa niaba yake na Mhe. Innocent Bashungwa, Mb ambaye ni Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo;

(c) Kupokea maoni ya wadau kwa mujibu wa kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Wadau waliofika mbele ya Kamati ni hawa wafuatao:

(i) Chama cha Wahasibu Tanzania (*Tanzania Association of Accountants – TAA*);

(ii) Ndugu. Ludovick L. Utouh;

(iii) Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA);

(iv) Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA);

(v) Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA);

(vi) Kampuni ya ushauri na ukaguzi wa hesabu ya Ernest & Young; na

(vii) Kampuni ya ushauri na ukaguzi wa hesabu ya KPMG.

Mheshimiwa Spika, wadau wengine waliwasilisha maoni yao kwa maandishi ambao ni:

(i) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*The University of Dar es Salaam – UDSM*);

(ii) *Institute of Internal Auditors (IIA)*;

(iii) *Delloite*;

(iv) Chuo Kikuu Mzumbe;

(v) Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM);

(vi) Kampuni ya ushauri na ukaguzi wa hesabu ya *Price water House Coopers (PWC)*; na

(vii) Kampuni ya ushauri na ukaguzi wa hesabu ya *Barkettily*.

(a) Uchambuzi wa Kamati wa kila ibara ya Muswada kwa kuzingatia hoja zilizotokana na maelezo, uchambuzi, maoni pamoja na nyaraka mbalimbali kuhusiana na Muswada huu;

(b) Majadiliano kati ya Kamati na Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb kuhusiana na hoja zilizobainika kwa kila ibara ya Muswada na kumshauri Waziri kufanya marekebisho katika ibara zilizoonekana kuhitaji marekebisho kwa mujibu wa kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge; na

(c) Uandaaji wa Taarifa ya Kamati pamoja na kutoa Taarifa kwa Spika kwa mujibu wa kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

3.0. MAONI NA USHAURI MAHSUSI WA KAMATI KUHUSIANA NA MUSWADA HUU

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unalenga kufanya marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi, Sura ya 286. Sheria inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ilitungwa na Bunge kupitia Sheria Namba 33 ya mwaka 1972 ambapo ni takribani miaka 49 iliyopita na imewahi kufanyiwa maboresho mara moja tu kupitia Sheria Namba 2 ya mwaka 1995.

Hivi sasa Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi, Sura ya 286 ina jumla ya vifungu 47 na Jedwali moja. Kupitia Muswada unaopendekezwa, jumla ya vifungu 23 vinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ambavyo ni takribani nusu ya vifungu vyote vya sheria hii na vifungu vipya 8 vinapendekezwa kuongezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa maudhui ya marekebisho hayo kwa kuzingatia changamoto ambazo mtoa hoja aliieleza Kamati ambazo Muswada huu umelenga kuzitatua pamoja na masuala mengine ambayo Kamati iliona yanafaa kuzingatiwa. Changamoto hizo ni pamoja na:

(a) wakaguzi wa hesabu kuandaa seti tofauti za taarifa za hesabu za fedha kwa nia ya kupotosha usahihi wa taarifa hizo;

(b) viwango vidogo vya adhabu vilivyopo kwenye sheria ya sasa ikilinganishwa na uzito wa kosa hali inayochangia ukiukwaji wa miongozo ya uandaaji wa hesabu; na

(c) kutokuwepo kwa masharti kwa wakaguzi wa hesabu kuwasilisha taarifa za ukaguzi Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (*National Board of Accountants and Auditors – NBAA*) na hivyo kusababisha kukosekana kwa kanzi data ya taarifa za hesabu.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati imefanya uchambuzi wa mapendekezo yote ya marekebisho kwa kila ibara ya Muswada kama ifuatavyo:

3.1. Ibara ya 4 inayohusu Marekebisho ya Kifungu cha 4 cha Sheria

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 4 kinachohusu Majukumu ya NBAA. Muswada unapendekeza kuongeza wigo wa majukumu ya Bodi ili iweze kusimamia na kudhibiti mafunzo yanayotolewa kuhusu masuala ya hesabu pamoja na kufanya mapitio ya ubora wa ukaguzi wa hesabu. Majadiliano ya Kamati na Serikali yalifikia mwafaka wa kukubaliana na majukumu yanayopendekezwa.

Aidha, Kamati iliishauri na kukubaliana na Serikali kufanya maboresho zaidi kwa kuongeza jukumu jipya litakayowezesha Bodi kushirikiana na taasisi nyingine zinazojihusisha na masuala ya uhasibu na ukaguzi. Pendekezo hilo ni kama ifuatavyo:

4. Subject to the provisions of this Act and any regulations made the functions of the Board shall be-

...

“(m) to foster collaboration between the Board and other institutions dealing with accountancy.”

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yataiwezesha NBAA kushirikiana na vyama na wadau wengine wanaohusiana na taaluma hii nchini kama vile Vyama vya Wahasibu Tanzania Bara na Zanzibar (TAA na ZAA) pamoja na taasisi nyingine zenye mrengo huo. Hatua hii itaiwezesha NBAA kubadilishana uzoefu na kupata namna bora zaidi ya kusimamia na kuiwezesha taaluma ya uhasibu nchini kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwa maslahi ya taifa.

3.2. Ibara ya 5 inayohusu Marekebisho ya Kifungu cha 6 cha Sheria

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5 inapendekeza kufuta kifungu cha 6 kinachohusu Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji na kukiandika upya kifungu hicho. Sheria ilivyo sasa inaeleza kuwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya uhasibu atamteua Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA ambaye atakuwa

ni mtu aliyejiriwa katika ofisi ya umma ambaye atateuliwa na katika nafasi hiyo kwa mujibu wa wa masharti ya uteuzi. Muswada unapendekeza kufuta masharti hayo na kuweka masharti mapya ambapo sasa inapendekezwa kuwa, mtu atakayeteuliwa na Waziri Mkurugenzi Mtendaji atapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) angalau shahada ya uzamili katika masuala ya uhasibu, fedha, utawala au uchumi;

(b) mwenye taaluma ya uhasibu kutoka katika taasisi inayotambuliwa;

(c) amesajiliwa na NBAA kama mhasibu; na

(d) mwenye angalau uzoefu wa miaka kumi ambapo kati ya miaka hiyo, miaka nane iwe ni ya uzoefu katika nafasi ya usimamizi (*managerial position*).

Kamati inakubaliana na mapendekezo haya kwa kuzingatia lengo lililoelezwa na Serikali la kuwezesha majukumu ya NBAA kusimamiwa na mtu mwenye sifa zinazohitajika kama ilivyo kwa taaluma nyingine hapa nchini.

3.3. Ibara ya 6 inayopendekeza Kuongeza Kifungu Kipya cha 6A

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 6A kinachohusu Utoaji wa Taarifa za NBAA. Ibara ya 6 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 6A mara baada ya kifungu cha 6 cha sheria kinachohusu masharti ya utoaji wa taarifa za Bodi. Kifungu hiki kinamzuia mjumbe au mwajiriwa wa Bodi kutoa taarifa yoyote inayohusiana na Bodi, isipokuwa kwa ruhusa ya maandishi kutoka kwa mtoa taarifa, ama kwa mujibu wa sheria au kwa amri ya Mahakama. Kamati inakubaliana na pendekezo hili kwa kuwa halijazuia kabisa utoaji wa taarifa zinazoihusu Bodi bali imeweka utaratibu bora wa kufuata ili taarifa hizo ziweze kupatikana na iwapo utaratibu huo utakiukwa itakuwa ni kosa la jinai na hivyo kuweka utaratibu wa udhibiti wa taarifa kwa kuwianisha na uwazi wa taarifa.

3.4. Ibara ya 7 inayohusu Marekebisho ya Kifungu cha 7 cha Sheria

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 7 inapendekeza kufuta kifungu cha 7 kinachohusu Usajili wa wanachama wa NBAA na kukiandika upya kifungu hichomojawapo ya marekebisho makubwa katika sheria hii ni haya yanayopendekezwa katika ibara hii kwa kuwa kuweka sifa za mtu kusajiliwa kuwa mhasibu au mkaguzi wa hesabu, kuanishisha aina za wahasibu na wakaguzi wa hesabu, masharti na vigezo vya kusajiliwa kwa kila aina, kuwatambua wahasibu na wakaguzi wa hesabu waliosajiliwa kabla ya mwaka 1972, utoaji wa cheti cha usajili, kuwatambua wanafunzi wanaosoma uhasibu au ukaguzi wa hesabu pamoja na uhifadhi wa rejesta ya wanachama.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo haya kwa kuwa yanawezesha kuhuisha sheria hii kuendana na wakati. Mapendekezo haya pia yanaenda sambamba na mapendekezo katika ibara ya 8 inayopendekezwa kufutwa kwa kifungu cha 10, 11, 12, 13 na 14 vinavyotaja sifa za kila aina za wahasibu na wakaguzi wa hesabu ambazo sasa zitakuwa chini ya kifungu kimoja cha 7. Aidha, marekebisho haya yanawiana na marekebisho ya kifungu cha 26 kupitia ibara ya 13 ambayo yanatambua matumizi ya aina mpya za majina ya wahasibu na wakaguzi wa hesabu yanayopendekezwa katika ibara ya 7 ya muswada.

3.5. Ibara ya 9 inayohusu Marekebisho ya Kifungu cha 18 cha Sheria

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 inayopendekeza marekebisho katika kifungu cha 18 kinachohusu utoaji na taratibu za cheti cha utendaji kazi. Ibara ya 9(b) ya Muswada inapendekeza kifungu kipya cha 18(2) kinachopendekeza muda wa uhuishaji wa leseni kuwa ni kipindi cha miezi 12. Mapendekezo haya yanaenda sambamba na marekebisho ya kifungu cha 21 kupitia ibara ya 10 ili kujumuisha wanachama ambao tayari wamesajiliwa. Kamati imeishauri na kukubaliana na Serikali kuwa muda huo uongezwe ili leseni za utendaji ziwe zinahuishwa kila baada ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yamezingatia kuwa kipindi cha miezi 12 ni kifupi mno na kuhisha leseni kila baada ya muda huo mfupi itakuwa usumbufu kwa wanataaluma na utoaji wa huduma kwa ujumla. Aidha, mapendekezo haya yanaendana na uzoefu unaotumika katika usimamizi wa taaluma nyingine kama vile wahandisi na madaktari.

3.6. Ibara ya 11 inayohusu Marekebisho ya Kifungu cha 24 cha Sheria

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 11 inayopendekeza kufuta kifungu cha 24 kinachohusu uanzishwaji wa Bodi ya Rufaa ya Wahasibu na Wakaguzi na kukiandika upya kifungu hicho. Ibara hii inapendekeza kuboresha muundo wa Bodi ya Rufaa hususan kwa kupendekeza mtu anayeteuliwa na Rais kuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo awe Jaji Mstaafu au mtu mwenye sifa za kuwa Jaji. Kamati inakubaliana na mapendekezo haya lakini imeishauri Serikali kufanya marekebisho yafuatayo:

(a) Kifungu cha 24(1)(b)(iv) kinapendekeza mjumbe wa Bodi ya Rufaa kutoka Mamlaka ya Mapato. Inapendekezwa kuwa, kwa kuwa tayari kuna mjumbe kutoka wizara ya fedha, ni vema badala ya mjumbe kutoka TRA, nafasi hiyo ateuliwe mjumbe kutoka vyuo vya elimu ya juu.

(b) Kifungu cha 24(b)(v) kiboreshwe ili kujumuisha wajumbe wanaoteuliwa kutokana na mapendekezo ya wawakilishi wa vyama vya wahasibu na wakaguzi, wawakilishi kutoka sekta binafsi au asasi za kiraia wenye ujuzi na uzoefu katika masuala ya uhasibu.

3.7. Ibara ya 12 inayohusu Marekebisho ya Kifungu cha 25 cha Sheria

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 12 inayopendekeza marekebisho ya kifungu cha 25 kinachohusu rufaa dhidi ya uamuzi wa NBAA. Maboresho yanapendekezwa katika kifungu hiki ili kuwezesha uamuzi unaotolewa na Bodi ya Rufaa kuweza kufanyiwa marejeo mahakamani. Kamati inakubaliana na mapendekezo kama yalivyo katika Ibara ya 12 ya Muswada.

Hii ni kwa sababu sheria ilivyo sasa inazuia kabisa uamuzi wa Bodi ya Rufaa kufanyiwa marejeo katika mahakama yoyote ambapo ziuo hilo ni kinyume na Ibara ya 107A.-(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 inayoeleza kuwa mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki nchini itakuwa ni Mahakama.

3.8. Ibara ya 14 inayohusu Marekebisho ya Kifungu cha 27 cha Sheria

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14 inapendekeza kufanya maboresho katika kifungu cha 27 kwa kuboresha adhabu kwa watu wanaofanya udanganyifu kana kwamba wao ni wahasibu au wakaguzi waliosajiliwa. Muswada unapendekeza kuongeza adhabu kutoka faini isiyozidi shilingi laki sita au kifungu kisichozidi miaka miwili au zaidi hadi faini isiyozidi shilingi milioni tano na isiyozidi asilimia 10 ya mapato ghafi lakini faini hiyo haipaswi kuzidi shilingi milioni.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya udanganyifu vinafanywa na wahalifu wasiokuwa na sifa katika taaluma husika almaarufu "makanjanja" au "vishoka" ambavyo athari zake kwa taifa na umma ni kubwa. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuongeza adhabu lakini Kamatii inapendekeza adhabu hizo ziboreshwe zaidi kwa kuongeza adhabu ya kutwaa (*forfeiture*) mapato yote yatakayokuwa yamepatikana kutokana na udanganyifu huo.

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili lizingatiwe pia katika ibara ya 16 ya Muswada inayopendekeza marekebisho katika kifungu cha 28 cha sheria kuhusiana na udanganyifu. Aidha, adhabu za faini zinazopendekezwa ziboreshwe ili ziwiane na kiasi cha mapato kitakachokuwa kimepatikana kwa njia ya udanganyifu.

3.9. Ibara ya 15 inapendekeza Kuongeza Kifungu Kipya cha 27A

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 27A kinachoipa NBAA mamlaka ya ukaguzi

wa utendaji kazi wa makampuni ya ukaguzi wa hesabu. Kamati inakubaliana na pendekezo katika ibara hii ambayo inaeleza kuwa, Bodi inaweza kufanya mapitio ya utendaji wa kampuni yoyote ya ukaguzi ili kuboresha kazi za ukaguzi. Katika kutekeleza hilo, Bodi inaweza kukagua nyaraka zozote zinazohusika zilizopo kwenye usimamizi wa kampuni, kutoa nakala au kuchukua sehemu ya nyaraka hizo. Aidha, Bodi inaweza kuomba taarifa zaidi au ufafanuzi wa jambo fulani kutoka kwenye kampuni ya ukaguzi na kampuni husika itawajibika kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo zaidi katika ibara hii yanaipa mamlaka NBAA kuamuru kampuni ya ukaguzi kulipa faini endapo NBAA itajiridhisha kuwa taarifa ya ukaguzi iliyoandaliwa na kampuni hiyo haijafikia viwango vinavyotakiwa. Faini hiyo ni kiasi cha fedha kisichopungua shilingi milioni tano au asilimia 10 ya mapato ghafi ya kampuni.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa adhabu hii ni kubwa mno kwa kuazingatia kuwa inahusiana moja kwa moja na utendaji kazi wa kila siku wa wanataaluma hawa. Hivyo, Kamati ilishauriana na kukubaliana na Serikali kufanya maboresho katika mapendekezo haya ya adhabu kwa kuweka faini isiyozidi asilimia kumi (10%) ya mapato yaliyotokana na kazi iliyobainika kutofikia viwango vya ukaguzi vinavyotakiwa.

3.10. **Ibara ya 17 inayohusu Marekebisho ya kifungu cha 29 cha Sheria**

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 29 (6) kinachozuia mtu yeyote kuajiri mtu ambaye hana sifa za masuala ya uhasibu kwa kukifuta na kukiandika upya kwa lengo la kuongeza faini. Sheria ilivyo hivi sasa inaeleza kuwa mtu yeyote atakayeajiri mtu ambaye hana sifa za masuala ya ukaguzi atakuwa ametenda kosa na endapo atatiwa hatiani atahukumiwa faini isiyozidi shilingi laki saba na elfu hamsini au kifungo kisichozidi miaka mitano au adhabu zote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kurekebisha adhabu hii kwa kuongeza faini kuwa ni kiasi kisichozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa mtu binafsi. Na ikiwa ni kampuni ya ukaguzi, kampuni hiyo itatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichozidi shilingi milioni kumi au asilimia kumi ya mapato ghafi ya kampuni au itakayokuwa kubwa zaidi isipokuwa kiasi hicho hakitazidi shilingi milioni thelathini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo haya lakini ilishauriana na kukubaliana na Serikali kwa kufanya maboresho zaidi katika faini inayoihusu kampuni ili faini hiyo iwe ni asilimia 10 ya ada ghafi ya ukaguzi (*gross audit fee*) badala ya mapato ghafi ya kampuni (*gross revenue*).

3.11. Ibara ya 18 inayohusu Marekebisho ya Kifungu cha 30 cha Sheria

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 30 cha Sheria kinaweka ulazima wa mtu yeyote au kampuni inayofanya biashara au kazi yoyote ya kitaaluma hapa nchini na yenye mali au mapato ghafi yaliyowekwa wa mujibu wa sheria kuajiri mhasibu aliyesajiliwa na Bodi ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa za hesabu. Marekebisho yanayopendekezwa katika kifungu hiki yana lengo la kuongeza kiwango cha mali au mapato ghafi ambacho kinatumika kama kigezo cha kuajiri mhasibu aliyesajiliwa na Bodi.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kubadilisha kiwango hicho kwa kigezo kwamba, mtu yeyote au kampuni inayofanya biashara au kazi yoyote ya kitaaluma italazimika kuajiri mhasibu liyesajiliwa na Bodi pamoja na kuandaa taarifa za hesabu kwa kuzingatia thamani ifuatayo:

(a) kuhusu thamani ya mali itakayozingatiwa, badala ya shilingi 100,000,000/= za sasa, thamani ya mali itakayozingatiwa iwe ni shilingi 300,000,000/=; na

(b) kuhusu mapato ghafi kwa mwaka yatakayozingatiwa, badala ya shilingi 50,000,000/= za sasa, mapato yatakayozingatiwa yawe ni shilingi 150,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikubaliana na pendekezo la Serikali lakini bado ilikuwa na maoni kuwa kiwango kilichoboreshwa ni kidogo mno kwa kuzingatia hali halisi ya biashara na ujasiriamali nchini. Mathalani, wajasiriamali wengi hivi sasa wanafanya shughuli zao katika maeneo ya katikati ya miji au maeneo yenye wakazi wengi ambapo thamani ya mali ni kubwa sana ikilinganishwa na mapato yanayotokana na shughuli zao.

Wengi wa wajasiriamali au wafanyabiashara wanafanya shughuli zao katika majengo yenye thamani kubwa lakini mapato ni madogo kwa kiasi cha kuweza kuajiri watu wengine zaidi ya wale wanaojihusisha moja kwa moja na shughuli za uzalishaji. Hivyo, kuwalazimisha kuajiri mhasibu aliyesajiliwa na Bodi itakuwa mzigo ambao unaweza kusababisha kufungwa kwa biashara hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati ilishauriana na Serikali na kukubaliana kuboresha vigezo hivyo kama ifuatavyo:

(a) kuhusu thamani ya mali itakayozingatiwa, badala ya shilingi 100,000,000/= za sasa, thamani ya mali itakayozingatiwa iwe ni shilingi 700,000,000/=; na

(b) kuhusu mapato ghafi kwa mwaka yatakayozingatiwa, badala ya shilingi 50,000,000/= za sasa, mapato yatakayozingatiwa yawe ni shilingi 500,000,000/=.

3.12. **Ibara ya 19 inapendekeza Kuongeza Vifungu Vipya vya 30A, 30B na 30C**

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19 inapendekeza kuongeza vifungu vipya vya 30A, 30B na ibara ya 30C ambavyo vinahusu uwasilishaji wa taarifa kwa NBAA, mamlaka ya ufuatiliaji wa wanachama wake pamoja na kazi wanazozifanya mtawalia. Kamati inakubaliana na mapendekezo katika kifungu kipya cha 30A ambacho kinataka taarifa zote za hesabu zilizokaguliwa kuthibitishwa na mkaguzi wa hesabu. Mkaguzi

huyo atapaswa kuwasilisha taarifa hizo NBAA ikiwa ni pamoja na taarifa ya mwaka ya mkaguliwa ndani ya siku thelathini tangu taarifa kukamilika. Aidha, NBAA inaweza kufanya marejeo ya taarifa hizo pamoja na kufanya ufuatiliaji wa wanachama wake kwa mujibu wa kifungu cha 30B na 30C mtawalia.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mapendekezo haya ya Serikali kwa kuwa yatawezesha kudhibiti uandaaji wa taarifa zenye upotoshaji zinazolenga kuikoshesha Serikali mapato pamoja na kuanzisha kanzi data ya taarifa za hesabu. Aidha, Kamati ina maoni kuwa, taarifa hizi zinaweza kuwa nyingi ikilinganishwa na uwezo wa rasilimali watu na rasilimali nyingine za kuweza kuzifanyia kazi kwa sasa. Hivyo, ni vema NBAA ikajipanga mapema ili mapendekezo katika ibara hii yaweze kuleta tija mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine katika ibara hizi ni adhabu kwa kutotekeleza mataka ya sheria. Muswada uapendekeza kuwa, endapo mtu au kampuni ya ukaguzi itakiuka vifungu hivi itakuwa imetenda kosa na iwapo itatiwa hatiani hukumu itakuwa ni faini ya kati ya shilingi milioni tano hadi shilingi milioni thelathini au kifungu kisichozidi miaka miwili au adhabu zote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano, Kamati ilikubaliana na Serikali kuhusu adhabu hizi kwa kuwa zinatarajiwa kuwezesha kudhibiti udanganyifu na kuhakikisha kuwa viwango vya uandaaji hesabu vya kitaifa na kimataifa vinazingatiwa. Aidha, viwango vya adhabu vinavyopendekezwa kwenye Muswada vinampa mtoa maamuzi nafasi ya kupima ukubwa wa kosa na kuona ni kiasi gani mkosaji anastahili kulipa.

3.13. Ibara ya 21, 22, 23, 24 na ibara ya 26 zinahusu maboresho ya jumla ya utendaji wa NBAA pamoja na masuala ya ukaguzi wa hesabu

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo haya kwa kuwa yanalenga kuimarisha misingi ya uwazi na

uwajibikaji katika mapato na matumizi ya fedha za NBAA. Aidha, kupitia mapendekezo ya ibara ya 26, Mkurugenzi Mtendaji anapewa mamlaka ya kuffilisha makosa ya jinai kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa ikiwemo kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini hali inayoweza kupunguza mzigo wa kesi mahakamani na kutoa fursa kwa wahasibu na wakaguzi wa hesabu kuendelea na majukumu yao, pale wanapokubaliana na ufiiflishaji huo, badala ya kupoteza muda mwingi mahakamani.

3.14. Maboresho mengine katika Muswada

Mheshimiwa Spika, Kamati imeshauriana na Serikali na kukubaliana maboresho katika maneno mengine ya Muswada kama ifuatavyo:

(a) Ibara ya 3 kwa: -

(i) kuboresha tafsiri ya maneno "***a certified public accountant in training***" kwa kuwa tafsiri hiyo inaweza kuwa na tata kwa kutokueleweka kama inamhusu mhasibu mwanafunzi au mhasibu aliyepo kwenye taasisi inayotoa mafunzo. Maboresho haya pia yazingatiwe katika kifungu cha 7(1)(iv);

(ii) katika tafsiri ya neno "***standards***" kwa kufuta maneno "***accounting standards***" kwa kuwa maneno "***financial reporting standards***" yanajumuisha maneno hayo.

(b) Ibara ya 4 inapendekeza kuongeza majukumu mapya ya NBAA. Kamati inapendekeza kufuta maneno "***and audit services***" yaliyopo katika aya (I) inayopendekezwa katika ibara ya 4(a) kwa kuwa maneneo hayo yapo ndani ya tafsiri ya neno "***accountancy***" iliyopo katika ibara ya 3(a) ambalo tayari limetumika katika aya hiyo.

(c) Kufuta neno "***certified***" lililopo katika mstari wa pili wa kifungu cha 30A(1) na ibara ya 20(a), (b)(4) na sehemu nyingine yoyote linapojitokeza katika Muswada na badala yake kuweka neno "***audited***" kwa kuwa wakaguzi hawathibitishi hesabu bali wanazikagua ambapo taarifa za ukaguzi huo inaweza kujitokeza zisiwe sahihi kwa asilimia 100.

(d) Katika ibara ya 23, kifungu kipyua cha 40(1) kinapendekeza NBAA kuwasilisha taarifa za mwaka kwa Waziri lakini matumizi ya maneno **“during that”** hayaakisi uhalisia wa uwasilishwaji wa taarifa hizo kwa mwaka wa fedha uliomalizika. Hivyo, ni vema maneno hayo yakafutwa na badala yake yatumike maneno **“for the previous”**.

(e) Katika ibara ya 26, kifungu cha 42A(1) kinapendekeza mamlaka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA kufifilisha adhabu za makosa chini ya sheria hii pamoja na sheria nyingine za kissekta. Hatua hii inaweza kusababisha mgongano wa kisheria kwa kuwa sheria nyingine za kissekta zinaweza kuwa na mamlaka na utaratibu mwingine wa kufifilisha makosa. Hivyo, ni vema maneno **“or any other sector legislation”** yakafutwa.

(f) Maboresho ya kiuandishi kama ifuatavyo:

(i) Ibara ya 2(b) yatumike maneno **“practising firm”** badala ya **“practicing firm”**;

(ii) Tafsiri ya neno **“accountancy”** ihamishwe kutoka ibara ya 3(a) kwenda ibara ya 3(b) kwa kuwa ni tafsiri mpya ambayo haikuwepo kwenye sheria;

(iii) Ibara ya 30B (3) isomeke **“A person who refuses to.....”** badala ya **“refused”**; na

(iv) Ibara ya 30C (3) isomeke **“A person who refuses to.....”** badala ya **“refused”**.

4.0. MAONI NA USHAURI WA JUMLA WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa katika kila ibara ya Muswada, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla ambao ni vema Serikali ikauzingatia na kuufanyia kazi kwa kuwa ni masuala yanayohusiana na utungaji wa sheria na taaluma ya uhasibu nchini kama ifuatavyo: -

4.1. Inapotokea Serikali inakusudia kuwasilisha Muswada Bungeni, endapo sheria ina vifungu vingi ambavyo vinakusudiwa kufanyiwa marekebisho kwa wakati mmoja, ni vema Serikali ikatumia utaratibu wa kuifuta na kuiandika upya sheria hiyo. Utaratibu huu utaliwezesha Bunge kuifanyia kazi sheria hiyo kwa ufanisi zaidi ikilinganishwa na inapowasilishwa kwa utaratibu wa marekebisho.

4.2. Kuna umuhimu wa kutenganisha majukumu ya taasisi inayohusika na udhibiti wa sekta/taaluma na ile inayohusika na wanachama kwa kuunda chombo cha usimamizi (*Public Oversight Body*).

4.3. Muswada haujaweka masharti kuhusu usimamizi wa wakaguzi wanaofanya kazi chini ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Suala hili liangaliwe kwa kina.

4.4. Ni vema Bodi zote za Wakurugenzi za mashirika yote ya umma kuwa na angalau mhasibu mmoja ambaye atasaidia kutoa ushauri kuhusiana na masuala ya usimamizi wa fedha.

4.5. Uanzishwe mkakati mahsusi wa kupitia sheria zote zinazohusiana na taaluma mbalimbali nchini ili kujiridhisha kama maslahi ya umma yamezingatiwa ipasavyo katika sheria hizo.

4.6. Serikali iweke utaratibu wa wanachama wa Chama cha Wahasibu Tanzania Bara (*Tanzania Accountants Association - TAA*) na Chama cha Wahasibu Zanzibar (*Zanzibar Accountants Association - ZAA*) wa kuweza kufanya kazi kwa pamoja.

5.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kukushukuru kwa namna ya kipekee kabisa kwa kuuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Kusema kweli, kwa mara ya

kwanza, mimi na Kamati yetu tumepata uzoefu mpya katika kazi ya kulisaidia Bunge lako Tukufu kutekeleza mojawapo ya majukumu ya msingi ya Bunge ya utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:

- 1) Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb – Mwenyekiti
- 2) Mhe. Japheti Ngailonga Hasunga, Mb – M/ Mwenyekiti
- 3) Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mb
- 4) Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwele, Mb
- 5) Mhe. Simon Songe Lusengekile, Mb
- 6) Mhe. Anton Albert Mwantona, Mb
- 7) Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
- 8) Mhe. Juma Othman Hija, Mb
- 9) Mhe. Idarus Faina Ravia, Mb
- 10) Mhe. Deus Clement Sangu, Mb
- 11) Mhe. Francis Kumba Ndulane, Mb
- 12) Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb
- 13) Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb
- 14) Mhe. Aysharose Ndogoli Matembe, Mb
- 15) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb
- 16) Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb
- 17) Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb
- 18) Mhe. Jackline Kainja Andrea, Mb
- 19) Mhe. Daudi Protas Venant, Mb
- 20) Mhe. Zubeida Khamis Shaibu, Mb
- 21) Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb
- 22) Mhe. Bakar Hamad Bakar, Mb

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nanelwa Mwiambi kwa ushauri wake kwa Kamati pale alipotakiwa kufanya hivyo. Natoa shukrani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati, kupitia kwa Mkurugenzi Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndugu Erick

Maseke na Ndugu Wilfred Magova pamoja na Maafisa Sheria walioishauri Kamati Ndugu Stephano Seba Mbutu na Ndugu Rehema Lazarus Kipera.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo za kipekee, naomba sasa nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb

**MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
HESABU ZA SERIKALI (PAC)**

03 Septemba, 2021

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Mmefanya kazi nzuri kwa niaba ya sisi Wabunge wote.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa utaratibu wetu ninayo majina hapa ya Wabunge mbalimbali wanaotaka kuchangia hoja hii, tutaanza na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla na Mheshimiwa Salome Makamba ajiandae.

MHE. BAKAR HAMAD BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu kuweza kuchangia muswada huu wa sheria ambao tunaenda kuujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa

Mwigulu Nchemba kwa uwasilishaji wake mzuri wa mapendekezo haya ya muswada huu wa sheria, lakini kipekee sana naomba nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati ya PAC, Mama Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, kwa uwasilishaji mzuri na wa fasaha sana kwenye hotuba yake ambayo ametoka kuiwasilisha. Mchango wangu mimi utakwenda kwenye maoni haya ya jumla ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia kwenye muswada huu wa sheria, Ibara ya 18 ambayo imefanyia marekebisho kwenye kifungu cha 30, inakwenda kuzifanya au kuzitaka biashara zote ambazo mitaji yake ni kuanzia milioni 700 ama *turn over* ya milioni 500 kwenda kuwasajili ama kuwaajiri wahasibu ambao wamesajiliwa wenye CPA, lakini tunazo taasisi ama mashirika ya umma makubwa yenye mitaji zaidi ya hizo milioni 700 na zaidi ya hizo milioni 500 ambazo zimetajwa ndani ya sheria hii ambazo zimefanya taasisi zisizokuwa za Serikali ziajiri wahasibu, lakini mashirika haya kwenye kurugenzi zao hayana wahasibu wenye CPA.

Kwa hiyo, tumependekeza kwenye Bodi za Wakurugenzi kwenye mashirika haya ya umma angalao na wao wawe na mhasibu japo mmoja kwenye bodi zile ambaye atakwenda kusaidia kwenye masuala haya ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bodi nyingi za wakurugenzi kwenye mashirika na mashirika yetu haya ndio ambayo yanakwenda kuzalisha na ndio ambayo yanakwenda kuongeza mapato makubwa kwenye nchi yetu. Sasa kuziacha tu bodi hizi bila ya wenye taaluma hii na jambo hili kuwekwa kwenye sheria kwa kweli ni kuzipa mianya bodi hizi kukwepa wana-taaluma hii wenye CPA. Kwa hiyo, tunapendekeza sana kwamba jambo hili lina uzito mkubwa na liweze kuchukuliwa kuingizwa kwa wahasibu wenye taaluma ya uhasibu wenye CPA kwenye Bodi za Wakurugenzi kwenye mashirika mbalimbali ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, NBAA ni taasisi ya kitaifa, lakini sheria hii ambayo tunaenda kuipitisha/kuitunga leo, ni

sheria ambayo inahusu Tanzania Bara peke yake. Tunatambua kwamba Zanzibar sasa hivi wapo kwenye mchakato wa kuanzisha bodi kama hii ambayo itahusiana na usajili wa wahasibu na wakaguzi kwa kule Zanzibar, lakini bado kuna ukakasi kwamba, kwa sababu hii ya *NBAA* ni Bodi ya Taifa, je, *recognition* ya wana-taaluma hawa itakuwaje? Wale ambao watasajiliwa na Bodi ya Zanzibar watakapokuja huku Bara watatambulikaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii bado ipo kimya sana, haijaleza kwamba, tutawatambua je wana-taaluma hii watakaotoka upande mmoja wa muungano kwenye sehemu nyingine, wale watakaotoka Tanzania Bara kwenda kufanya kazi Zanzibar Bodi ya Zanzibar itakuwaje, lakini wale ambao watasajiliwa na Bodi ya Zanzibar watakaokuja kufanya kazi huku Bara watatambulikaje na sheria hii? Kwa hiyo, tunaomba pia Mheshimiwa Waziri aje atueleze jambo hili kwenye sheria hii litakaaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa sababu, taasisi hii ni ya kitaifa, tayari ime-*comply* na imejiunga na taasisi mbalimbali za kimataifa, sasa siamini kwamba taasisi kama hii ambayo itaundwa kule Zanzibar itapata ruhusa wapi ya kuweza kujisajili na taasisi za kimataifa? Ziko taasisi mbalimbali kama *IVAC*, lakini iko *PAFA*, kuna *INTROSAI* na *AFROSAI*; taasisi zote hizi *NBAA* ni mwanachama kule, lakini je, Bodi ya Zanzibar ambayo itaenda kuundwa sasa hivi itakuwa mwanachama kule? Itaruhusiwa kuundwa kule?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, tunaona kwamba, kwa *experience* tunazo bodi au tunazo taasisi ambazo Zanzibar na Tanzania Bara zinakanganyana kwenye kujiunga ama kupata ushirikiano kwenye mashirika ya kimataifa, nikitoa mfano, tunayo *TFF* na *ZFF* kule mpaka leo Zanzibar si mwanachama wa mashirika yale au taasisi zile za kitaifa zinazohusiana na jambo hili. Kwa hiyo, na jambo hili tunaliona kwamba, huko mbele huenda, kuna wasiwasi, ikaja ikatokezea mkanganyiko kama huu na ikatokezea mtafaruku kwenye mambo yetu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 4 kwenye muswada huu imetaja majukumu ya Bodi hii ya *NBAA*, lakini majukumu haya tunaona kwamba yamechukuliwa/ yamechanganywa majukumu ya udhibiti na usimamizi. Tumependekeza kwamba tuanzishe *public oversight body* ambayo itaenda kushughulikia baadhi ya majukumu kwamba, tusiipe mzigo mkubwa taasisi hii ya *NBAA* kufanya mambo yote ya udhibiti pamoja na usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii asilimia 100. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wyclif Makamba. Mheshimiwa Radhia Idarus Faina ajiandae.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na awali ya yote nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujalia uhai, lakini pia kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo tukiwa wazima, bukheri wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachangia kwenye maeneo mawili tu, vifungu viwili; kifungu pendekezwa cha 18 kwenye muswada na kifungu cha 19 kwenye muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 18 kinaenda kubadilisha kifungu cha 30 kilichokuwepo kwenye sheria ya awali, ile sheria ya mwaka 1973 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2002 ambapo mapendekezo ya marekebisho yaliyopo kwenye muswada, kama yalivyowasilishwa na Serikali, yanaenda kupandisha viwango vya mali kutoka *assets* za shilingi milioni 100 ama zaidi kwenda kwenye shilingi milioni 300 au zaidi, lakini pia *gross turnover* ya shilingi milioni 50 hadi shilingi milioni 150; kwamba wafanyabiashara wote ambao watakuwa wana-*assets* za zaidi ya shilingi milioni 300 ama *gross turnover* ya zaidi ya shilingi milioni 150 watawajibika kwa mujibu wa sheria kuajiri wahasibu ambao wana *CPA* ama wahasibu wale wakaguzi

wa hesabu ambao wamesajiliwa kama *CPA PP (Certified Public Accountant in Public Practice)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ninadhani pamoja na Serikali kuleta mapendekezo ya marekebisho ambayo yanaongeza viwango kutoka milioni 100 mpaka 300, kutoka milioni 50 mpaka milioni 150 bado viwango hivi ni vidogo sana na ningependelea Serikali watazame jambo hili katika muktadha tofauti kidogo. Kwamba, bado milioni 300 ni ndogo sana kuwa ni mali za mfanyabiashara, kuna wafanyabiashara kwa mfano kwenye *nature* ya biashara kama ya dawa (*pharmacy*); kama kibanda kile ni mali yake na ana *warehouse* hizo *assets* tu peke yake zinaweza zikafika hata milioni 200, lakini pia dawa, ule mzigo alioweka mle ndani, unaweza ukazidi milioni 200 hata milioni 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukichanganya vyote hivi vitazidi milioni 500, milioni 600 kama mtaji na hivyo, kumtaka lazima awe na mhasibu nadhani ni kumuongezea *cost* za uendeshaji. Ni kumuongezea gharama za uendeshaji na usimamizi wa biashara yake ambazo pengine hazihitaji kwa sababu kuna uwezekano mkubwa, mfano mimi binafsi ni Daktari wa Tiba, mke wangu ni Mfamasia ama ni daktari kama ilivyo sasa, mtoto wetu akawa mfamasia, tukaamua kufungua biashara ya *pharmacy* na tukakaa sisi wenyewe kama familia pale, hatuhitaji mhasibu. Na sisi wala hatuhitaji mifumo *complicated*, tunahitaji mfumo rahisi wa *computer* ambapo tunaweka *data* za mauzo, *data* za *stock* na tukitoka jioni tunafunga ofisi yetu tunarudi nyumbani, mhasibu wa nini hapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kutikana na *nature* ya biashara yetu, kutokana na mtaji, kutokana na *gross turnover* ambayo tunapata tutalazimika kuweka mhasibu wakati sisi hatuhitaji mhasibu.

Kwa hiyo, mapendekezo yangu ni kwamba, hata hivi viwango vinavyopendekezwa vya *assets* za thamani ya milioni 300 ama *gross turnover* kwa mwaka ya shilingi milioni 150 yarekebishwe na viwango hivi viongezwe pengine kutoka

milioni hiyo 300 inayopendekezwa kwenda mpaka kati ya bilioni moja na nusu hadi bilioni mbili na kutoka milioni 150 mpaka bilioni moja kwa kiwango cha chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itafanya *requirement*, uhitaji wa kuwa na mhasibu kwenye *organization* kuwa wa maana zaidi kwa sababu, hii ni biashara kubwa. Na pengine bilioni moja ni mtaji mkubwa na hivyo, mtu anayeendesha biashara ya kuzungusha bilioni moja kiukweli anahitaji mhasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mfano mkulima ana shamba ekari 500 ama ekari 1,000 ana matrekta mawili, ana *power tillers*, ana ma-*godown* hapo *site* yake, ana mashine ana *harrow*, ana *planters* kwa ajili ya kupandia, ana mashine ya kupulizia dawa, ukiangalia *assets base* ya huyu mfanyabisahara ambaye ni mkulima kimsingi na Wabunge wengi nafahamu hapa ni wakulima, utakuta uwekezaji kwa maana ya lile shamba, ma-*godown*, pamoja na hizo *farm implements* ambazo anatomia kufanya shughuli ya kilimo inazidi bilioni moja.

Sasa *turnover* anaweza akalima ekari 100 ama akalima ekari 200 na mwisho wa siku pengine bei zimeanguka kama zilivyoanguka mwaka huu bei za baadhi ya nafaka hapa nchini, mauzo yake yakawa chini ya shilingi milioni 200/300. Ukimtaka huyu mtu lazima awe na mhasibu ni kumuwekea masharti ambayo yanamuongezea gharama za uendeshaji ambazo pengine hazihitaji sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, tunapotunga sheria ni lazima tuwe makini sana kwa sababu kuja kurekebisha ni kazi na sidhani kama Ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu atakapoanza kusimamia utekelezaji wa sheria hii hatopata kelele endapo viwango vitakuwa chini. Maana yake wanaofanya biashara ya mabeli ya mtumba wana zaidi ya milioni 300 wanayozungusha wote watatakiwa wawe na wahasibu, wanaofanya biashara ya maduka ya jumla wote watatakiwa kuwa na wahasibu na sidhani kama kwa sasa tunahitaji kelele hiyo katika siasa za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nililopenda kuzungumzia ni kifungu cha 19 cha muswada ambacho kinaenda kubadilisha sheria hii iliyopo sasa kwa kuongeza kifungu cha 30A, 30B na 30C, ambayo hii inahitaji kuwe na mawasilisho ya *audited financial statement* kwenda NBAA kwa ajili ya *record*. Kwamba, kila mhasibu anayekagua hesabu za taasisi ama za mfanyabiashara mmoja lazima azichukue zile hesabu na awajibike kuziwasilisha NBAA kila mwaka kadiri anavyofanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutaka uwajibikaji, pamoja na kutaka ku-*enhance transparency*, kuweka uwazi zaidi kwenye biashara, hiki ni kifungu hatarishi sana kwa ustawi wa biashara hapa nchini na kwa nini nasema ni hatarishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kifungu ambacho kitaenda kufanya biashara nyingi sana zikwame kupata mikopo kwenye *bank* zetu. Sitaki kuongea sana mambo ambayo yako *unethical*, lakini nadhani hata kukiweka hiki kifungu chenyewe ni *completely unethical*, ni kinyume kabisa na maadili ya *confidentiality* kwa maana ya siri kati ya mhasibu na *directors* wa kampuni ambayo ameenda kuikagua, kwamba mhasibu anawekewa kifungu hapa ambacho kinamtaka alazimike kupeleka hesabu za mteja wake NBAA wakati yeye ana-*non disclosure agreement* na mteja wake kwamba, asitoe siri ya zile hesabu ambazo anaenda kumkagua huyu mhasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki kinaleta hatari gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Malizia Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, eeh, muda umeisha? Ahsante naomba nimalizie tu hapa dakika moja tafadhali

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu Serikali wanapo-*introduce* kifungu hiki lengo lao ni kutaka kuweka uwazi zaidi, lakini pia lengo lao ni kutaka kuwadhibiti wale wahasibu ambao wanatengeneza hesabu mbili-mbili kwenye kampuni moja. kwamba, kuna hesabu zinazoenda benki, lakini pia kuna hesabu zinazoenda *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hakuna asiyejua kwamba kumekuwepo na hii *practice* toka kabla ya uhuru na itaendelea kuwepo kwa sababu hii ni *practice* ambayo inawafanya wafanyabiashara warekebishe hizo hesabu kwa kuzi-*doctor in some way* ili waweze kukopesheka. Hii ni siri ambayo ipo na tunaifahamu na sidhani kama wazee wetu mwaka 1973 walipokuwa wanaenda kukitunga hiki kifungu hawakuwa wanajua hii *practice* ipo; walijua, lakini waliamua kunyamaza wakaacha hiyo *environment* ya biashara ifanye kazi kama inavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wazee wetu walijua kwamba, saa nyingine ukikuta jinni limefunikwa kwenye chupa, basi usilifungulie. Hujui wazee waliolifungia humo ndani walikuwa na nia gani.

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante sana Mheshimiwa. Hoja yako imeeleweka, ahsante sana.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba atafuatiwa na Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi leo nichangie kuhusiana na sheria hii ya wahasibu na wakaguzi.

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo, katika sheria hii nitarejea marekebisho ya kifungu cha 11 au ibara ya 11 ya muswada ambayo inahusiana na *establishment of Accountants and Auditors Appeal Board*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Bodi hii ya Wahasibu na *Auditors* wametaja watu ambao wataingia kwenye Bodi na katika orodha hiyo wameweka watu katika mafungu matano; nikienda (a) wanasema; *a chairman who shall be appointed by the President from among retired Judges or any person with qualification which may warrant such a person to be appointed as a Judge*.

(b) Wakasema wataweka *five members* ambapo *member* wa kwanza atakuwa ni *law officer* ambaye ana *represent* Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; *member* wa pili ni *one senior member from the Ministry responsible for Finance*; na *member* wa tatu ni *one senior member from the Bank of Tanzania*; wa nne ni *senior member from Tanzania Revenue Authority*; na wa tano hapa ndiyo kwenye ukakasi ni *two members with knowledge and practical experience in accountant professional*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye kifungu hiki wameweka uwanja mkubwa sana wa Waziri kuchagua mtu yeyote ambaye ana elimu ya uhasibu anaweza kuingia kama *member* wa bodi, watu wawili hii ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu nataka nishauri hapa, tunazo taasisi au vyama vya kitaifa vya wahasibu au watu wenye taaluma inayofanana na uhasibu ambao Waziri anaweza kwenda kuchagua *members* kutoka kwenye vyama hivyo, badala ya kupewa uhuru wa kuchagua mtu yeyote kwa sababu anaweza akaweka mtu yoyote hata rafiki yake, hata ndugu yake kwa sababu amepewa nafasi hiyo kwa mujibu wa sheria. (Makofi)

Kwa hiyo, ukisoma kwenye hotuba ya Kamati ukurasa wa pili viko vyama hapa ambavyo vimetusaidia kutuletea

mapendekezo ya Kamati, kuna Chama cha Wahasibu Tanzania (*The Tanzania Association of Accountants*) au kuna Taasisi ya Uhasibu Tanzania (*TIA*) na vyama vingine vinavyofanana na hivi. Waziri apewe *mandate* kwenye sheria hii kwamba hao watu wawili atakaowachagua basi awatoe kwenye vyama vya kitaaluma vinavyofahamika kitaifa ili waweze kuingia kama *members* wa bodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukiacha tu hivyo faida ya kuwachagua watu hawa wanapata uwakilishi, lakini wataweza kuwakilisha makundi makubwa ambayo yako nyuma yao, ni muhimu sana sheria hii ikazingatia jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Ibara ya 12 ya muswada; Ibara hii ya 12 ya muswada imeleta mabadiliko kwa kufuta maneno yaliyokuwepo kwenye kifungu cha 25(1) cha sheria mama. Maneno yale yanasomeka ifuatavyo; wanasema, "*The principal Act is amended in section 25(1) by deleting the words "and every order of the Appeals Board under this section shall be final, conclusive and binding upon all parties concerned, and shall not be subject to a review by any court."*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kifungu kama ziko sheria zingine zilizo na kifungu hiki zinachozuia kwamba maamuzi ya Bodi ya Rufaa yatakuwa ndiyo maamuzi ya mwisho na hakuna chombo kingine chochote kitakachoruhusiwa kupitia maamuzi hayo. Hiki kifungu kinakinzana na Katiba, ukisoma Ibara ya 107(a) ya Katiba inasema; mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumeleta mabadiliko ya muswada huu na ukiangalia kwenye mabadiliko ya muswada huu vifungu vinavyofanyiwa mabadiliko na kufutwa ni vingi mno, kwa maana hiyo kuna uwezekano kwamba ziko sheria nyingi kwa sababu hizi sheria imezeeka, ni ya mwaka 1972.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba kwa sababu tuko kwenye zoezi letu la uchangiaji ili tuweze kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima na kutunga sasa sheria. Hiki kifungu unachokisema hapa umeshakisoma kinasema mabadiliko kinayofanya kinataka haya yafutwe yasiwepo, maana yake hizi changamoto unazosisema zilikuwepo wakati yapo, sasa yanafutwa sasa hoja yako ni nini kwenye kufutwa haya maneno unataka yawepo au yaendelee kutokuwepo?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu kwa vile naongea Kiswahili cha Kisukuma, unajua tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu hapa ni kwamba hii sheria ni ya mwaka 1972, ina miaka karibu 49 na ilikuwa na hiki kifungu humu ndani kinaishi. Hoja yangu kama sheria zipo nyingi za namna hii zenye kifungu cha namna hii, ipo haja ya Tume ya Mabadiliko ya Sheria kufanyia *review* ya sheria zote ili kuweza kuondoa vifungu ambavyo vinakinzana na katiba kama hiki ambacho kimeonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naunga mkono kukifuta hiki kifungu kitu ambacho kinanipa wasiwasi ni kwamba sheria hii inanipa ukakasi mkubwa, sheria hii imeishi miaka 49 ikiwa na kifungu kinachosema Bodi ndiyo itakuwa ina maamuzi ya mwisho, hivi fikiria sheria ngapi ambazo hazijafanyiwa *review* zina matatizo kama haya. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome nakubaliana na wewe kwa asilimia 100, lakini sasa kwa sababu tuko katika hatua ya kutunga sheria na sasa Serikali imeleta kifungu hiki wewe unaeleza kana kwamba viko mahali pengine ambayo ndiyo kazi yetu sisi kama Bunge ni kazi yetu wewe kama hapo unayo orodha ya hivyo vifungu wewe vitaje kwa sababu ukieleza kwa namna unavyoeleza sasa mimi nataka nikuongoze vizuri.

Muda adhimu wa Bunge unakuwa sasa huutumii vizuri, kwa sababu kifungu hiki ilicholeta marekebisho ni Serikali sasa

ukianza kufikiri kwamba viko na vingine basi uvilete maana sasa hivi tunayotunga sheria ndiyo hii hapa, hata kama ina miaka 60, 40 lakini tunayotunga ni hii hapa na kifungu tayari kimeshafutwa.

Sasa hapo tunalalamika au tunataka kifutwe yaani kiondoke kwa sababu ukizitungumzia sheria nyingine siyo tunazozitungumzia sasa hapa, tunazungumzia sheria hii, wewe kifungu hiki unatakaje? Ndiyo hoja.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendeleo, katika sheria hiyo hiyo ya mabadiliko ya sheria hii hii kifungu cha 14 cha muswada kinafanya marekebisho ya kifungu cha 27 cha sheria mama ukienda pale (b) kwa hiyo inakuwa ni 14(b) kinasema; *“deleting the closing phrase and substituting for it the following; (b) in the case of practicing firm, to a fine of not less than five million shilling or ten percent of the firm’s gross revenue, whichever is greater, provided that the amount charge shall not exceed thirty million shillings.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nishauri hapa kwenye kifungu hiki kama wana *charge* kiwango cha chini ni milioni tano, halafu wanasema au watampiga faini yule mwenye kosa watampiga faini asilimia 10 ya mapato ghafi, halafu wanasema asilimia 10 hiyo isizidi milioni 30; *the shortcut* is wangeandika tu kiwango kisichopungua *five million* na kisichoziidi *30 million shillings*, kwa sababu ukisema *the greater value* yaani *it is over wording* kwenye *legal drafting* unakuwa umeandika maneno mengi ambayo kimsingi ungeweza tu kuya-cover kwa kuweka tu ile *30 million* na *five million* isipungue. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiachana na kifungu hicho ningependa pia kushauri katika muswada huu na mimi nakubaliana na mapendekezo ya Kamati cha kwanza nakubaliana na mapendekezo ya Kamati ambayo wameyatoa katika ukurasa wa 18 kuhusiana na kutenganisha majukumu ya *NBAA* yale majukumu ya *regulation* na majukumu ya kuwasajili hawa wahasibu na hii ndiyo *practice*,

sasa hivi ilivyo kwa mujibu wa sheria na muswada huu mpya *NBAA* inawasajili wahasibu kwa maana ya kuwapa zile *certificates*, wakati huo huo inawasimamia wakikosea ina bodi ya kuwasimamia na mambo kama hayo. Sasa ni majukumu mengi ahalfu wakati huo huo yeye ndiyo anakuwa ndiyo *referee* na wakati huo huo ndiyo mchezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni nini kwenye hili; mimi nashauri *NBAA* kama ilivyo kwa upande wa taaluma ya sheria *Law School* ndiyo inayowa-*train* wanasheria na wanapata *certificate* ya *practice* wakitaka kuwa mawakili, lakini kwa upande mwingine *TLs* ndiyo ambayo inahusika ndiyo Chama cha Wanasheria; kusajili na kuwasimamia wanachama wao na mambo ya kinidhamu.

Kwa hiyo, ningeshauri hapa tutenganishe hizi *function* mbili ya *regulation* na *registration* kutoka *NBAA* wazitenganishe ili kupunguzia majukumu, lakini pia kuongeza ufanisi katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hayo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Salome Makamba, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Ravia Idarus Faina atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana ajiandae.

MHE. RAVIA IDARUS FAINA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama hapa, vilevile nikushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe ushauri kwa mambo kama mawili, kwa vile Zanzibar hakuna Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi na walio wengi wahasibu wa Zanzibar ni wanachama wa *NBAA*, kwa hiyo ningeshauri Serikali mbili zikakaa; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweka *harmonize* ya Muungano hii sheria ikatumika kwa Tanzania nzima ili wahasibu wapate kufanya kazi zao kwa ufanisi mzuri, lakini

pili kuna wahasibu ambao wana CPA na wao waweze kufanya kazi zao kwa muongozo uliokuwa sahihi.

Kwa mfano unapofungua kampuni ya ukaguzi wa mahesabu Zanzibar iweze kufanya ukaguzi Tanzania Bara na vilevile utapofungua kampuni ya ukaguzi Tanzania Bara ifanye kazi Zanzibar. Vilevile nipende kutoa ushauri kwamba nziombe tena Serikali mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakae na wazipitie Sheria za Fedha ambazo zinaathiri taaluma ya uhasibu ziwekwe sawa kwa maslahi ya pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kinachonishawishi kuunga mkono hoja ni kwa sababu tu itafungua maslahi makubwa kwa kada hii ya wahasibu na niwaombe Wabunge wenzangu tuupitishie muswada huu wa sheria ili ulete maslahi makubwa kwa wahasibu. Ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa mtoa hoja ajiandae.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia katika muswada huu, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta muswada huu muhimu hapa Bungeni, ambao una maslahi mapana ya nchi yetu kwa kweli nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuuchambua muswada huu na kuandika ripoti nzuri sana ambayo imewasilishwa leo Bungeni, kwa kweli tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nitumie nafasi hii kuwapongeza wadau mbalimbali ambao wametoa maoni

mbalimbali ya namna ya kuboresha muswada huu. Ni kweli kabisa *NBAA* inafanyakazi kubwa mbili; kazi ya kwanza ni ya udhibiti (*regulator*) lakini kazi ya pili ni ya kusimamia uendeshaji. Sasa hizi kazi katika maeneo mengi zimetenganishwa na sisi kama Kamati tuliliangalia sana katika suala hili kwamba namna tunavyoweza kutenganisha, lakini kutokana na hali tuliyoiona tukasema sasa hivi hatuwezi kutenganisha, tutaacha kwanza ziendele kufanyakazi hiyo ifanywe na *NBAA* lakini baadae vyama vya kitaaluma vijiiimarisha ili kusudi viweze kuchukua jukumu lile la usimamizi wa uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilifikiri ni muhimu ni masuala mahususi kama mawili au matatu ambayo nataka kuchangia; la kwanza ni hili muswada huu ni wa Tanzania Bara, lakini muswada huu kitendo cha kuwa ni wa Tanzania Bara kunaleta *complication*, kunafanya kwamba wahasibu walioko Zanzibar na wakaguzi wa mahesabu wa Zanzibar wasiweze kutambuliwa na kusajiliwa na *NBAA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tulipoliangalia kwa undani na baada ya kushauriana na Serikali, tumeona hii ni changamoto, lakini tukasema kwasababu masuala ya fedha ni ya Muungano basi Serikali ije iangalie huko mbele, waje wafanye marekebisho kupitia marekebisho ya sheria mbalimbali ili huu Muswada uweze pia ku-*apply* Zanzibar kama wataona inafaa, lakini baada ya *consultation* na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa hiyo, sisi tukasema kwa sababu sasa hivi kwa hali ilivyo kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijahusishwa, tukiamua kwamba tuingize iwe ya Muungano tutakuwa tumekiuka taratibu, kwa hiyo tukaona kwamba tutairudisha nyuma. Kwa hiyo tukasema tuende na Muswada kama ulivyo lakini baadae Serikali ione haja ya kwenda kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar waje na marekebisho baada ya mashauriano kusudi sasa wale wenzetu wahasibu walioko Zanzibar, wakaguzi wa mahesabu waliopo Zanzibar waweze sasa kutambuliwa na kusimamiwa.

Kwa sasa hivi ilivyo *NBAA* wanasimamia wahasibu kutoka Zanzibar kwa makubaliano yaliyoandikwa kwa *memorandum*. Kwa hiyo, wahasibu kutoka Zanzibar wanasajiliwa na *NBAA*, wakaguzi wanasajiliwa na wanafanyakazi Tanzania Bara na wanafanya Zanzibar, lakini kwa makubaliano siyo kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, tunafikiri sasa imefika wakati sheria lazima itamke vizuri kabisa kwa uwazi, kwa hiyo hili sisi tunafikiri Serikali itaifanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine baada ya kuangalia majukumu ya *NBAA* yanayofanywa tumeona kwamba *NBAA* ina kazi nyingi sana; kwanza kazi yake ni kuhakikisha inatengeneza *standards* za kusimamia taaluma ya uhasibu na *standards* hizi ziko nyingi sana sasa hivi, ziko za biashara, ziko zile za mashirika ya umma na taasisi za umma ambapo wanatengeneza, wanachukua za kimataifa, wanazi-*modify* wanahakikisha zina-*fit* katika mazingira yetu, lakini pia wanalojukumu la kusimamia wana taaluma wote; lakini tatu wanalo jukumu la kuhakikisha kwamba wanahakikisha taaluma hii nidhamu na maadili ya taaluma yanazingatiwa katika utekelezaji wa majukumu; lakini zaidi ya hapo wanasimamia katika kutoa elimu na ujuzi kwa wahasibu hawa ili kusudi waweze kupata maarifa ya kutosha na kuweza kutekeleza majukumu yao sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi ya hayo kutoa huduma kwa wanachama mbalimbali, lakini lipo jukumu lingine kubwa wanatakiwa kupitia ubora wa ripoti zote za ukaguzi zilizofanywa na makampuni mbalimbali na wataalamu mbalimbali (*Audited Financial Statement*). Sasa tunaona haya majukumu yalivyo ni mengi na ni makubwa, wewe mwenyewe ni *regulator*, halafu wewe mwenyewe ndiyo mwendeshaji na msimamizi, kidogo inakinzana, kwa hiyo, sisi kama Kamati tumeliona hilo na tumeshauri kwamba Serikali ione haja ya kuanzisha taasisi nyingine ambayo itasimamia baadhi ya majukumu *oversight board* tumependekeza kuwe na *oversight board* ambayo inaweza ikasimamia ubora wa taarifa za kiukaguzi zitakazokuwa zinafanywa (*Audited Review Financial Statement*) zile *review* waka-*review* na kupitia italeta ubora na tutaweza kufikia

viwango vile ambavyo vinatambulikana kimataifa na tukasema *NBAA* pia inaweza ikashirikiana katika hiyo *oversight board* na ika-*provide* hata Sekretariet kiasi kwamba wakaweza kutekeleza majukumu sawasawa. Kwa hiyo, hili tumeona kwamba ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni suala la utoaji wa elimu, kwa sababu sasa hivi kama ilivyo katika maeneo mengi na wahasibu wengi pamoja na wakaguzi wa mahesabu wengi wanakuwa na taaluma ile ya madarasani wamefaulu mitihani, wanavyo vyeti, lakini ikija kwenye uhalisia wa kufunga mahesabu imekuwa ni changamoto kubwa na hili hasa tatizo ni kubwa zaidi kwenye upande wa taasisi za umma. Serikalini huko ambako unakuta kwamba mtu anapangiwa kaeneo kamoja tu ikija kufunga mahesabu ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi sisi tumesema na Kamati imependekeza na Serikali imekubali nashukuru wamekubali karibu mapendekezo mengi ambayo tumeyaleta, kwamba kuwe na ushirikiano wa dhati kati ya vyama vya kitaaluma na *NBAA* na kwa mara ya kwanza sasa sheria kwa mabadiliko haya kama yalivyokubaliwa japo sijaona ile *schedule of amendment* humu ndani, lakini nafikiri tulivyokubaliana na Serikali kuwe sasa na itamke kuwe na mahusiano na ushirikiano na vyama vya kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vyama vya kitaaluma kama Chama cha Wahasibu Tanzania (*TIA*), lakini kimesajiliwa kama ni chama cha hiari, kuna Chama cha Wahasibu Wanawake Tanzania, lakini kuna Chama cha Wahasibu Zanzibar, vyote vinashirikiana. Sasa tukafikiri kwamba ifike mahali sheria hii ivitambue hivyo vyama, washirikiane na *NBAA* katika kutoa mafunzo na elimu kwa wahasibu wetu na wakaguzi ili wapate weledi wa kutosha na kuweza kutekeleza majikumu yao kama inavyotakiwa na ili nashukuru Serikali imekubali na ninaamini kwamba mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo lingine kulikuwa na pendekezo ambalo limeletwa na Serikali

kwamba sasa mhasibu yule mkaguzi wa mahesabu akishakagua hesabu anatakiwa achukue ripoti yake apelike *NBAA*, halafu sisi tukasema kidogo hili lina mvutano kwa sababu linaleta mushikeri kwa sababu huyu yeye ni mkaguzi, amekuwa *engaged* na *client*. Sasa kuchukua ripoti ya *client* kwenda kuipeleka *NBAA* ina-*breach ethics* za makubaliano. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tukasema hilo lingeangaliwa, lakini baadae tulikubaliana na Serikali tukasema basi kwa sababu sasa hivi tulitaka kwamba kwenye vitabu anayekuwa *charged* na jukumu ni Bodi ya Wakurugenzi, lakini tukaona kuiweka Bodi ya Wakurugenzi kwenye Muswada wa Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi itakinzana na sheria zingine zinazoitambua, kwa mfano *Companies Act* na sheria zinazozungumzia Bodi ya Wakurugenzi, kwa hiyo, tukaiacha hivyo hivyo tukasema kwamba ibaki kama mapendekezo yalivyo, huyu mkaguzi akishamaliza kukagua *Audited Financial Statement copy* yake aipeleke kule anaposimamiwa na taaluma ili taaluma kama kukiwa na mushikeri mtu yeyote akitaka kufanya *reference* anaweza kufanya *reference* pale, lakini anaweza pia ikapitiwa na kuangaliwa ubora wa hiyo taarifa na wanataaluma wenzake. Kwa hiyo, hilo nafikiri tumelipendekeza na tumeona ni zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, na niseme kama alivyosema Mheshimiwa Kigwangalla kwamba labda tunakizana kuanza kutengeneza vitabu vingi. Hatuwezi kujenga Taifa ambalo tunatengeneza vitabu viwili/vitatu ambavyo havifanani, kitabu lazima kiwe ni kimoja taarifa zinazokwenda *TRA*, zinakwenda *NBAA*, zinazokwenda kokote lazima zifanane ili Taifa ambalo tunasema liwe unatengeneza vitabu vitatu, sijui vingapi hilo litakuwa ni Taifa la ajabu. Kwa hiyo, mimi nafikiri mabadiliko haya tunayokwenda kuyafanya ni mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna pendekezo ili la *assets* kwamba taasisi yoyote ikiwa na mali zinazofikia thamani ya shilingi milioni 700 basi au kama wana mauzo *turnover* ya shilingi milioni 500 waajiri mhasibu

anayetambuliwa, mimi nafikiri hili ndiyo tumekubaliana. Mapendekezo ya awali yamesharekebishwa ndiyo tumefikia sasa kwa milioni 500 kwenye *turnover* na milioni 700 kwenye mali za Serikali naamini hiyo itasaidia sana katika kuhakikisha tunaboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja naomba Wabunge tuiunge mkono sheria hii ipite bila tatizo lolote. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, mtoa hoja ajiandae.

MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea maboresho haya na Serikali, haya ni maboresho muhimu sana na nipongeze Kamati kwa maoni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja ukurasa wa sita kifungu cha 6(1) *actually* ni kifungu cha 5(1) kwa mujibu wa muswada; *the principal Act is amended by repealing section 6*; pale *section 6* inasema kwamba; *the Minister shall appoint the Executive Director of the Board on such terms and conditions as he may determine*. Napendekeza badala ya neno *as he may determine* tuweke *as per public service guidelines*.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine kifungu cha 6(2)(d) inasema kwamba wale watu watakaochaguliwa pale kwenye (d) *has at least ten years work experience out of which, eight years being in managerial position*. My question is *has at least ten years work experience; which experience? I think it should experience on the relevant field*, kwa sababu mwingine anaweza akawa *ten years experience but experience ya lawyer and not as accountant*, so kama wataalamu wa uandishi wanaweza wakaangalia *at least ten years work experience may be on the relevant field*, isiwe open.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine sana sana napongeza kwenye *sanction* na *penalty* ndiyo nita-*focus* sana, naenda ukurasa wa 10 wa muswada ambapo ukurasa wa 10; *oh my God*, kuna *page* nyingine haijatoka *page nine*, ukurasa wa 10 hapa kifungu cha 11 cha muswada ambacho kina kinazungumzia *establishment of accounts and auditors; section 24* kwamba; *there is hereby established an appeals board to be known as Accountants and Auditors Appeal Board which shall consist of*; pale kwenye (b) yake kuna (i), (ii), wameelezea *a lawyer, a law officer, one senior member from Ministry responsible for finance, one senior member from Bank of Tanzania and one senior member from TRA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza hapa baada ya (b)(v) kuwepo *immediately adding (vi)* ambayo itasema hivi; *“The Minister shall have regard to the gender balance,”* kwa sababu hawa wanaoingia *by virtual of their post sometimes* wote wanaweza wakawa “me” au “ke,” kwa hiyo tuongeze tu pale (b) itakuwa (vi) baada ya (v) mapendekezo yangu. *Minister shall have regard to the gender balance at all times the number of female members shall not be below two, it can be three, four but not below two.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante eneo lingine ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Pindi Chana umepeleka marekebisho? Umepeleka Jedwali la Marekebisho?

MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali lilikuwa linachapwa, sijui kama litawahi. (Kicheko)

NAIBU SPIKA: Haya endelea na mchango wako.

MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nadhani watu wa *printer* wanaweza wakananilli, haya ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ukurasa huo, huo *section 12*, hiki kifungu cha 12 naipongeza sana Serikali

kutuletea haya marekebisho, kwamba hiki Kifungu sasa kinafutwa, kwa kweli nitumie nafasi hii kupongeza, lakini pia kwa ruksa yako nitumie nafasi hii kukumbashana kwamba hata kama hapa mwisho ilisema; *“and shall not be subject to review by any court.”* Kwa mujibu wa Katiba kwamba Katiba ni sheria mama hata kama hiki kifungu kilikuwepo haizuii mtu kwenda Mahakamani kudai *rights* zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hata kama kilikuwepo mtu ana *rights* zake Mahakamani kwenda ruksa. Kwa sababu tunajua nini maana ya Katiba, lakini napongeza kabisa kifungu hiki kufutwa, lakini haki ya wananchi ilikuwa haijazuiiwa, walikuwa wana haki kwenda kudai *their right in any court* kwa sababu wanakwenda kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haraka, haraka kule kwenye vifungu ukurasa wa 12, *section 16*, ninaposoma mimi *section 16* pale kuna 16(b)(6)(a) inasema; *“in the case of an individual person, to a fine not exceeding ten million shillings or to imprisonment for a term not exceeding two years,”* naona kama *minimum sanction* haipo, kwa hiyo naomba tu wataalam watuwekee *minimum*. Naona hapa kuna *maximum, minimum* haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine pale 17(6)(a) *in the case of individual personal to a fine not exceeding ten million shillings or imprisonment for a term not exceeding two years* naona kama *minimum* haipo, tuweke *minimum*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ukurasa wa 13, *section 18(d)* nadhani hiki kifungu sijui kimeondolewa, kuna maneno yapo pale sikuwa nimeyaelewa, haya maneno yanasema hivi (d) *in sub-section (2)(b), by deleting the words...*, kwa hiyo napongeza kwa sababu haya maneno yalikuwa hayajaeleweka na Waziri ametuletea yawe *deleted; fifty thousand million shillings* nikawa sijaelewa, *fifty thousand million*, lakini ndiyo yanakuwa *deleted* yaani ndiyo inaboreshwa hivyo, pongezi zangu zipo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, enelo lingine ukurasa wa 14, kifungu cha 30B(3) *page 14*; “A person who refused to produce further information under this section, commits an offence and shall, on conviction, be liable to a fine not exceeding twenty million, minimum haipo, au tunaenda na maximum bila kufunga chini kwamba Hakimu, Jaji ataamua kama ni shilingi kumi, shilingi ishirini, thelathini, laki au ni vizuri kufunga na chini *not less than*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine nitaji-focus sana kwenye masuala ya *fine*. Ukurasa wa 15 hiki ni kifungu cha 30C *maximum fine* ipo, *minimum again* haipo. Hiyo ni 30C(2); *A registered member who refused to provide information or clarification sought under this section commits an offence and shall, on conviction, be liable to a fine of not exceeding five million shillings or to imprisonment; minimum haipo na hii sheria inarekebisha sana maboresho haya.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 16 kifungu cha 40, napongeza kifungu cha 23 kina *amend* kifungu cha 40 *annual performance* ambapo kifungu cha 40(2) inasema na nianze na 40(1) *The Board shall prepare and submit to the Minister within four months after the close of each financial year the annual report on the performance of the Board during the financial year. (2) The Minister shall, at the earliest available opportunity, cause a copy kuwa submitted before the National Assembly.*

Je, kuna haja ya kuweka muda au tuache *earliest available opportunity*. Tunaweza tukakopa ile ya juu *within four months* na yeye akipokea *within four months* ailete Bunge maana *within four months* lazima kuna kikao cha Bunge, lakini itategemea kama ni cha bajeti au cha Miswaada *any way* ndiyo najjuliza tu kuna haja ya kuweka muda.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya kwanza au ya pili?

NAIBU SPIKA: Ya pili.

MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite mtoa hoja ili aje ahitimishe hoja yake. Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, uje uhitimishe hoja yako.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuweza kuhitimisha hoja hii na nianze kwanza kwa kukushukuru kwa kuendesha vizuri mjadala huu na niwashukuru Wajumbe wa Kamati wakiongozwa na Mwenyekiti ambapo wametoa maoni kuanzia kwenye Kamati na hapa ambapo Mwenyekiti amewasilisha vema na kuweka wazi kwamba kwa kiwango kikubwa karibu yote tulishakubaliana kati ya Serikali na Kamati na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwenye hii hoja na kuhitaji baadhi ya maeneo yawekewe ufafanuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikuombe niende moja kwa moja kwenye baadhi ya maeneo ambayo yangehitaji ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na haya machache aliyoyasema Dkt. Pindi Chana ambayo ndiyo yapo hapa mwishoni mwishoni, kwenye eneo lile ambalo anaongelea kuhusu *terms and conditions as he may determine* akiwa anaelezea kwa maana hiyo Waziri na sisi Serikali tulishalionana na kwa ajili ya muda tumeweka baadhi ya marekebisho. Kwa hiyo, tukubaliane na yeye marekebisho ambayo anayaandaa yaendane na ya kwetu ambayo tumeshayaandaa kwa mujibu wa *Hansard* iweze kusomeka *subject to sub-section (2) the Minister shall appoint the Executive Director on the Board in accordance with the Public Service Act, on such terms and condition as provided for in*

the scheme of service; ambapo itakuwa imeshaondoa ile dhana ya kwamba atakavyoona inafaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kile kipengele cha pili ambacho kilikuwa kinaongelea *which working experience*, Mheshimiwa alichokuwa anakisema kina mantiki kwamba ni *experience* ipi, lakini Serikali tulikuwa tunaona iendelee kuwa vile kwa maana ya hii *working experience* ambayo tumeliandika hapa ni nyongeza ya zile sifa sasa ambazo Mheshimiwa Mbunge amezisema kwamba ni vizuri zikawepo. Kwa maana hiyo hii *working experience* tuliyoiweka ina-*supplement* zile sifa sasa za *field* yake kwa sababu hapo juu tumeshataja (a) *awe holder of at least Master Degree in Accounting, Finance, Management and Economics; has an accountancy professional qualification obtained from recognized institution; is a registered* hapo kwa mujibu wa *gender sensitivity he or she is registered by the board as a Certified Public Accountant or Certified Public Accountant in Public and Practice*. Sasa hii inaongezea hizi sifa kwa hiyo tukizichukua tena hizi sifa ziwe hapa tulikuwa tunaona inaweza ikawa ina *repeat* kwa sababu *already* huyu mtu tunayemuongelea tunasema awe na hizo sifa hapo juu. Halafu tukasema basi kwa sababu anaenda kwenye menejimenti awe pia sasa na nyongeza ya *working experience* katika *level* ya menejimenti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo alilisema Mheshimiwa Mbunge ndugu yangu aliyekuwa anaongelea kuhusu pande mbili hizi za Muungano, haya masuala ya pande mbili za Muungano yanakuwa *guided* na miongozo pamoja na sheria inayoongelewa kama ni ya Muungano au laa. Kama sheria si ya Muungano kwa vyovyote vile sheria itakayotawala utaratibu wa utungaji ama marekebisho lazima yafuate utaratibu huo.

Kwa maana hiyo jambo hili kwa kuwa si la Muungano tusingeweza kushirikisha upande mwingine kama ambavyo Mheshimiwa Hasunga ameliweka vizuri, taratibu zinazotegemewa hadi sasa ni kwamba wenzetu wa upande wa pili wa Zanzibar na wenyewe watapita hizi hatua, tunajua,

lakini taratibu hizo zikiwa zimeshafanyika na ambavyo ilikuwa ikitumika kutakuwepo na kusaini *MoU* kwa ajili ya makubaliano ya namna ya kushirikiana ili watu ambao watakuwa *certified* upande wa huku ama *certified* upande wa pili wa Muungano ile *certification* iweze kutambulika katika hizo pande zote mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kabla ya sheria, *administrative measure* zitaendelea kufanyika za *MoU* za mashirikiano na kwa sababu hii nchi ni moja na Muungano wetu ni wa kindugu hili jambo mpaka sasa wameweza kuwa wanafanya hivyo na baada ya taratibu za aina hii kufanyika pia upande wa pili wa Muungano mashirikiano haya yataendelea kufanyika ili *certification* hizi ziweze kutambulika pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ilikuwa imetolewa ambayo ilikuwa inahusisha aliisema Mheshimiwa Salome iliyokuwa inahusisha wajumbe wale wawili kama Waziri asiwateue kutoka sehemu yoyote, jambo hili tulishakubaliana kwenye Kamati na kwenye marekebisho tumeweka na nadhani kile tulichokiweka tulishasema moja atoke kwenye *higher learning institution* na wale wawili watoke kwenye *association* hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge alikuwa anazisema na tukaongeza pia kwamba au kwenye *private sector* kwa sababu pia tunaweza tukapata *experience* hiyo ya wale ambao wameshafanya na kazi katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile lingine ambalo alikuwa analisema Mheshimiwa Kigwangalla moja kama alivyosema Mheshimiwa Hasunga moja tayari tumeshakubaliana kwenye Kamati vile viwango tumeshaweka kwenye *turnover* milioni 500 na kwenye *assets* tulishaweka milioni 700.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize kimoja tu, *essence* ya kuwa na wahasibu katika taasisi zetu hizi na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla anasema tusifungue chungu kilichokuwa kimefungwa zamani, kuna umuhimu mkubwa sana wa watu

wetu kuanza kuwa *oriented*, kuelekezwa namna ya kuendesha hizi shughuli kwa njia za kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifuatilia kuna maeneo mengi watu wetu wanaumizwa katika hatua fulani, fulani hivi kutokana tu na kwamba hawatunzi kumbukumbu na wengine wengi kwa sababu hawakutunza kumbukumbu huwa wanaridhika tu kumia na hatambui kama ameumia kwa sababu kumbukumbu hazikuwepo. Sana sana tu unakuta anaona kikubwa kile anachoonna anakadiriwa kwa sababu hata hivyo hana cha kulinganisha nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo tunakokwenda kama alivyosema Mheshimiwa Hasunga ni vizuri watu wetu wakaanza, kadri biashara zinavyoanza kutengemaa, zinavyoanza kuwa rasmi, ni vizuri sana wakaanza kutunza vizuri mahesabu yao kwa sababu itawaepusha kwenye kuonewa na itawaepusha kwenye kumia na biashara nyingine unaweza ukakuta hazikui kwa sababu kile kinachokadiriwa huenda kikawa siyo sahihi kwa sababu kumbukumbu iliyo sahihi haipo. Kwa maana hiyo sisi bado tunaona ni vyema sana watu wetu wawe *oriented* kwenye kutunza kumbukumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge na tulikubaliana na Kamati kuhusu viwango vile kuwa vidogo sana kwamba tutakuwa tumewaweka kwenye gharama hata wale ambao biashara zao bado ni ndogo. Lakini biashara zikishakuwa rasmi, kama ambavyo Mheshimiwa Hasunga amesema ni vizuri sana watu wetu wakaenda kwenye utaratibu ulio rasmi ili kuweza kutunza kumbukumbu vizuri na pia kwenda kwenye ile *essence* ya hoja aliyoisema Mheshimiwa Rais ya watu kulipa kodi iliyo halali, mtu alipe kile anachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kuna baadhi ya maeneo, siyo mengi lakini yapo, kuna baadhi ya maeneo, hata mwananchi anapolalamika kuna wakati unashindwa umsaidiaje kwa sababu hata yeye ukimuuliza kumbukumbu zake zinasemaje, anakuwa hana. Kwa hiyo, unakuta

umetumika tu uzoefu, ama mtazamo, ama kumbukumbu za hisia kwamba mwaka fulani aliwahi kufanya hivi, mwaka fulani akafika hapa, basi ndiyo inajengwa *trend* ambayo huenda ikawa si sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nitoe rai watu wetu tukubali kwenda kwenye mifumo hii iliyo rasmi kwa sababu ndiyo tutakuwa tunakwenda kuwa rasmi na tutaweza kutunza kumbukumbu zilizo sahihi na si vyema sana na si uungwana kuwa na maisha ya kudanganya danganya kila wakati, yaani unapoulizwa na benki unatoa namna hii, unapokuja kukaguliwa na upande mwingine tena unatoa hesabu zilizo namna nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla alikuwa anasema kwamba wazee wetu waliyaona hayo na wakaacha hivyo hivyo, tunakokwenda ukiweka na kukua kwa teknolojia, mifumo mingi itakuwa inakwenda inasomana. Kwa hiyo, kuna watu siku zinazokuja kule mbele anaweza akakosa mkopo kwa vile tu kuonekana takwimu anazopeleka ni za kudanganya na moja kwa moja akaonekana huyu kumbe ana asili ya udanganyifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunakokwenda biashara zikiwa zinafanyika vizuri na mifumo hii inasomana, ni vizuri tuwe na kumbukumbu ambazo ziko sawa na ndiyo zitakuwa zinamtambulisha mtu huyo na zitakuwa zinaitambulisha biashara hiyo na hakuna ukaguzi unaoweza kumpeleka hatiani kama hizo ndiyo kumbukumbu zinazosomeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo hili nilikuwa nalisisitiza hata watu pia wanapofanya manunuzi, siyo busara, wala uungwana, wala uzalendo kwenda kuuliza bei mbili, kwamba kitu hiki nipe bei isiyo na risiti ya *TRA* au nipe yenye risiti. Bei iwe moja tu ile ile kwamba ina risiti ya Mamlaka ya Mapato ya *EFD* ambayo ina-*include* pamoja na kodi zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo tukirasimisha haya masuala ya biashara na kumbukumbu

zake zikawa zinatunzwa vizuri itatusaidia kuondokana na baadhi ya migogoro ambayo inajitokeza inayohusisha uonevu, lakini pia itatuweka mahali pazuri sisi pia hata kama Serikali kwenye upande wa kuweza kukadiria.

Sasa hivi makadirio yanakwenda yakiwa hayatabiriki kwa sababu kumbukumbu katika baadhi ya maeneo zinaweza zisiwe zimenyooka.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Wabunge wote waliochangia na niombe kama kuna eneo moja sijalitaja mridhie tu kwamba tumeshaweka kwenye mabadiliko, kwa hiyo, kuna baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge mmechangia, tumeshaya-include kwenye mabadiliko yetu haya ambapo mabadiliko mengi pia tulishakubaliana na Kamati ambao ni wawakilishi wa Bunge katika mjadala huu tuliokuwa tunaufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya na kwa sababu tutakwenda pia kupitia eneo moja baada ya lingine, kama kuna eneo nitakuwa pia nimeliacha pembeni basi tutapitia pia pale tukumbushane kile ambacho tutakuwa tulishakubaliana kwenye Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tutaendelea sasa na utaratibu wetu. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa
Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021
(*The Accountants and Auditors (Registration)
(Amendments) Bill, 2021*)**

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tukae. Katibu.

Waheshimiwa Wabunge, kuna marekebisho ya jumla ambayo nalazimika kuyasema hapa ili niwe nimewahoji kwa ujumla wake.

Katika marekebisho yaliyoletwa na upande wa Serikali, wanapendekeza kufuta maneno kwenye muswada wote; maneno *gross revenue* popote yanapotokea na kuyaweka maeneno yafuatayo; *gross audit fee*. Kwa hiyo wanafuta maneno *gross revenue* popote yanapotokea kwenye muswada na kuweka maneno *gross audit fee*.

Sasa kwa sababu vipo vifungu ambavyo katika marekebisho haya ya Serikali havijaguswa kimoja kimoja, lakini vitakuwa vimeguswa na maneno haya, nalazimika kuwahoja kwa maneno haya kwanza halafu ndiyo tuendeleo na vifungu vingine.

*(Marekebisho ya Serikali yalipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima)*

MWENYEKITI: Katibu.

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 5
Kifungu cha 6

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 7

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kifungu namba 7 kuna kifungu kipya cha nane kimeongezwa.

Kifungu Kipya cha 8

(Kifungu Kipya kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 11

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13

Kifungu cha 14
Kifungu cha 15

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 16

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 17

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 21
Kifungu cha 22

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 23

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 24
Kifungu cha 25

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 26

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 28

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *rearrangement*, kwa hiyo tunakwenda mpaka kifungu namba 28.

MWENYEKITI: Haya, baada ya kuongeza kifungu namba 8 ambacho tulishawahoji ili kuweze kuongezeka kupitia marekebisho ya Serikali, kutakuwa na mabadiliko ya namba za hivi vifungu. Kwa hiyo kifungu cha mwisho kitakuwa ni 28 kitakapobadilishwa.

Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa hoja, Taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021

(The Accountants and Auditors (Registration) (Amendments) Bill, 2021) kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja lilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana. Sasa nitawahoji.

(Hoja lliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Nadhani walioafiki wameshinda.
(Makofi)

Sasa kwa utaratibu wetu nitamuita tena Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamebainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hiyo *(A Bill for an Act to Amend the Accountants and Auditors Registration Act in order to address some challenges which were encountered during its implementation)*.

(Kusomwa Mara ya Tatu)

(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 (The Accountants and Auditors (Registration) (Amendments) Bill, 2021) Ulipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii tumeshafika mwisho wa hatua zinazotakiwa katika utungaji wa sheria kwa upande wa Bunge, na sisi tumekamilisha zoezi hilo baada ya Katibu kutusomea muswada huu kwa mara ya tatu.

Sasa utaelekea kwa Mheshimiwa Rais ili aweze kutoa kibali chake ili muswada huu uwe sasa sheria kamili kwa mujibu wa taratibu ambazo Katiba yetu inatuelekeza na kwa hiyo niseme Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 (*The Accountants and Auditors (Registration) (Amendments) Bill, 2021*) umepitishwa na Bunge rasmi, utasubiri kibali cha Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nitumie fursa hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango na timu yake yote kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuipitia sheria hii na kuona ina maeneo mbalimbali kulingana na nchi yetu namna tulivyoendelea na hatua tuliyofikia kwamba inahitaji marekebisho hapa na pale. Tunawapongeza sana na tunawashukuru kwa kuliona hilo.

Lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Hesabu za Serikali pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kufanya kazi nzuri ambayo kama Serikali ilivyosema hapa ndani kupitia Waziri wa Fedha na Mipango, amekiri michango mingi iliyotolewa na Kamati, ushauri uliotolewa na Wajumbe wa Kamati hii Serikali imeuzingatia na huo unakuwa ni kuonesha kwamba Serikali ni sikivu, inaelewa kwamba shughuli ya kutunga sheria ni ya Bunge, na ninyi kama watu ambao mmefanya kazi kwa niaba ya Bunge mmefanya kazi nzuri, tunawapongeza sana kwa marekebisho mbalimbali ambayo mmehakikisha sheria hii inayachukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri kama ambavyo Wabunge imetokea hapa walikuwa wanachangia pia mambo mengine ambayo pengine hayapo kwenye sheria hii, ni ushauri tu wa jumla kuanza kuangalia sasa namna ambayo

marekebisho ya sheria yatakuwa hayasubiri muda mrefu namna hiyo kwa sababu Bunge lipo miaka yote, hakuna haja ya kusubiri muda mrefu kwa yale marekebisho ambayo yanaendelea. Kama ambavyo nchi yetu inapitia mabadiliko ya maendeleo mbalimbali kwa hiyo kuna haja ya kuendelea kuangalia maeneo ya maboresho kwenye sheria yetu hii lakini pia na sheria nyingine hapo baadaye ikiwa ni pamoja na kuzingatia ushauri wa Kamati kwa yale maeneo ambayo inaona kwamba mmeshakubaliana kufikia hatua fulani, lakini pengine wangependa muende hatua kubwa zaidi. Kwa hiyo, naamini kwa hapo baadaye mtaangalia huo uwezekano wa kwenda hizo hatua nyingine ambazo ni kubwa zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, ninayo matangazo matatu hapa; kwanza ni tangazo la nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. Mheshimiwa George Boniface Simbachawene ndiye atakayekaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaporejea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika amepokea hiyo taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo Dodoma na kwa hiyo, nafasi yake ya Ukuu wa Shughuli za Serikali Bungeni imekaimishwa kwa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mkimuona amekaa pale wale ambao mna changamoto zinazomhitaji Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni kusogea pale inaweza ikawa mtihani kwa sababu kile kiti hakitakiwi kukaliwa na mtu yeyote, lakini unaweza ukamuona kwa muda wako. Unaweza ukapeleka hapo na yeye atayafikishwa huko yanakotakiwa kwenda. Kwa hiyo, tunakupongeza sana Mheshimiwa Simbachawene kwa kuaminiwa kukaimu nafasi hiyo kubwa kabisa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati tukianza kipindi chetu hiki cha Bunge siku ya leo nilitangaza kuhusu Tamsha la Michezo kati ya *Bunge Sports Club* na Benki ya *NMB*, hapa tumeongezewa taarifa za ziada kwamba Waheshimiwa Wabunge kwanza fulana kwa ajili yetu sisi sote Wabunge ziko

tayari. Tunapotoka hapa tutakuwa tukizipata pale kwenye lango kuu, kila Mbunge apite hapo apate fulana yake kwa ajili ya matembezi hayo kesho asubuhi. *(Makofi)*

Kwa hiyo ukishapata fulana tunakutarajia uje katika fulana hiyo ya *NMB* ukiwa umependeza kabisa tayari kwa kumpokea mgeni rasmi ambaye ndiyo nataka nintangaze hapa.

Mgeni rasmi wa jambo hili zito la michezo kati ya *Bunge Sports Club* na Benki ya *NMB* atakuwa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, ndiye atakayetuongoza katika matembezi hayo kesho. *(Makofi)*

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, muwahi kabisa hapo, asiwepo mtu atakayekuwa amezuiwa wakati msafara wa Makamu wa Rais ukija hapa. Kwa hiyo tuwahi, saa kumi na mbili kila mmoja awe amefika hapo ili Makamu wa Rais anapokuja basi atukute sisi wengine wote tumejipanga tayari kwenda naye kwenye viwanja vya Chinangali. *(Makofi)*

Taarifa nyingine nilizozisema asubuhi zinaendelea vilevile, lakini wale ambao hawakupata fursa ya kujifua asubuhi basi wana muda jioni hii wakajifue, maana kesho wakati wa zawadi hakuna kupokeleana, anapokea aliyeshinda na nilikuwa namsikiliza hapa naona Mheshimiwa Ester Bulaya amejipanga kupata medali ya dhahabu kwenye mbio, sijui amejipanga kiasi gani, lakini tumtakie kila la heri. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge, baada ya shughuli ile ya kesho ambayo Mheshimiwa Spika aliagiza jana sote tushiriki, hiyo ya *Bunge Sports Club*, keshokutwa siku ya Jumapili, tarehe 05, Septemba, 2021 tutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu chanjo ya Ugonjwa wa UVIKO-19 itakayofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa tano asubuhi.

Semina hii inaratibiwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria semina hiyo muhimu ili tuweze kusikiliza wataaam wetu wanasemaje, na sisi kama tunayo mapendekezo au maswali yoyote kuhusu jambo hili basi inatupa fursa tukihudhuria.

Kwa hiyo nirudie tena, muda ni saa tano na ninyi mnafahamu siku hizi vikao vyetu havichelewi, vinaanza kwa muda. Kwa hiyo, semina hii itaanza saa tano kamili siku ya Jumapili, Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyokuwa nayo hapa Mezani.

Baada ya kusema haya naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa nane kamili mchana.

(Saa 11.25 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 6 Septemba 2021, Saa Nane Mchana)